# ULINGANIFU WA TAARIFA ZA HABARI: TATHMINI YA TAFSIRI KUTOKA KISWAHILI HADI KIKIPSIGIS KATIKA KITUO CHA KITWEK

**KIMETTO HILLARY KIMUTAI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2016**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu chochote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.

……………………………… ………………..………

Sahihi Tarehe

KIMETTO HILLARY KIMUTAI

C50/67011/2013

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tulioteuliwa kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo kikuu.

……………………………… …………………………

Sahihi Tarehe

DKT. ZAJA OMBOGA

Msimamizi-Chuo Kikuu cha Nairobi.

……………………………… …………………………

Sahihi Tarehe

DKT. PRISCA JERONO

Msimamizi-Chuo Kikuu cha Nairobi.

## TABARUKU

Kazi hii namtabarukia marehemu dadangu **Salome Chepkorir**. Kifo chako kilijiri siku moja baada ya kukamilisha kwangu kuandika tasnifu hii.

## SHUKRANI

Kazi hii ni tokeo la mchango wa wahusika mbalimbali wanaostahili shukrani tele. Kwanza kabisa, shukrani zinamwendea Mwenyezi Mungu kwa kunijalia busara ya kuwazia kurejea chuoni ili kuendeleza masomo yangu zaidi. Kuwazia na kuanza masomo hakuleti manufaa yoyote kama mtu atakosa nguvu na ukakamavu wa kuyakamilisha. Mambo haya mawili niliyapata kutoka kwa Mungu ndiposa nashadidia shukrani kwake.

Pili, natoa shukrani zangu kwa wasimamizi wangu Dkt James Zaja Omboga na Dkt Prisca Jerono ambao walibadilishana usukani katika safari iliyofikia hatima ya tasnifu hii. Mseto wa ujuzi wa Dkt Zaja katika masuala ya tafsiri pamoja na umilisi wa Dkt Jerono wa lugha zinazohusika katika mada ya tasnifu hii ulichangia kuzalika kwa kazi hii ambayo ina upekee wa aina yake. Mungu awakirimie ari ili mwendelee kuwafaa wengine zaidi.

Tatu, nawashukuru wahadhiri wangu walionifunza kozi mbalimbali kama Prof Mwenda Mbatia, Prof Kineene wa Mutiso, Prof John Habwe, Dkt Iribemwangi, Dkt Jefwa Mweri, Dkt Zaja Omboga, Dkt Prisca Jerono, Dkt Amiri Swaleh na Dkt Mbuthia. Mlitupa ujuzi na lukuki ya maarifa kupitia mafunzo na ushauri ambao tulipotilia maanani tukalisukuma gurudumu la uzamili hadi ukingo uliokuwa kama mazigazi katika siku za awali.

Nne, nawashukuru wenzangu tulioabiri pamoja treni ya uzamili. Wao ni Chesebe (Shujaa wa Kibukusu), Kihara, Misheck, John Bosco, Kevin, Mangistu, Saar, Polycarp, Jared, Mogusu, Mwangi, Roy, Florah, Winfred, Jackline, Agnes, Asha, Sylveria, Adeline, Caroline, Wangeci, Lilian, Florence, Gitonga, Nyambeki, Kemunto, Emily, Bosiori na Njeri. Masihara yenu yalifanya safari iwe na mvuto, tukapumbazika kuona ikiwa fupi.

Tano, ninamshukuru Bw Weldon Orioop Kirui, mtangazaji wa Shirika la Utangazaji la Kitaifa (KBC) kwa kuniauni kupata miswada ya taarifa za habari kutoka idhaa ya Kiswahili na tafsiri zake katika Kikalenjin kutoka idhaa ya Kitwek. Kila mara nilipohitaji miswada ya tarehe yoyote niliyoichagua ungehakikisha umenisukumia kupitia anwani ya

barua pepe kwa muda mfupi kama inavyowezekana. Mungu akumiminie baraka chungu tele.

Sita, natoa shukrani kwa wazazi wangu, marehemu babangu Stephen Cheruiyot na mamangu Esther Cheruiyot. Malezi yenu yamenifikisha hapa nilipofika, nami bado nalenga mbele. Mliwekeza katika elimu, nikawa faida ya uwekezaji huo. Kwa marehemu shangazi yangu Alice Tele (Obot Esther), kauli zako nilipokuwa katika shule ya msingi kwamba nisome 'hadi nifike Nairobi' ni ndoto ambayo imekwisha kutimia. Nimefika tayari.

Saba, shukrani zangu za dhati zimwendee mke wangu mpendwa Gladys Kimetto na wanangu Lawrence Kibet na Benedict Kiprono. Mlinipa idhini niwe mbali na nyumbani mara nyingi nilipohudhuria masomo chuoni, nanyi mkaingiwa na ukiwa ambao mlistahimili hadi nilipokamilisha shughuli hii ya kipekee. Pia ipo miradi ambayo ilisitishwa kwa muda ili tuelekeze raslimali masomoni. Nawashukuru kwa hilo.

Nawashukuru walimu wenzangu wa shule ya upili ya wasichana, AIC Litein, wakiongozwa na mwalimu mkuu Bi. Betty Chepkwony. Mlinitia motisha ya kukamilisha kazi hii kwa muda mfupi kama inavyowezekana. Mlinisisitizia kwamba sehemu ya kiusomi niliyoichagua ilikuwa mwafaka zaidi kwangu kuliko yoyote nyingine; mbeleni nikachukulia mlikuwa mkinivisha kilemba cha ukoka lakini nimetanabahi kwamba mlikuwa mmebaini hivyo.

Mwisho, japo si wa mwisho katika umuhimu, natoa shukrani kwa Lily Chepkemoi aliyepiga chapa sura ya kwanza ya tasnifu hii kisha akanielekeza kuhusu namna ya kuendeleza sura zilizosalia. Kwa hakika kuna wengi waliofanikisha kazi hii ambao kuwataja kwa majina kutaibusha tasnifu nyingine kamili. Kwa sababu hiyo, naomba mniruhusu niwashukuru kwa jumla na kuwaombea thawabu. Nasema kwenu: Asante.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| HC | Hadhira Chanzi |
| HL | Hadhira Lengwa |
| KBC | Kenya Broadcasting Corporation |
| Kiamb | Kiambatisho |
| LC | Lugha Chanzi |
| LL | Lugha Lengwa |
| MC | Matini Chanzi |
| ML | Matini Lengwa |
| Rej | Rejelea |
| TH | Taarifa za Habari |
| UM | Ulinganifu wa Maana |

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza ulinganifu wa taarifa za habari zinazotafsiriwa kutoka Kiswahili hadi Kikipsigis, mojawapo ya lahaja za Kikalenjin, katika kituo cha redio cha Kitwek ambacho ni kitengo cha Shirika la Utangazaji la Kitaifa (KBC). Utafiti huu ulichochewa na udadisi tuliofanya katika shirika hili ambao ulibainisha kwamba habari zinazosomwa katika kituo cha Kitwek ni tafsiri za zile zinazosomwa katika idhaa ya Kiswahili ya KBC. Utambuzi huu ulitupa mshawasha wa kuchunguza ulinganifu wa taarifa hizo. Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza aina za tafsiri, matatizo yanayokumba tafsiri, vyanzo vya matatizo yenyewe pamoja na kupendekeza njia mbalimbali za kukabiliana na changamoto zinazokumba tafsiri za taarifa za habari katika kituo kilichoteuliwa. Nadharia ya ulinganifu amilifu ya Nida ilitoa msingi wa kinadharia katika utafiti huu. Aidha, nadharia ya mawasiliano ya Newmark ilihusishwa kama nadharia changizi kutokana na uhusiano uliopo kati ya mihimili yake na ile ya nadharia ya ulinganifu amilifu. Data msingi katika utafiti huu ilikuwa miswada ya taarifa za habari katika Kiswahili na katika Kikipsigis. Uchanganuzi linganishi wa miswada hiyo ulifanywa ili kutathmini ulinganifu wa maana kwenye matini za miswada hiyo. Kutokana na uchanganuzi huo, imedhihirika kwamba tafsiri maana na tafsiri mawasiliano huchangia pakubwa katika kuibushwa kwa viwango vya juu vya ulinganifu wa maana kati ya matini za lugha chanzi na za lugha lengwa ilhali tafsiri ya moja kwa moja na tafsiri huru husababisha upotoshaji mkubwa wa maana ya matini chanzi katika matini lengwa. Vilevile imebainika kwamba tafsiri za taarifa za habari ni shughuli ambayo hukumbwa na matatizo anuwai kama tofauti za kiisimu na za kitamaduni kati ya lugha chanzi na lugha lengwa, upenyezaji na udondoshaji wa vipengele vya matini chanzi katika lugha lengwa na uchangamano katika tafsiri za misemo na nahau. Pia uchunguzi wetu umedhihirisha kwamba ipo mikakati mbalimbali inayoweza kutumiwa na mtafsiri kukabiliana na changamoto hizo kama ufutaji wa dhana inayotatiza, ufafanuzi na maelezo, matumizi ya neno fidia katika lugha lengwa, matumizi ya neno la mkopo, matumizi ya dhana yenye maana ya kijumla, uundaji wa istilahi mpya, urejeleaji wa makamusi na mtafsiri kuwa na stadi za kukabiliana na changamoto za tafsiri. Utafiti huu ni mchango katika kuelewa jinsi tafsiri zinazohusisha lugha zinazotofautiana kimuundo zilivyo changamano. Utafiti huu unapendekeza kutumiwa kwa matokeo yake kama mwongozo wa kukabiliana na changamoto za tafsiri hata katika nyanja nyinginezo kwa kutilia maanani hali kwamba japo nyanja zinatofautiana kwa namna moja au nyingine, mikakati ya tafsiri katika nyanja zenyewe huingiliana.

**YALIYOMO**

IKIRARI .......... ii

TABARUKU .......... iii

SHUKRANI .......... iv

ORODHA YA VIFUPISHO .......... vi

IKISIRI .......... vii

**SURA YA KWANZA .......... 1**

UTANGULIZI .......... 1

1.0 USULI WA MADA .......... 1

1.1 TATIZO LA UTAFITI .......... 4

1.2 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO .......... 5

1.3 MALENGO YA UTAFITI .......... 6

1.4 NADHARIA TETE .......... 7

1.5 UPEO NA MIPAKA .......... 7

1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA .......... 8

1.6.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Tafsiri Kwenye Vyombo vya Habari .......... 8

1.6.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Matatizo ya Tafsiri .......... 11

1.7 MSINGI WA KINADHARIA .......... 17

1.7.1 Nadharia ya Ulinganifu .......... 18

1.7.2 Nadharia ya Mawasiliano .......... 20

1.7.3 Uhusiano kati ya Nadharia ya Ulinganifu Amilifu na Nadharia ya Mawasiliano22

1.8 NJIA ZA UTAFITI .......... 23

**SURA YA PILI** ............................................................ **26**
AINA ZA TAFSIRI ZINAZOTUMIKA KATIKA TAARIFA ZA HABARI KATIKA KITUO CHA KITWEK ............................................................ 26
2.0 UTANGULIZI ............................................................ 26
2.1 AINA ZA MATINI ZA TAFSIRI ............................................................ 26
2.1.1 Matini Elezi ............................................................ 27
2.1.2 Matini Arifu ............................................................ 27
2.1.3 Matini Amili ............................................................ 28
2.2 AINA ZA TAFSIRI ............................................................ 28
2.2.1 Tafsiri ya Moja kwa Moja ............................................................ 29
2.2.2 Tafsiri Huru ............................................................ 35
2.2.3 Tafsiri Maana ............................................................ 38
2.2.4 Tafsiri Mawasiliano ............................................................ 42
2.3 HITIMISHO ............................................................ 46

**SURA YA TATU** ............................................................ **48**
MATATIZO YANAYOKUMBA TAFSIRI ZA TAARIFA ZA HABARI KATIKA KITUO CHA KITWEK ............................................................ 48
3.0 UTANGULIZI ............................................................ 48
3.1 Tofauti za Kiisimu kati ya Lugha Chanzi na Lugha Lengwa ............................................................ 49
3.1.1 Tofauti za Kimofolojia ............................................................ 49
3.1.2 Tofauti za Kisintaksia ............................................................ 51
3.1.3 Tofauti za Kisemantiki ............................................................ 53

3.2 Tofauti za Kitamaduni kati ya Lugha Chanzi na Lugha Lengwa ....57
3.4 Upenyezaji wa Vipengele Vipya katika Matini Lengwa ....72
3.5 Uchangamano katika Tafsiri za Misemo na Nahau ....73
3.6 HITIMISHO ....75

**SURA YA NNE ....76**
MIKAKATI YA KUKABILIANA NA UKOSEFU WA ULINGANIFU WA MAANA KATIKA TAFSIRI ZA TAARIFA ZA HABARI ....76
4.0 UTANGULIZI ....76
4.1 NJIA ZA KUKABILIANA NA UKOSEFU WA ULINGANIFU WA MAANA ..76
4.1.1 Urejeleaji wa Makamusi ....77
4.1.2 Matumizi ya Dhana yenye Maana Elezi ....78
4.1.3 Matumizi ya Dhana yenye Maana ya Kijumla ....79
4.1.4 Matumizi ya Neno Fidia katika Lugha Lengwa ....80
4.1.5 Matumizi ya Neno la Mkopo ....81
4.1.6 Matumizi ya Ufafanuzi na Maelezo ....83
4.1.7 Ufutaji wa Neno Linalotatiza ....84
4.1.8 Uundaji wa Istilahi Mpya ....85
4.1.9 Ujuzi na Stadi za Tafsiri ....91
4.2 HITIMISHO ....93

**SURA YA TANO .......................................................................................................94**

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....................................................................94

5.0 UTANGULIZI ...........................................................................................94

5.1 HITIMISHO ...............................................................................................95

5.2 MAPENDEKEZO .......................................................................................97

**MAREJELEO ............................................................................................................99**

KIAMBATISHO 1......................................................................................... xi

KIAMBATISHO 2...................................................................................... xvii

KIAMBATISHO 3..........................................................................................xx

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 USULI WA MADA

Tafsiri ni mchakato wa mawasiliano unaohusu kuhamisha maana na ujumbe ulio katika lugha chanzi (kuanzia hapa LC) hadi lugha lengwa (kuanzia hapa LL). Uhamishaji huu unapaswa kutilia maanani kwamba uamilifu wa matini chanzi (tangu hapa MC) unastahili kudumishwa katika matini lengwa (tangu hapa ML). Kwa kufanya hivi, sifa za kisemantiki, kimtindo na kiutekelezi za MC zinatarajiwa kuhifadhiwa. Kwa kuwa tafsiri ni shughuli inayohusisha lugha zinazotofautiana kwa namna mbalimbali, mtafsiri hukabiliana na changamoto chungu tele anapojaribu kudumisha lengo la mwandishi wa MC katika ML.

Tafsiri imechangia pakubwa katika maendeleo ya binadamu. Imeunganisha jamii mbalimbali za watu wanaotumia lugha tofauti. Tafsiri ni njia ya mawasiliano, nyenzo ya kueneza utamaduni na ni mbinu mojawapo ya kujifunza lugha. Inatumika kutolea maelezo ya kibiashara, hasa maelekezo ya jinsi ya kutumia bidhaa, katika vyombo vya habari, nyaraka rasmi kama ripoti za kimataifa, makala za kitaaluma na kadhalika. Tafsiri pia imetangamanisha lugha na tamaduni za mataifa mbalimbali tangu mataifa yenyewe yalipoanza maingiliano na ushirikiano miongoni mwao. Usahihi wa tafsiri za kutekeleza majukumu haya unapaswa kutiliwa mkazo kwani tafsiri isiyo sahihi inaweza kuleta matatizo na hata hasara.

Taaluma ya tafsiri hutazamwa kama sayansi inayohusu matumizi ya lugha yenye uketo mwingi. Ni sehemu ya isimu linganishi na hujikita sana kwenye maana. Tafsiri humwezesha mtafsiri kulinganisha lugha mbili katika viwango tofauti kama vile sarufi, maana na msamiati. Pia tafsiri hutuonyesha jinsi lugha zinavyotofautiana au kulingana sio tu katika sarufi au maneno bali pia katika matumizi. Mtafsiri huweza kuonyesha ujuzi wake wa isimu na sarufi ya lugha zote mbili, LC na LL. Zoezi lake hujaribu kupata kiwango cha juu cha ulinganifu wa maana (tangu hapa UM) baina ya lugha zote mbili.

Cartford (1965) anaeleza ulinganifu wa maana katika tafsiri kama hali ya kuwepo kwa uhusiano baina ya ML na MC. Uhusiano unaojitokeza hapa ni ule unaoipa ML hadhi ya kuchukuliwa kuwa ni tokeo la tafsiri ya MC. Pym (2010) anasema kwamba ulinganifu hutumiwa kama kigezo cha kukadiria iwapo mchakato wa tafsiri umefaulu au la. Kigezo hiki ni thabiti na hutumika katika uchunguzi na uchanganuzi wa shughuli za tafsiri.

Kufaulu kwa zoezi la tafsiri kunaweza kutatizika kutokana na mambo mbalimbali. Tatizo kuu linatokana na uwezo wa mtafsiri wa kuzielewa lugha zote mbili kwa undani. Pia msimamo na mwelekeo wake binafsi kuhusu kila mojawapo ya lugha zinazohusika unaweza kuwa kikwazo katika harakati za kujaribu kufikia tafsiri bora. Kama mtafsiri ataitukuza lugha moja, yeye ataegemea upande wa lugha hiyo na kuipuuza ile nyingine. Anaweza kuirundikia sifa lugha anayoitukuza na kupanua maana kwa kuongezea yasiyo ya kweli na kuyaacha mengi ya maana na yaliyo muhimu katika lugha ya pili.

Ujuzi wa isimu humsaidia mtafsiri kuelewa miundo ya sentensi na jinsi ya kuzifupisha, kuzirefusha na kuigeuza mipangilio ya maneno katika sentensi zenyewe. Ujuzi huu pia utamsaidia kuelewa viwango vya maana, msamiati wa kawaida, wa kiufundi n.k. Utamwezesha kuelewa matumizi ya lugha kisarufi, kitamathali, kirejista, kilahaja n.k na kumsaidia kuteua mambo yenye uzito na yafaayo kutafsiriwa. Mtafsiri anatarajiwa kuwa na uwezo wa kimawasiliano na maarifa ya kulinganisha maumbo ya kimatini katika mifumo yote miwili ya LC na LL.

Idhaa zote za Shirika la Utangazaji la Kitaifa (KBC) zinazotangaza katika lugha za kienyeji hutegemea tafsiri katika baadhi ya vipindi vyao. Utafiti wetu unahusu UM katika tafsiri za taarifa za habari (tangu hapa TH) kutoka Kiswahili hadi Kikipsigis. Kwenye uchunguzi wetu tutatathmini kiwango cha UM kama inavyopokelewa na wasikilizaji wa lugha ya Kikipsigis.

Lahaja ya Kikipsigis ni mojawapo ya lahaja za lugha ya Kikalenjin. Ina wazungumzaji wake katika kaunti za Kericho na Bomet, na sehemu za kaunti za Nakuru na Narok. Lahaja nyinginezo za Kikalenjin ni kama Kinandi, Kitugen, Kikeiyo, Kimarakwet, Kipokot na Kisabaot (Toweett, 1979). Chesaina (1991) anaeleza kwamba jamii ya Kikalenjin imeundwa kutokana na lahaja nane ambazo ni: Kikeiyo, Kimarakwet, Kikipsigis, Kinandi, Kipokot, Kitugen, Kiterik na Kisebeei. Kulingana naye, lahaja za Kimarakwet, Kinandi, Kikeiyo, Kikipsigis na Kitugen hufanana kwa asilimia kubwa.

Kipkorir (1985) anasema kwamba lahaja ya Kikipsigis ina wazungumzaji wengi kuliko lahaja zote, ikifuatiwa na Kinandi, Kitugen, Kikeiyo, Kimarakwet, Kipokot na Kisabaot mtawalia. Kutokana na idadi kubwa ya wazungumzaji wa lahaja ya Kikipsigis, ni bayana kwamba kuna matumizi mapana ya lahaja hii katika vyombo vya habari vinavyotoa matangazo katika Kikalenjin ndiposa tumeteua kama msingi wa kutathmini kiwango cha ulinganifu wa TH zinazotafsiriwa.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Vyombo vya habari vimekuwa vikitumika sana kama njia ya mawasiliano kwa umma nchini Kenya. Kumekuwa na ongezeko la idadi ya vituo vya runinga, redio, magazeti, majarida na njia nyinginezo za mawasiliano. Vituo vya redio kwa sasa ni zaidi ya 115 (Taz. kiambatisho) huku idadi kubwa yavyo vikitangaza kwa lugha za kiasili. Hii inaonyesha kwamba kumekuwa na mshawasha wa kutaka kufikia idadi kubwa ya wasikilizaji, waliosoma na wasiosoma, kwa lugha wanazozielewa.

Shirika la Utangazaji la Kitaifa hukusanya habari kwa lugha moja, aghalabu Kiingereza au Kiswahili, kisha zitafsiriwe katika lugha za kiasili. Tumebaini kwamba kuna mambo mbalimbali yanayoathiri uwasilishaji wa maana katika tafsiri zinazofanywa. Mambo haya husababisha kuwepo kwa viwango vinavyotofautiana vya UM. Kazi hii inalenga kuchunguza vyanzo vya ukosefu wa UM na kupendekeza njia za kukabiliana navyo ili kufikia tafsiri bora tukijikita kwenye kituo kimojawapo kinachopatikana katika Shirika la Utangazaji la Kitaifa kinachotangaza kwa lahaja za Kikalenjin.

Japo tafiti nyingi zimewahi kufanywa kuhusu tafsiri kwa kutumia nadharia mbalimbali, tafiti zenyewe zimeegemea kwenye lugha za Kiingereza na Kiswahili, ambapo lugha ya Kiingereza aghalabu huwa LC huku Kiswahili kikiwa LL. Tafiti nyingi hazijafanywa kwa kuchukulia Kiswahili kama LC na lugha za kiasili kama LL. Ni katika utambuzi huo wa kuwepo kwa pengo hilo la kiusomi ndiposa tukaamua kushughulikia tafsiri za TH kutoka Kiswahili hadi Kikipsigis ambayo ni lahaja mojawapo ya Kikalenjin.

## 1.2 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO

Katiba ya Kenya iliyopitishwa mwaka wa 2010 inatambua hali ya wingilugha nchini. Hali hii ya wingi lugha inaipa tafsiri nafasi muhimu kwa kuwa ujumbe unaopatikana katika lugha moja unaweza kuhawilisha hadi lugha nyingine. Pia katiba yenyewe inatambua haki ya kidemokrasia ya upataji habari kwa umma kupitia njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari. Tafsiri kama zoezi la ubadilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka LC hadi LL itawezesha vyombo vya habari kutekeleza jukumu kuu la kufikisha ujumbe kwa HL. Hata hivyo, zoezi hili linapaswa kuhakikisha kwamba mawazo kati ya MC na ML yanalingana.

Udadisi wetu kwenye Shirika la Utangazaji la Kitaifa (KBC) umetubainishia kwamba TH zinazosomwa katika lugha ya Kikipsigis katika kituo cha Kitwek zinatafsiriwa kutoka TH za Kiswahili zinazosomwa katika idhaa ya Kiswahili. Utambuzi huu umetupa mshawasha wa kuchunguza tafsiri za habari hizo ili kutathmini kiwango cha ulinganifu wa maana. Tunaamini kwamba shughuli hii kama ilivyo tafsiri ya aina yoyote hukumbwa na matatizo mbalimbali yanayosababishwa na vyanzo mbalimbali. Tunalenga kuonyesha

matatizo hayo na kudhihirisha jinsi yanavyoathiri zoezi la tafsiri kisha kupendekeza njia mbalimbali za kukabiliana na matatizo hayo.

Kwa kudurusu kazi zilizofanywa na watafiti wengine kuhusu masuala yanayofungamana na tafsiri, tulibaini kwamba nyingi yazo ni zile zinazohusu Kiswahili kama LL. Kadri ya ufahamu wetu, ni tafiti chache zilizo na lugha za kiasili kama LL. Hali kadhalika ni tafiti chache zilizochukulia Kiswahili kama LC. Utafiti wetu utahusisha Kiswahili kama LC na lahaja ya Kikipsigis kama LL. Ifahamike kuwa lugha hizi mbili zinatofautiana kimuundo. Pia zinatokana na makundi mawili tofauti: moja ya Kibantu (Kiswahili) na nyingine isiyo ya Kibantu (Kikipsigis). Tunalenga kuonyesha tofauti za kimuundo na za kimsamiati zinazojitokeza baina ya lugha hizi na jinsi tofauti hizo zinavyoathiri viwango vya ulinganifu wa maana na zoezi la tafsiri kwa jumla.

### 1.3 MALENGO YA UTAFITI

(a) Kuchunguza aina za tafsiri zinazotumiwa na watafsiri wa taarifa za habari za Kikipsigis katika kituo cha Kitwek.

(b) Kubainisha matatizo yanayokumba tafsiri za taarifa za habari za Kikipsigis katika kituo cha Kitwek.

(c) Kuchunguza vyanzo vya matatizo yanayokumba tafsiri za taarifa za habari za Kikipsigis katika kituo cha Kitwek.

(d) Kupendekeza njia za kukabiliana na matatizo yanayokumba tafsiri za taarifa za habari za Kikipsigis katika kituo cha Kitwek.

## 1.4 NADHARIA TETE

(a) Zipo aina mbalimbali za tafsiri zinazotumiwa na watafsiri wa taarifa za habari za Kikipsigis katika kituo cha Kitwek.

(b) Tafsiri za taarifa za habari za Kikipsigis katika kituo cha Kitwek hukumbwa na matatizo mbalimbali.

(c) Matatizo yanayokumba tafsiri za taarifa za habari za Kikipsigis katika kituo cha Kitwek husababishwa na mambo mbalimbali.

(d) Kuna njia mbalimbali za kukabiliana na matatizo yanayokumba tafsiri za taarifa za habari za Kikipsigis katika kituo cha Kitwek.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA

Vituo vya redio vinavyotangaza katika lahaja za Kikalenjin ni pamoja na Kitwek, Kass, Chamge, Radio Injili–Kericho, Sayare na Kong'asis. Hata hivyo, utafiti wetu umefungamanishwa na kituo cha Kitwek ambacho ni kitengo cha Shirika la Utangazaji la Kitaifa (KBC). Utafiti wetu utachanganua taarifa za Kiswahili za idhaa ya Kiswahili na za Kikipsigis katika idhaa ya Kitwek. Tutajikita kwenye taarifa za habari tu bila kujihusisha na vipindi vinginevyo. Kwenye taarifa, tutajifunga kwenye habari za kitaifa, kimataifa, michezo na hali ya anga.

Japo lugha ya Kikalenjin ina lahaja nyingi utafiti wetu utachunguza ukosefu wa UM katika lahaja ya Kikipsigis. Uchunguzi wetu umebainisha kwamba watafsiri wa TH katika kituo cha Kitwek ni wazawa wa lahaja ya Kikipsigis, Kinandi na Kitugen. Pia tumebainisha kwamba watafsiri hawa wanabadilishana zamu na kwa hivyo uchanganuzi

wetu utajifungia kwenye TH zinazotafsiriwa na mtafsiri wa Kikipsigis. Kwa mantiki hiyo tutachunguza viwango vya UM katika TH zinazotafsiriwa katika Kikipsigis.

## 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Mengi yameandikwa kuhusu tafiti zilizofanywa kuhusu tafsiri. Kwa sababu hiyo tumeigawa sehemu hii mara mbili ili kushughulikia yaliyoandikwa kuhusu tafsiri kwenye vyombo vya habari na yaliyoandikwa kuhusu matatizo ya tafsiri.

### 1.6.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Tafsiri Kwenye Vyombo vya Habari

Matini zitafsiriwazo hujikita katika sajili mbalimbali na uteuzi wa visawe vitumikavyo kuwakilisha dhana zipatikanazo katika matini hufanywa kwa kuzingatia sajili inayohusika katika matini hizo. Mzee (1980) ametafiti kuhusu tafsiri za makala magazetini katika sajili mbalimbali. Ameonyesha makosa tofauti tofauti ambayo yanabainika katika tafsiri zinazofungamana na sajili hizo. Amekashifu tendo la mtafsiri kulazimisha sintaksia ya MC katika LL. Kazi hii inahusiana na kazi yetu tunaposhughulikia tafsiri inayohusisha lugha mbili zinazotofautiana kisintaksia. Pia kazi hii ina mwingiliano wa chanda na pete na kazi yetu kwa kuwa kazi zote mbili zina upeo wa vyombo vya habari. Aidha, tutachanganua makosa yanayodhihirika katika tafsiri za TH kwa mujibu wa sajili ya vyombo vya habari.

Makosa yanayofanywa katika tafsiri katika nyanja mbalimbali husababishwa na vyanzo kadha wa kadha. Makosa hayo huwa na athari kubwa katika uwasilishaji wa maana za kimatini kutoka LC hadi LL. Ali (1981) alijadili makosa mbalimbali yanayojitokeza katika tafsiri za TH za Sauti ya Kenya. Alidhihirisha namna tafsiri mbaya zinavyopotosha

mawasiliano kati ya Sauti ya Kenya na wasikilizaji wake. Ametaja matatizo yakiwemo ukosefu wa ujuzi wa kutosha kwa upande wa watafsiri, muda mfupi wa kuandika tafsiri pamoja na matatizo mengineyo yasiyofungamana moja kwa moja na lugha. Kazi hii ilizingatia tafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, nasi tunachunguza tafsiri zinazotoka Kiswahili hadi Kikipsigis ili kubainisha iwapo kuna UM katika kazi zinazotafsiriwa katika lugha hizi na kutathmini vyanzo vya hali itakayobainika katika uchunguzi wenyewe. Vilevile utafiti wetu unahusiana na huu kwa upande wa mazingira ya utafiti; Shirika la Utangazaji la Kitaifa lililokuwa Sauti ya Kenya hapo awali.

Kufanikiwa kwa shughuli ya uhawilishaji wa ujumbe kutoka MC hadi ML kunachangiwa na udhahiri na usahihi upatikanao katika MC. Kutokana na jambo hili, mtafsiri anapaswa kuwa na ujuzi katika uhariri ili kuwa na utambuzi wa hali ya kutokuwepo kwa uwazi katika MC na kuhakikisha anafasiri kwa usahihi matini kabla ya kuzitafsiri. Muchemi (1998) ameonyesha athari kwenye udhahiri na usahihi katika tafsiri za makala magazetini. Ameonyesha aina mbalimbali za makosa ya tafsiri magazetini ambayo ni kikwazo cha udhahiri na usahihi wa makala. Anapendekeza uwazi katika MC udumishwe unapohawilishwa katika ML. Mipaka ya utafiti huu inalingana na ile ya kazi yetu na uhusiano huu utachangia kufanikisha harakati zetu za kutimiza malengo ya shughuli yetu. Tunapopania kuchunguza mikakati thabiti ambayo mtafsiri anatarajiwa kuweka ili kufikia uwazi na udhahiri katika uhawilishaji wa ujumbe ulioko kwenye MC, kazi hii itatuwekea msingi wa kufikia madhumuni hayo.

Tofauti za kimuundo baina ya lugha zinazohusika katika tafsiri huzua changamoto kwa mtafsiri kwa kuwa tofauti hizo zisipobainika na kusawazishwa kuna uwezekano wa kulazimishwa kwa miundo ya LC katika LL, hali itakayosababishaji upotoshaji wa maana. Kaviti (2005) ameshughulikia makosa ya kisintaksia katika tafsiri za makala magazetini kutoka Kiingereza hadi Kiswahili katika kampuni ya Nation Media Group. Ametumia magazeti ya *Daily Nation* na *Taifa Leo* kuonyesha jinsi sintaksia isiposawazishwa ipasavyo katika shughuli ya tafsiri, maana inayodhamiriwa kuwasilishwa na mwandishi wa MC hupotoshwa. Kwa kuwa utafiti wetu unajikita katika uchanganuzi wa lugha mbili zinazotofautiana kisintaksia kazi yake itakuwa ya manufaa kwetu tunapochunguza jinsi maumbo katika lugha zinazoshughulikiwa yanavyosawazishwa.

Misingi ya nadharia ya ulinganifu ina uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazotinga kufikiwa kwa tafsiri bora. Kilonzo (2011) amechanganua changamoto zinazowakabili wahariri, wakusanyaji wa habari na watafsiri wa TH za runinga. Utafiti wake umeegemezwa kwenye nadharia ya ulinganifu ulioasisiwa na Nida (1964). Amefafanua misingi ya nadharia ya ulinganifu na jinsi inavyoweza kutumika kufikia tafsiri bora. Ameonyesha hali mbalimbali zinazodhihirisha ukosefu wa UM katika tafsiri ya TH kutoka Kiingereza hadi Kiswahili na sababu zinazochangia kutokea kwa hali hiyo. Vilevile amependekeza njia mbalimbali zinazoweza kutumika ili kupunguza viwango vya kutofautiana kwa MC na ML za TH zilizotafsiriwa. Japo kazi hii inahusiana na yetu kwa upande wa nadharia na mipaka, lugha zinazohusika katika tafiti zenyewe zinatofautiana, hali itakayoweka msingi wa ulinganishaji wa matokeo yazo na kujenga mahitimisho fulani.

### 1.6.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Matatizo ya Tafsiri

Baadhi ya matatizo yanayokumba tafsiri huwa yamezagaa katika nyanja zote. Pia kanuni zinazowaongoza watafsiri katika nyanja tofauti aghalabu zinalingana. Lefevere (1975) amechunguza matatizo yanayojitokeza katika tafsiri na uwezekano wa kutafsiri katika uwanja wa fasihi hasa ushairi. Ameangazia kanuni mbalimbali zinazomwongoza mtafsiri pamoja na kufafanua manufaa na dosari za kila kanuni. Ametoa tathmini ya namna kanuni zenyewe zinavyochangia kufanikisha mawasiliano. Ametoa mapendekezo ya taratibu zinazopaswa kufuatwa katika tafsiri ya fasihi. Pia ameonyesha nafasi ya tafsiri katika ukuzaji, usomaji na uchambuzi wa fasihi. Vilevile amejadili athari za tafsiri katika fasihi ya LL. Ingawa kazi hii imejikita katika uwanja wa fasihi, tutapata mwongozo wa kinadharia ambao utatufaa katika utafiti wetu kutoka kwayo.

Aina za tafsiri zitumikazo hutegemea aina za matini, sajili na miktadha mbalimbali ambamo matini zenyewe zimeandikwa. Newmark (1982) alishughulikia mitazamo ya wataalamu waliomtangulia kwa kuangazia nadharia na kanuni za tafsiri, matatizo wanayokumbana nayo watafsiri na kutoa mapendekezo kuhusu jinsi ya kuyatatua matatizo hayo. Amedurusu na kuyatathmini upya maoni ya wataalamu wa masuala ya tafsiri waliomtangulia na kujadili umuhimu wa kuwepo na misingi imara ya nadharia, kanuni na taratibu ambazo zinamwongoza mtafsiri katika kutimiza lengo lake la kufikisha maana asilia kwa HL. Pia ametaja aina za tafsiri ambazo zinatumika kutegemea hali mbalimbali za matini, sajili na miktadha mbalimbali. Tathmini yetu ya ulinganifu wa maana itafanywa kwa mkabala wa kazi hii wa kuchunguza matatizo yanayoathiri tafsiri za TH na kuweka wazi kanuni na taratibu zinazowezesha kupatikana kwa tafsiri bora zaidi.

Tofauti za kimazingira na za vipengele vya utamaduni kati ya LC na LL ni miongoni mwa vikwazo vikubwa vya kufikiwa kwa tafsiri bora. Aidha, kutomudu barabara lugha zinazohusika katika tafsiri kunaweza kusababisha upotoshaji wa maana ya MC katika ML. Mutahi (1987) ameangazia matatizo ya tafsiri kwa kujikita katika fasihi simulizi. Amedhihirisha kwamba matatizo ya tafsiri yanatokana na tofauti za kimuundo kati ya LC na LL, tofauti za kimazingira na tofauti za vipengele vya utamaduni. Anasisitiza kwamba kando na mambo yaliyotajwa, ni sharti mtafsiri azielewe barabara lugha zote mbili zinazohusika ili kufikia tafsiri bora. Masuala haya yanachukua nafasi kubwa katika kazi yetu tunapochunguza viwango vya ulinganifu wa maana katika matini za TH.

Mtafsiri anapaswa kufanya uteuzi wa maneno au mafungu ya maneno anayotumia kuwakilisha dhana zilizotumika katika matini zinazotafsiriwa ili kuhawilisha habari iliyokusudiwa kutegemea miktadha ya MC. Kazi bora za tafsiri ni tokeo la mtafsiri kufanya uteuzi wa masuala kadhaa yanayodhihirika kuondoa vikwazo vya kueleweka kwa matini za tafsiri. Shitemi (1990) amejadili namna mtafsiri wa matini anavyofanya uteuzi wa yale anayoyaandika kwa dhamira ya kuwasiliana vyema na HL. Kulingana na Shitemi, tofauti zinazojitokeza baina ya matini ya LC na ile ya LL zinatokana na sababu za uteuzi wala si kimakosa kama inavyochukuliwa na wahakiki wengi wa tafsiri. Kazi hii ina mchango muhimu katika kazi yetu tunapochunguza vyanzo vya ukosefu wa UM katika TH tunapotathmini hali tofauti tofauti zinazomlazimu mtafsiri kufanya uteuzi mwafaka ili kumwondolea vikwazo vinavyotatiza uwasilishaji wa ujumbe ulionuiwa kupitishwa na mwandishi wa MC ya TH kwa HL.

Misingi ya nadharia ya maana ina maingiliano makubwa na ile ya nadharia ya ulinganifu amilifu na ya mawasiliano. Nadharia hizi zote zinaweka msisitizo katika maana ya kimatini kuliko umbo la kimatini. Mwangi (1996) akiifanyia tathmini kamusi ya Johnson (1939) ya Kiingereza – Kiswahili, amechunguza matatizo ya leksikografia tafsiri katika kamusi za uwili lugha. Amefanya tathmini hii kwa mkabala wa nadharia ya maana. Ameyashughulikia makosa ya tafsiri katika viwango mbalimbali vya lugha kama vile sarufi na semantiki. Pia amejadili kwa kifupi dhana ya tafsiri, leksikografia – matini na nafasi ya maana katika tafsiri. Amesisitiza kwamba maana ni kipengele cha muhimu katika tafsiri. Japo utafiti wetu haukuhusisha nadharia ya maana, maoni yake kuhusu umuhimu wa maana katika tafsiri yatahimili utafiti wetu.

Kutokana na tofauti zinazodhihirika katika vipengele vya kitamaduni na vya kiisimu kati ya lugha za ulimwenguni, vipengele vya fani huwa vigumu kuhamishwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Mutie (1997) ameangazia matatizo yanayohusu kuhamisha sanaa katika kazi zilizotafsiriwa. Akirejelea tamthilia ya *Mizigo* iliyotafsiriwa kutoka *The Burdens*, anaeleza namna sanaa hudhoofishwa katika kazi ya tafsiri hasa katika kipengele cha fani. Suala aliloshughulikia hudhihirika katika kazi nyingi za tafsiri. Kazi yake itatufaa katika utafiti wetu tunapochunguza matatizo yanayohusu uhamishaji wa vipengele vya mtindo kutoka MC ya TH hadi ML. Lugha zinazohusika katika utafiti wetu zinabaidika kimuundo na hali hii ni kikwazo kikuu katika uhawilishaji wa fani. Japo kazi yake imejikita kwenye matini za kifasihi nayo yetu inahusu matini za vyombo vya habari, zote zinatumia fani sawa katika miktadha inayotofautiana.

Ubora wa kazi ya tafsiri hutegemea ujuzi wa mtafsiri na stadi za kukabiliana na changamoto za tafsiri. Yapo matatizo yanayosababishwa na dosari au udhaifu wa mtafsiri kutomudu shughuli hii na matatizo mengine yasiyofungamana na uwezo wa mtafsiri mwenyewe. Osano (1997) amefanya uchanganuzi wa matatizo ya tafsiri katika *Risasi Zianzapo Kuchanua* (1975). Ameyachunguza matatizo ambayo husababishwa na udhaifu au pungufu mbalimbali kwa upande wa mtafsiri. Pia ameshughulikia matatizo ambayo yanatokana na sababu ambazo mtafsiri hana uwezo wa kuyaepuka; matatizo yanayohusiana na sababu nyinginezo katika lugha kando na pungufu za upande wa mtafsiri mwenyewe. Tumeyafanya mambo yaliyochunguzwa katika kazi hii kama chukulizi na tunadhamiria kuchanganua matatizo ya tafsiri za TH na kuyaainisha kutegemea kiini cha kutokea kwa matatizo yenyewe ili kuthibitisha madai yanayojitokeza katika kazi yake.

Kuwepo kwa vikoa vya maana katika lugha mahsusi kunasababisha changamoto za tafsiri ambapo neno katika lugha moja linaweza kuwa na maana halisi na kukosa neno lenye maana ya kijumla katika lugha nyingine, na katika hali nyingine neno linaweza kuwa na maana ya kijumla katika lugha moja na kukosa neno lenye maana halisi katika lugha nyingine. Kamau (2008) amechunguza jinsi maana inaweza kupotoshwa iwapo ujumbe ulionuiwa kupitishwa na mwandishi wa MC haujahamishwa kikamilifu kwa HL. Anadokeza kwamba hali kama hiyo husababishwa na mambo kadha wa kadha kama vile nia ya mtafsiri na uwezo wake wa kukabiliana na zoezi la tafsiri. Utafiti wake ulitumia kielezo cha tafsiri ya Kiswahili ya *Shamba la Wanyama* kutoka *Animal Farm* ya Kiingereza. Kwanza ameainisha dhana zilizotumika katika MC kwenye vikoa vya maana kisha akavitumia vikoa hivyo kama msingi wa kulinganisha MC na ML. Alitathmini

ufaafu na kutofaa kwa dhana zilizotumika katika ML na hatimaye kueleza kiwango cha kubadilika kwa maana. Tunadhamiria kufanyia tathmini kiwango cha athari ya kuwepo kwa vikoa vya maana katika lugha za uchunguzi wetu katika uwasilishaji wa maana na kazi hii itatupa mwongozo ufaao.

Viwango vya ulinganifu wa maana hutofautiana kutoka tafsiri moja hadi nyingine kutegemea kanuni zinazoongoza tafsiri hizo, aina za tafsiri zinazohusishwa na misingi ya kinadharia ambayo kazi zenyewe zimehimiliwa. Nyaga (2009) amechunguza UM katika tafsiri ya fasihi. Akitumia *Usaliti Mjini* kama kielelezo, amedhihirisha sura mbalimbali za ulinganifu na namna ulinganifu unaweza kuibua matatizo ya uibushi wa maana. Ingawa utafiti wake umefungamanishwa na matini za kifasihi, ukweli ni kwamba kila aina ya matini hudhihirisha sifa zake mbalimbali za ulinganifu almuradi matini yenyewe imechanganuliwa katika misingi ya kuchunguza sajili inayohusika katika matini hiyo. Sura mbalimbali za ulinganifu wa maana zilizochunguzwa katika kazi hii ni nyenzo kuu tutakayotumia kufanya upambanuzi wa matini za TH ili kutathmini viwango vya UM.

Vikwazo vinavyokumba tafsiri katika nyanja mbalimbali ni vya aina tofauti tofauti kutegemea vyanzo vya vikwazo vyenyewe. Muchiri (2012) amechunguza aina mbalimbali za vikwazo vinavyotokea katika tafsiri zinazofanywa na wanafunzi wa viwango vya shahada ya kwanza na ya uzamili na athari zinazoletwa na vikwazo hivyo katika maana ya ujumbe uliokusudiwa. Uchunguzi wake ulilenga vikwazo vinavyomkabili mwanafunzi wa taaluma ya tafsiri anapotafsiri kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, na kutoka Kiswahili hadi Kiingereza. Aina za vikwazo vilivyochunguzwa ni kama: vikwazo vya kileksika, vya kisintaksia na vikwazo vya kisarufi ambapo mtafsiri

hupuuza tofauti za kimuundo baina ya lugha mbili zinazohusika au kushawishika kuhamisha kanuni za kisarufi, kwa kujua au kutojua, kutoka LC hadi LL. Tutapata msingi wa kuainisha vikwazo vya tafsiri za TH kutokana na kazi hii ili kuturahisishia tathmini ya kiwango cha UM.

Uhamishaji wa maana kutoka LC hadi LL unahitaji umakinifu mkubwa katika uteuzi unaofanywa kuhusu namna ya kuhamisha vipengele vya MC hadi ML kwa njia itakayorahisisha ufasiri wa ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa. Mutugi (2012) ameshughulikia matatizo yanayoibuka katika tafsiri za kauli za pronomino kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Amedhihirisha kwamba athari za tafsiri mbaya ni kupotoshwa kwa maana. Anadai kuwa tafsiri inahusu uteuzi mwingi kuhusu habari zipatikanazo katika sentensi. Anaona tafsiri kama mchakato wala si tukio. Kwenye mchakato wenyewe, kuna uhamishaji wa maana kutoka LC hadi LL. Utafiti wetu utachota mawazo yanayowiana na misingi ya nadharia zinazotuongoza kutokana na kazi yake hasa kuhusu uteuzi unaofanywa ili kudumisha maana ya MC na kuwezesha mawasiliano kutokea baina ya mtafsiri na HL ya TH.

Tafsiri zinazofanywa kwa HL ya watumizi lugha wa kawaida zinapaswa kuzingatia lugha itakayoeleweka kwa urahisi. Mtafsiri, hivyo basi, anapaswa kuwasilisha habari kwa hadhira hiyo kwa njia sahili. Moraa (2013) amechunguza matatizo yanayodhihirika katika matini tafsiri za kimatibabu. Anasema kwamba utabibu ni taaluma ambayo lugha yake huwa na wasifu maalum na hivyo huhitaji ujuzi na uangalifu mkubwa. Kwake, utambuzi wa upekee huo wa lugha ya kimatibabu hutupa shauku ya kutambua namna lugha hiyo huweza kuwasilishwa kwa njia sahili kwa matumizi ya watumizi lugha wa

kawaida. Taarifa zinazosomwa katika redio na vyombo vinginevyo vya habari hutumia lugha yenye sifa fulani mahsusi. Ni sharti mtafsiri wa TH atambue upekee wa lugha ya uanahabari ili abuni mkakati wa kupitisha habari kwa HL kwa namna itakayohakikisha ujumbe wake unaeleweka kwa urahisi.

Nadharia ya ulinganifu amilifu husisitiza uwasilishaji wa maana katika matini kwa kuzingatia muktadha pasipo kung'ang'ania uhamishaji wa umbo la matini. Akitumia nadharia hii kama nadharia changizi, Nyangeri (2014) amechunguza jinsi vitendo usemi vilivyomo kwenye tafsiri za *Musa na Shamba la Shule* na *Musa na Watekanyara* vilivyotafsiriwa. Ameonyesha jinsi uteuzi umefanywa kuvitafsiri vitendo usemi kulingana na muktadha vinamojitokeza. Kwa namna ambavyo uchunguzi wake wa ulinganifu umekitwa kwenye miktadha ya matini za kifasihi ndivyo ambavyo uchunguzi wetu wa ulinganifu utakitwa kwenye miktadha ya matini za vyombo vya habari pamoja na kutathmini utendakazi wa nadharia ya ulinganifu amilifu katika muktadha wa TH.

## 1.7 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti wetu utajikita kwenye nadharia ya ulinganifu, hasa ulinganifu amilifu. Aidha, tutatumia nadharia ya mawasiliano kama nadharia changizi. Hii inatokana na mantiki kwamba ni sharti kuwe na *ulinganifu wa kiuamilifu* kati ya MC na ML kwa kuwa dhamira ya tafsiri ni ya *kimawasiliano*, nayo mawasiliano yenye udhahiri hutokea pale ambapo maana katika MC inadumishwa katika ML. Tutaonyesha sababu za kutumia nadharia hizi kwa kuonyesha uhusiano uliopo kati ya nadharia hizo mbili.

### 1.7.1 Nadharia ya Ulinganifu

Cartford (1965) alifafanua ulinganifu kama uhusiano uliopo baina ya MC na ML. Uhusiano huu unaipa ML hadhi ya kuchukuliwa kuwa ni tafsiri ya MC. Mawazo haya yaliungwa mkono na Nida (1969), Toury (1980), Pym (1993) na Kroller (1995). Wote wanaafikiana kwamba tafsiri inakusudia kuunda ML iliyo sawa na MC. Pym (2010) anasema kwamba ulinganifu hutumika kukadiria kufaulu kwa tafsiri.

Nida na Taber (1964) wanafafanua ulinganifu amilifu kama kanuni ya tafsiri ambayo mtafsiri hulenga kuhamisha maana ya MC kwa njia ambayo itaibusha athari ile ile kwa HL ya ML kama ilivyokuwa kwenye HL ya MC. Wanashikilia kwamba mara nyingi umbo la MC hubadilika katika ML lakini maana hudumishwa almuradi muktadha wa MC umehifadhiwa. Kutokana na mawazo haya, wananadharia hawa wana msimamo kuwa ujumbe wa kimatini au ubora wa kisemantiki wa kazi ya tafsiri ni muhimu kuliko umbo la matini. Hivyo basi, tafsiri inapaswa kuleta athari sawa kwa wasomaji wa MC na wa ML.

Ulinganifu amilifu ni tokeo la maendeleo yaliyokuwa yamefikiwa katika uwanja wa Isimu- Matini. Hii ni kulingana na House (1977). Tangu kufikiwa kwa maendeleo hayo, kipashio cha tafsiri kimechukuliwa kuwa matini ambayo hufanya kazi katika miktadha, hali na utamaduni fulani mahususi. Kulingana na nadharia hii kila kipashio huwa na uhusiano na kile kinachokitangulia na kile kinachokifuata.

Kwa kuzingatia ulinganifu amilifu, MC huchanganuliwa kwa undani huku vipengele vya nia na majukumu vikipewa kipaumbele. Lengo la uchanganuzi wa kipragmatiki wa matini ni kupata nia ya mwandishi pamoja na namna anavyoieleza hiyo nia yake. Nia hii inapaswa kufinyangwa na mtafsiri katika ML kwa namna ambayo hutekeleza jukumu sawa na lile linalopatikana katika MC. Mwanzoni, maelezo kuhusu nadharia ya ulinganifu amilifu yalihusu tafsiri za maandiko ya Kibiblia. Tafsiri zilizofanywa zilijikita kwenye umbo na kupuuza maana iliyokusudiwa kufikia HL. Watafsiri walijali ulinganifu wa umbo lakini mwanaisimu Nida (1964) alipendekeza nadharia hii ya ulinganifu amilifu inayozingatia uamilifu wa matini inayohusika.

Ulinganifu amilifu huangazia mpokezi wa habari kuliko umbo la kisarufi la matini. Kwa msingi huu, lengo la mtafsiri ni kuhakikisha kwamba HL inapokea ujumbe kwa namna ambayo inaweza kuuelewa na kujihusisha nao. Kwa kuwa lengo kuu ni kupitisha mawasiliano, mtafsiri anapaswa kuteua neno au kirai ambacho kitawasilisha maana iliyokusudiwa sawasawa kwa HL. Ili kufikia lengo hili, mtafsiri hujikita kwenye maana. Kwa misingi ya nadharia hii, inakubalika mtafsiri atumie kipashio ambacho kina umbo tofauti katika LL na kile kinachotumika katika LC almuradi kinaweza kuwasilisha maana kikamilifu.

Kuna vigezo vitatu vinavyopaswa kuzingatiwa katika uchunguzi wa UM wa MC na ML. Mwanzo, ulinganifu hupatikana wakati faridi kwenye MC na ML huwa na nduni zinazofanana huku kila matini ikiwa kwenye muktadha wake. Kigezo cha pili ni kuchunguza kama kiwango cha maana ya kimuktadha huwiana na idadi ya nduni zinazojitokeza kwenye matini zote. Hii ni kwa sababu ulinganifu huwa wa kiwango cha

juu kadri nduni zenyewe zinavyozidi kuongezeka. Mwisho, tafsiri inaweza kurejelewa kiviwango kama iliyo sahihi au isiyo sahihi kwa mujibu wa kiwango cha ulinganifu wa faridi zinazohusika.

### 1.7.2 Nadharia ya Mawasiliano

Nadharia hii iliasisiwa na Newmark (1981). Inajaribu kuwasilisha maana kamili ya kimuktadha kwa njia ambayo kiini na lugha ya kimatini inakubalika na kueleweka kwa msomaji. Tafsiri inayoegemea kwenye nadharia hii hulenga kutimiza usahihi wa kimatini kwa upande wa muktadha wa yaliyomo katika MC. Katika mkabala wa nadharia ya mawasiliano ML aghalabu huwa bora kuliko MC kwa kuwa mtafsiri hujaribu kufikia kiwango cha juu cha uwasilishaji wa muktadha wa MC.

Nadharia hii huchukua mtazamo wa kuona tukio la mawasiliano kama kiini cha tafsiri. Mawasiliano yenyewe hutilia mkazo mambo matatu makuu: chanzo cha habari (msemaji au mwandishi), mpokezi wa habari (msikilizaji au msomaji) na nia pamoja na hisia za mwandishi au msemaji (chanzo) kama inavyojitokeza katika kazi yake. Nadharia hii inajaribu kuwasilisha maoni, mawazo, falsafa, itikadi na msimamo wa mwandishi wa MC kwenye ML.

Shannon na Weaver (1949) wanasema kwamba jumbe zinapitishwa kutoka kwa msemaji au mwandishi hadi kwa mpokezi kwa namna ya ishara za sauti au maandishi kulingana na njia iliyoteuliwa kuwasilisha ujumbe wenyewe. Mambo yanayowasilishwa huwa yamebuniwa na anayewasilisha, na mambo yenyewe yanaweza kuwa ya kweli au yasiyo

ya kweli. Pia yanaweza kuwasilisha hisia za aina fulani na vilevile huweza kufungamana na masuala ya kijamii au ya kitamaduni.

Katika nadharia ya mawasiliano, mtafsiri anaweza kuzidisha thamani ya mawasiliano kwa njia mbili: kuboresha matini yake ya LL au kurekebisha MC ili kuondoa dosari au vikwazo vinavyozuia kueleweka vyema kwa ujumbe unaowasilishwa. Mambo yanayoweza kusababisha utata hurahisiswa na mtafsiri kwa madhumuni ya kupitisha vyema kwa mpokezi ambaye anatarajiwa kuelewa ujumbe vyema kupitia kwa mfumo wa kisarufi na kimaana wa LL. Mtazamo wa nadharia hii ni kwamba ujumbe unapaswa upokelewe sawa na vile ambavyo mpokeaji wa MC angeupokea katika LC.

Nadharia hii ilipendekezwa ili kujaribu kutafuta mbinu ambayo inakaribiana na uhalisi wa tafsiri. Hali hii ilitokana na ukweli kwamba lengo la tafsiri ni kuwasiliana na msomaji kwa kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa MC. Ikiwa tafsiri hailengi mawasiliano basi huchukuliwa kama zoezi ambalo halijafanikiwa wala kuwa na manufaa yoyote. Inajaribu kuamsha hisia za msomaji kama ilivyo katika MC. Jambo la muhimu analopaswa kuzingatia mtafsiri ni mpokezi wa ML. Lazima ujumbe umfikie au uwasilishwe kwa namna atakavyoielewa kwa wepesi. Mtafsiri anapotafsiri kwa lengo hili, yeye hufahamu kwamba mpokezi wa ujumbe hatazamii kupata ugumu au utata wowote katika tafsiri anayoisoma. Mpokezi wa matini iliyotafsiriwa anaisoma akijua kwamba hakuna maelezo mengine kando ya tafsiri anayoisoma.

Mtafsiri ana uhuru wa kuboresha MC na kuifanyia marekebisho yanayoweza kufanikisha mawasiliano. Mtafsiri pia husahihisha makosa pale ambapo MC haijaandikwa vizuri. Ana jukumu la kuboresha mantiki na kuhakikisha kwamba matini inatiririka vilivyo. Kwa ujumla, anapaswa kuondoa mambo yote yanayoweza kuwa vikwazo katika uelewaji wa MC. Ingawa tafsiri mawasiliano ni kwa manufaa ya mpokezi, haistahili kupuuza muundo, mtindo, sarufi, muktadha na vipengele vinginevyo vinavyohusu matakwa ya LC. Kwa kila hali, lengo la tafsiri ni kueleweka na hivyo basi huweka ujumbe wazi.

Omboga (1986) alipendekeza tafsiri mawasiliano kuwa ni mwafaka zaidi kwa kuwa ina uwezo mkubwa wa kukabiliana na kiasi kikubwa cha matatizo ya tafsiri. Osano (1997) anashadidia madai ya Omboga kwa kusema kuwa baadhi ya kazi zilizowahi kutafsiriwa vyema zaidi na kufikia upeo wa juu zilichukua mwegemeo wa kimawasiliano ambao hauna matatizo mengi ukilinganishwa na aina nyinginezo za tafsiri.

### 1.7.3 Uhusiano kati ya Nadharia ya Ulinganifu Amilifu na Nadharia ya Mawasiliano

Nadharia ya ulinganifu amilifu inalenga kuibusha maana ya ujumbe wa kimatini iliyo sawa au inayokaribiana zaidi na maana ya kimatini katika MC. Kwa upande mwingine, nadharia ya mawasiliano inalenga kuibua athari kwa msomaji wa ML iliyo sawa na ile iliyoibushwa kwa msomaji wa MC. Katika hali zote mbili, muktadha wa MC ndio uti wa mgongo wa shughuli ya tafsiri. Nadharia hizi hazijifungi kwenye miundo ya lugha kuliko uamilifu wa ujumbe unaowasilishwa. Nia ya mtafsiri ni kuwasilisha lengo la mwandishi wa MC pamoja na namna anavyolieleza.

Nadharia hizi ni za muhimu katika tafsiri wakati lugha zinazohusika, MC na ML, zinatofautiana kimuundo na kufanya tafsiri ya moja kwa moja kuwa ngumu kuielewa. Zote mbili zinajaribu kumfanya msomaji wa ML kuhusisha muktadha wa kimatini na utamaduni wa LL bila kumlazimu kuelewa masuala ya kitamaduni ya LC. Zote zinajaribu kumfanya msomaji wa ML kuuelewa ujumbe kwa urahisi bila kutarajia ugumu au utata. Mtafsiri ana uhuru wa kuyarekebisha makosa yapatikanayo katika MC kabla ya tafsiri. Uhuru huu haupatikani katika nadharia nyinginezo.

Mpokezi wa habari hutiliwa maanani kuliko umbo la kisarufi la matini. Mawasiliano hupitishwa kwa kuteua kipashio ambacho kitawasilisha maana inayolengwa kwa urahisi. Pia nadharia hizi zinalenga kutimiza usahihi wa kimatini katika msingi wa muktadha wa yanayowasilishwa katika MC. Katika mikabala yote miwili, aghalabu ML huwa bora kuliko MC kwa sababu mtafsiri hujaribu kufikia kiwango bora zaidi cha uwasilishaji wa muktadha.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Tuliweka makubaliano na wawasilishaji wa TH katika Shirika la Utangazaji la Kitaifa (KBC) na walikuwa wakitupatia miswada ya taarifa za Kiswahili na za Kikipsigis kwa njia ya barua pepe. Miswada hii ndiyo tuliyofanyia uchanganuzi linganishi ili kubainisha makosa yanayodhihirika katika tafsiri za taarifa zenyewe na kuvitathmini vyanzo vya makosa yenyewe. Baadhi ya miswada inayosheheni mifano tuliyotumia imetolewa kama vielelezo kwenye mijadala yetu katika sura zinazofuata na mingine ambayo haikutumika kudondoa mifano imewekwa kwenye kiambatisho.

Miswada tuliyotumia ilikuwa ya kati ya tarehe 5 Machi hadi tarehe 5 Aprili 2016. Kusudi letu la kufungamanisha miswada na wakati huu ni kule kupatikana kwake ndani ya kipindi cha utafiti wetu. Nyakati tofauti tofauti huwa na mada tofauti tofauti zinazoelezwa kwa kutumia dhana tofauti tofauti. Kwa sababu hiyo, upana huu wa wakati umetuwezesha kutathmini jinsi dhana hizo zimetafsiriwa. Tuliteua siku tatu za kila juma: Jumatatu, Ijumaa na Jumapili. Uteuzi huu umefanywa kwa njia hii ili kuhakikisha kwamba TH za katikati ya wiki na zile za mwishoni mwa wiki zimehusishwa katika sampuli ya miswada. Kigezo kilichotumika kuteua siku tatu za juma ni kwamba hizi ndizo siku za wiki ambazo mtafsiri ambaye ni mzawa wa lahaja ya Kikipsigis huwa zamuni.

Utafiti wetu pia ulihusisha kudurusu vitabu, majarida, tasnifu, majuzuu na kuchakura mtandaoni ili kupanua ujuzi wetu kuhusu masuala ya tafsiri yanayohusiana na mada yetu na tafsiri katika upana wake. Udurusu huu pia ulitubainishia mwanya au mianya iliyohitaji kuzibwa katika taaluma ya tafsiri na kutupa mwelekeo katika suala la utafiti.

Tulitumia mahojiano ili kujaliza uchanganuzi wa miswada ya habari. Tuliwahoji wanahabari wa kitengo cha TH katika kituo cha Kitwek wanaohusika katika ukusanyaji, uandishi, na tafsiri za habari. Kwa kuwa upeo wetu wa utafiti ni kwenye shirika la kitaifa, tuliomba kwanza idhini ya wasimamizi wa shirika hili ili kuturuhusu kutekeleza shughuli yetu kwenye shirika lao.

Mtafiti ni mzawa wa lahaja ya Kikipsigis na alitumia tajiriba yake kuyachanganua miswada ya taarifa za habari ili kubainisha iwapo kuna ulinganifu wa kimawasiliano au dosari zinazosababisha kupotoshwa kwa maana kati ya MC na ML. Alilinganisha na yaliyomo kwenye miswada ya LC, ambayo pia ana tajriba nayo kutokana mafunzo aliyopata kuhusu LC katika ngazi zote za kielimu.

# SURA YA PILI

# AINA ZA TAFSIRI ZINAZOTUMIKA KATIKA TAARIFA ZA HABARI KATIKA KITUO CHA KITWEK

## 2.0 UTANGULIZI

Ubora wa zoezi la tafsiri hutegemea aina ya/za tafsiri inayotumika/zinazotumika kutafsiria matini inayohusika. Kabla ya kuteua aina ya tafsiri itakayotumika ni sharti mtafsiri abainishe ni aina gani ya matini anayoshughulikia kwa sababu kuna aina mbalimbali za matini kama zilivyo aina mbalimbali za tafsiri. Sura hii ilichunguza aina mbalimbali za tafsiri zinazotumiwa kutafsiria TH za kituo cha Kitwek pamoja na kutathmini utendakazi wa kila mojawapo ya aina za tafsiri zinazohusika. Kabla ya kuchunguza aina za tafsiri tutaanza kwa kubainisha aina mbalimbali za matini ili kuonyesha ni aina ipi ya matini ambayo TH zinajikita.

## 2.1 AINA ZA MATINI ZA TAFSIRI

Matini za tafsiri zinaweza kuainishwa katika makundi mbalimbali kwa kufuata vigezo tofauti tofauti. Kuna matini za kiteknolojia, kifasihi, kisiasa, kisayansi, utawala n.k. Uainishaji wa matini hudhibitiwa na dhima zinazotekelezwa na matini zenyewe. Buhler (1965) alipendekeza dhima tatu kuu za lugha:

(i) Dhima elezi: lugha hutumika kwa dhima ya kueleza hisia za mtu binafsi bila kujali hadhira. Mtafsiri hajali hadhira ambayo itasoma au kusikiliza makala yake. Kiini cha dhima hii ni mwandishi wa matini inayorejelewa.

(ii) Dhima arifu: katika dhima hii, lugha hutumika kutolea taarifa na kiini cha dhima yenyewe ni ukweli. Lugha inayotumika katika TH tunazoshughulikia katika uchunguzi wetu inadhibitiwa na dhima.

(iii) Dhima amili: lugha hutumika kwa madhumuni ya kuibua hisia fulani au kuchochea hadhira ili kuitikia ujumbe wa matini kwa namna fulani. Kiini cha dhima amili ni hadhira ya matini inayohusika.

Kwa kuzingatia dhima hizo, matini zinazotafsiriwa zinaweza kuainishwa ifuatavyo:

### 2.1.1 Matini Elezi

Matini za aina hii huegemea zaidi kwa mwandishi wa matini yenyewe. Mwandishi hutumia lugha kueleza sifa zake bila kujali anayelengwa. Mifano ya matini hizo ni kama fasihi iliyobuniwa kwa makini kama mashairi na aina nyinginezo za riwaya au tamthilia, kauli za kimamlaka kama vile nyaraka za kisiasa na za kisheria, matini za kifalsafa na wasifu.

### 2.1.2 Matini Arifu

Matini hizi zinahusu mada ya maarifa au taaluma kama uchumi, uanahabari, ualimu n.k. Matini hizi huwa katika maumbo sanifu kama vile katika vitabu, majarida, taarifa na ripoti za kiakademia kama tasnifu. Matini arifu huwa na sifa mbili kuu; kwanza inatafsiriwa na idadi kubwa ya watafsiri walioajiriwa na mashirika ya kimataifa na kampuni kubwa kubwa na pili, asilimia kubwa ya matini arifu huwa zimeandikwa vibaya na mara nyingi huwa na taarifa zisizo za kweli na kwa hivyo ni jukumu la mtafsiri kufanya masahihisho yanayohitajika ya maudhui na mtindo wa lugha. Tafsiri za matini za aina hii zinatarajiwa ziwe bora zaidi kuliko MC.

### 2.1.3 Matini Amili

Matini hizi zimeegemea upande wa wasomaji au hadhira na zinalenga kuibua hisia za msomaji na kumfanya afikirie au atende kwa namna fulani kwa mfano matangazo ya biashara au redio, maelekezo au propaganda, maombi na fasihi pendwa. Kuna mambo yanayopaswa kuzingatiwa na mtafsiri wa matini amili: uhusiano baina ya mwandishi na hadhira sharti uonyeshwe bayana kupitia zana za kiisimu na ni lazima iandikwe kwa lugha inayoeleweka kwa hadhira mara moja. Hadhira isipoeleweka mtafsiri hatakuwa ametekeleza matarajio ya mwandishi.

Kutokana na uainishaji wa matini kwa kutegemea dhima, ni bayana kwamba TH zinachota sifa kutokana na kila mojawapo ya aina hizo. Kutokana na dhima elezi, baadhi ya maudhui ya TH hayalengi kuibua hisia za HL, kwa mfano kuna habari kama vile za utabiri wa hali ya anga ambazo aghalabu haziathiri hisia za sehemu ya hadhira au hadhira nzima. Hii inafanya TH kuchukuliwa kama matini elezi. Lengo kuu la TH ni kuarifu au kutoa taarifa ili kuwasilisha ukweli fulani kwa hadhira. Dhima hii hufanya TH kuchukuliwa kama matini arifu. Kwa upande mwingine, uanahabari kama taaluma iliyo na uamili wa kuwasilisha habari kwa hadhira ili kuibusha mwitiko fulani huweka TH katika kundi la matini amili.

## 2.2 AINA ZA TAFSIRI

Uainishaji wa matini katika makundi mbalimbali ni muhimu kwa sababu aina mahsusi ya matini ndiyo inayomwongoza mtafsiri katika uteuzi wa mbinu mwafaka za kutumia katika tafsiri yake. Kwa mfano, matini amili huwa na mwelekeo wa kutafsirika zaidi kwa kutumia tafsiri ya mawasiliano. Vilevile, zoezi la tafsiri linapofanyika kibiashara,

gharama za tafsiri hupangwa kulingana na aina ya matini. Mambo haya humchochea mtafsiri kuteua aina mwafaka zaidi ya kutumia kutafsiri matini za aina tofauti tofauti ili kutimiza malengo anayowekea zoezi lake la tafsiri. Sehemu hii itatathmini aina mbalimbali za tafsiri zinazotumiwa na watafsiri wa TH katika kituo cha Kitwek.

Omboga (1986) aliorodhesha aina mbalimbali za tafsiri kama zifuatazo: tafsiri ya moja kwa moja, tafsiri maana, tafsiri huru na tafsiri mawasiliano. Uainishaji wake ni sawa na ule wa Ali (1980) ambao unajumuisha aina hizo zote za tafsiri isipokuwa tafsiri mawasiliano. Aina hizi za tafsiri ndizo zinazochukuliwa kuwa miongozo ya tafsiri. Watafsiri hutumia aina moja au zaidi ya miongozo hii kwa njia ya kutegemeana. Katika aina moja ya matini, zaidi ya aina moja ya tafsiri huweza kutumika.

Newmark (1988) aliorodhesha aina nyinginezo za tafsiri kama vile tafsiri kihuduma, tafsiri wazi, tafsiri habari, tafsiri kiutambuzi na tafsiri kiakademia. Japo kuna aina hizi nyingine za tafsiri zilizojitokeza baada ya zile zilizokwisha kutajwa, uchanganuzi wetu utatilia maanani aina hizo nne za tafsiri; tafsiri ya moja kwa moja, tafsiri huru, tafsiri maana na tafsiri mawasiliano. Sababu kuu ya kuzingatia aina hizi ni kwamba aina za tafsiri zilizojitokeza baadaye zinachota sifa kutoka kwa kila mojawapo ya aina hizo nne.

### 2.2.1 Tafsiri ya Moja kwa Moja

Beekman na Callow (1974) walifafanua tafsiri ya moja kwa moja kama tafsiri inayopitisha vipengele vya LC hadi LL kwa namna ambavyo maafikiano makubwa baina ya lugha hizo hudhihirika. Huzingatia usahihi, uhalisi na uaminifu wa kupitisha ujumbe. Tafsiri ya moja kwa moja inapotekelezwa kikamilifu, hufikia kiwango ambacho neno

katika MC linatafsiriwa kwa neno lililo kisawe chake katika ML. Husisitiza zaidi kuwepo kwa ulinganifu wa vipengele kama maana, umbo la LC na LL katika mchakato wa tafsiri.

Kwa kuwa aina hii ya tafsiri husisitiza maafikiano ya moja kwa moja kati ya MC na tafsiri yenyewe, tafsiri inayotokana na aina hii ya tafsiri huwa ni ya neno kwa neno, maana kwa maana na umbo kwa umbo. Maneno yote hupewa visawe katika LL na husomeka kama MC. Tafsiri hii hutilia mkazo kufikisha ujmbe katika LL bila kubadilisha chochote katika LC. Matini hutafsiriwa kwa uhalisi, uaminifu na usahihi. Inadhihirisha muundo, mtindo, umbo na sarufi ya MC.

Matatizo mengi yanahusishwa na tafsiri ya aina hii kutokana na kutafsiri neno kwa kisawe chake katika LL bila kujali tofauti za kimfumo baina ya lugha zinazohusika katika tafsiri. Sentensi zinazoibushwa hukosa mshikamano na mtiririko unaotarajiwa kuwepo. Lengo la mwandishi wa MC aghalabu haliwasilishwi kwa HL. Tafsiri ya aina hii hujaribu kulazimisha sura ya LC kwenye umbo la LL bila kutilia maanani kuwa kila lugha huwa na upekee wake wa jinsi ya kuweka vipashio vya kisarufi, maumbo ya maneno na sauti katika mpangilio wake.

Kasoro nyingine inayodhihirika katika tafsiri ya moja kwa moja ni kwamba HL hupuuzwa. Hii ni kwa sababu tafsiri hii hujikita zaidi katika fikra na mtazamo wa mwandishi wa MC kuliko jinsi inavyozingatia matarajio ya HL na lugha yao na jinsi ambavyo hadhira hiyo inavyoelewa na kufasiri maana. Katika tafsiri hii maana huathirika vibaya na kuvurugika zaidi. Ubora wa tafsiri hudhibitiwa na kanuni za kisarufi pamoja na namna ya kuwasilisha maana, jambo ambalo halitiliwi maanani katika tafsiri ya moja

kwa moja. Ukiukaji wa kanuni hizo huzua mawasiliano yaliyopotoshwa kama inavyodhihirika katika mfano huu:

Kielelezo 1

| | |
|---|---|
| **Shughuli ya upigaji kura inaendelea katika kaunti ya Kericho** na eneo bunge la Malindi. Katika kinyang'anyiro cha Useneta, kaunti ya Kericho, mgombeaji wa chama cha KANU, Paul Sang alilalamika kuwa maajenti wa chama hicho walifurushwa kutoka vituo saba vya kupigia kura katika eneo bunge la Belgut na kwenye vituo viwili katika eneo bunge la Kipkelion Mashariki. **Sang ameiomba tume hiyo kuingilia kati kwa haraka suala hilo** huku akionya kuhusu juhudi za mrengo wa Jubilee za kujaribu kuiba kura kwenye uchaguzi huo mdogo. | ***Tesei tai en inguni en oret ne kararan lewenisiet en kaunti nebo Kericho*** *en lewenisiet nepo senate ole kaimuch kobit kaimutik kan kotoikei lewenisionotok...Kebor kangunyngunyet ne borchingei ng'echeret en chamaitab Kanu Paul Sang akobo alak eng biik che telelchin chamainoton chebo chamainyi chekakiwekta eng ketesiosiek 7 eng komasta nebo Belgut ak ketesiosiek alak 2 eng komasta nebo Kipkelion kongasis.* ***Kasom kibagengeinoton kochutchi kwen yautionotok*** *katiny biriikab kura loo che kakiwekta eng ketesiet nebo Kabartegan ak ketechi chamaitab Jubilee koistoegei tiemetab kochor kurainik.* |

1. Sang ameiomba tume hiyo **kuingilia kati** kwa haraka suala hilo…

   *Kasom kibagengeinoton* ***kochutchi kwen*** *eng chokchinet yautionotok…*

   (Aliomba tume hiyo **kuingilia kati** kwa haraka suala hilo…)

Mfano uliotolewa hapo juu hudhihirisha namna mtafsiri amelazimisha maumbo ya LC katika LL. Dhana *kuingilia kati* ni nahau ambayo mtafsiri ameng'ang'ania kutafsiri kwa njia ya moja kwa moja pasipo kutilia maanani hali kwamba nahau katika lugha moja si lazima iwe na kisawe chake katika lugha nyingine. Matumizi ya maelezo au neno fidia lingeweka wazi maana ya kile kinachowasilishwa katika MC kwa namna ambayo ingeeleweka zaidi kuliko jinsi ambavyo imewasilishwa katika tafsiri hiyo ya moja kwa moja.

Tafsiri hii hupuuza mambo ambayo ni muhimu katika zoezi la tafsiri kwa kuwa haijali matakwa ya LL kwa kulazimisha kuchukua maumbo, muundo, mtindo na sarufi isiyokuwa yake. LL hulazimika kuchukua dhana ambazo hazieleweki na tafsiri inayotokea hukosa mawasiliano. Tafsiri ya moja kwa moja husababisha upatano wa maneno fulani katika LL ambao hauna maana yoyote au maana inayoibushwa huwa kinyume na masharti ya LL. Pia maana iliyo kinyume na itikadi na falsafa za LL huwasilishwa. Mfano ufuatao unadhihirisha upatano wa maneno katika MC na ML lakini ujumbe wa MC umepotoshwa.

Kielelezo 2

| | |
|---|---|
| Timu ya kandanda ya Liverpool ilitwaa ushindi katika mechi ya marudiano iliyochezwa baina yake na timu ya Barcelona leo alasiri. Bao la pekee la timu hiyo lilifungwa na Gerrand. **Mchezaji huyo wa kiungo cha kati alifunga bao lililoipatia timu hiyo ushindi** katika dakika ya 68. | *Konyor kobelishet timitab Liverpool en ureriet ne koketyingei ak timitab Barcelona en koskoleng'utab ra. Golit ne inegei en urerionotok ko konyorchingei urerenindet Gerrand.* ***Katiorindonoton bo kebebertab kwen ko kager golit ne koipchi timinoton kobelishet*** *en dakiket ab 68.* |

2. Mchezaji huyo wa kiungo cha kati **alifunga bao** lililoipatia timu hiyo ushindi.

   *Katiorindonoton bo kebebertab kwen ko* ***kager golit*** *ne koipchi timinoton kobelishet.*

   (Mchezaji huyo (wa kandanda) wa sehemu ya kati **alifunga bao** lililoipatia timu hiyo ushindi)

Maana inayojitokeza katika tafsiri ya dhana zilizokolezwa si wazi kwa sababu tafsiri hiyo inaibusha taswira ya mhusika anayechukua kitu fulani na kufunika au kufunga uwazi fulani. Ugumu wa kueleweka kwa tafsiri hii unatokea kwa misingi kwamba mchezo unaozungumziwa katika MC ambao ni kandanda una ugeni wa kiwango fulani katika

utamaduni na itikadi za lugha ya ML. Maana ingekuwa wazi au kukaribiana zaidi na ile iliyoko katika MC iwapo mtafsiri angetumia njia ya maelezo au ufafanuzi. Kulazimishwa kule kwa tafsiri ya dhana namna ilivyo katika MC kumesababisha kukosekana kwa UM kati ya MC na ML kulikotokana na mtafsiri kutaka kuhifadhi maumbo ya MC katika ML.

Omboga (1986) alieleza kwamba kwa sababu ya kusisitiza mawiano ya moja kwa moja, usahihi na uhalisi, tafsiri inayojitokeza huathiriwa na miundo ya lugha ya makala. Anasisitiza kuwa fauka ya kuelemea katika lugha ya makala pia huelemea upande wa mawazo ya mwandishi wa makala hiyo. Anasema kwamba japo tafsiri hukusudiwa msomaji katika LL tafsiri za moja kwa moja hazimsaidii msomaji huyo sana. Hii ni kwa sababu tafsiri hizi zinajifunga sana katika makala na hivyo kushindwa kufanikisha mawasiliano.

Tafsiri ya aina hii huwa vigumu kueleweka kwa sababu ni vigumu kulinganisha lugha mbili. Hakuna lugha zozote mbili ambazo zinalingana kwa kila sifa na kule kulazimisha kuwepo kwa maafikiano ya moja kwa moja kati ya vipengele vya lugha zenyewe kunasababisha kutofaulu kwa shughuli ya tafsiri kwa sababu kutaibuka upotoshi mkubwa wa maana inayowasilishwa na mwandishi wa matini na hivyo kutofikia malengo ya tafsiri husika. Pia inapunguza masharti au kanuni za LL. Mfano ufuatao unadhihirisha namna mtafsiri amelazimisha kuwepo kwa maafikiano ya moja kwa moja kulikosababisha upotoshi wa maana.

Kielelezo 3

| | |
|---|---|
| Valentine Kipketer na Winfred Kimitei ndio washindi wa mbio za mwaka huu za mama wa-taifa za Half Marathon. Zaidi ya watu elfu-40 walijisajili kushiriki katika makala ya tatu ya mbio hizo yaliomalizikia uwanja wa taifa wa Nyayo. **Mbio hizo zilihudhuriwa na mke wa kwanza wa Rwanda** Jeanette Kagame. Naibu rais William Ruto na mkewe Rachel Ruto pia walishiriki kwenye mbio hizo. | *Kaibelis Valentine Kipketer ak Winfred Kimitei eng labatet ne kakiim nebo tetutietab First lady half marathon ne kakiay eng karonetab raini. Kosirgey biik che sirey 40,000 eng kebebertaab somok nebo labata nitok ne kabeek eng kiwanjetaab Nyayo.* ***Komiten en ng'waechoton kwondo ne tai nebo emetab Rwanda*** *lady Jeannette Kagame. Kamiten kora eng labatanotok rubeywotab president William Rutto ak kwondonyin Rachael Rutto.* |

3. Mbio hizo zilihudhuriwa na **mke wa kwanza** wa Rwanda…

   *Komiten en ng'waechoton* **kwondo ne tai** *nebo emetab Rwanda…*

   (**Mke wa kwanza** wa nchi ya Rwanda alihudhuria mbio hizo.)

Ufasiri wa tafsiri ya *mke wa kwanza* kwa HL ni jambo gumu kwa sababu dhana yenyewe ni tatanishi kwa kuwa inaweza kubeba maana nyingi. Inaweza kutumiwa kwa maana ya mke anayekuwa wa kwanza kufanya au kuhusika katika jambo lolote. Utata huu wa kimaana hauzuki tu kutokana na namna dhana yenyewe ilivyotafsiriwa bali utata wenyewe una usuli katika MC ambapo matumizi yenyewe bado yanakanganya hata hadhira ya MC. Inawezekana kwamba dhana hiyo ilitokana na tafsiri ya moja kwa moja kutoka lugha nyingine bila kuzingatia muktadha wa matumizi yake. Tafsiri inayofanywa kwa njia hii huwa ni kwa manufaa ya mpokezi wa ML ambaye ana umilisi wa kiwango cha chini cha LC.

Licha ya matatizo mbalimbali ya tafsiri ya moja kwa moja yaliyokwisha kuangaziwa, haina maana kwamba tafsiri hii haina manufaa yoyote. Newmark (1982) anasema kwamba ingawa tafsiri ya moja kwa moja ina upungufu mwingi, inapaswa kuchukuliwa kuwa hatua ya mwanzo katika kufikia tafsiri bora zaidi. Kwa upande mwingine kuna hali mbalimbali ambapo kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya maumbo yapatikanayo katika MC na yale ya ML, na kutafsiriwa kwayo kwa njia ya moja kwa moja kunazalisha tafsiri inayoweza kueleweka barabara pasipo kusababisha utata wowote wa kimaana. Hata hivyo, uhusiano wa moja kwa moja unaozungumziwa hapa ni wa kisadfa na haina maana kwamba lugha fulani mbili zinaweza kulingana katika hali zote.

### 2.2.2 Tafsiri Huru

Aina hii ya tafsiri inajali habari au maudhui kuliko masuala mengine. Haijishughulishi na mtindo, muktadha, umbo na sarufi na lengo lake ni kuwasilisha ujumbe ulioko katika MC bila kujali msamiati, sentensi na mtindo uliotumika. Mbinu hii ya tafsiri hukaribia sana kuwa maelezo kwa muhtasari wa ujumbe asilia.

Kielelezo 4

| | |
|---|---|
| Polisi wanachunguza kisa ambapo mmoja wa walinzi wa seneta wa kaunti ya Nairobi Mike Sonko aliuawa kwa kupigwa risasi na kunyang'anywa bunduki yake katika mtaa wa Mwiki jijini Nairobi. **Mlinzi huyo alipigwa risasi kichwani na kufariki alipokuwa akitibiwa** katika Nairobi Hospital hapo jana. Ilisemekana mlinzi huyo Bakari Tsuma alikuwa amemsindikiza Seneta huyo hadi kwenye eneo la Gigiri usiku wa manane Ijumaa na kuelekea kwake nyumbani katika mtaa wa Mwiki ambapo alipigwa risasi. Duru ziliarifu kwamba mlinzi huyo alipigwa risasi na watu watatu waliojihami kwa bunduki aina ya AK-47 na bastola. Polisi wanasema kufikia sasa hakuna mtu aliyekamatwa kuhusiana na tukio hilo. Kwa upande wake **Sonko anasema sasa anahofia maisha yake kufuatia mauaji hayo.** | *Tese tay ak chikilishet polis akobo yautiet ne kokimwook ak kebar, yeitya keib bundukit ne kotinye ribindetab senator eng county nebo Nairobi Mike Sonko eng komastaab Mwiki yutok nairobi.* ***Mwaat kele kokimwook afisaya notok komosta nebo metit ak koit kobeet sobenyi kotesetay ak kanyayset*** *eng sipitalitaab Nairobi eng betutab amut. Ko kaimuut Sonko kwo Gigiri eng betutab komut kasi ribindet notok ne naat ko Bakari Tsuma ak koweek koinyi eng mwiki ole kokimong'chi ak kemwook. Kamwa Sonko ak polis kole kokimwook chichotok biik 3 che kotindoy bundukitab AK47 kobot pistolishek.Kakomwa Polis kole tesetay ak chikilishet konay kole ng'o ne koisuldoe yautit notok. Eng komastanyi ko* ***kamwa Sonko kole mitey akine sobenyi ole ng'oi amu imuchi kokocheng'e biik chotok.*** |

4. Mlinzi huyo alipigwa risasi kichwani na kufariki alipokuwa akitibiwa…

   *Mwaat kele kokimwook afisaya notok komosta nebo metit ak koit kobeet sobenyi kotesetay ak kanyayset…*

   (Inasemekana kuwa afisa huyo alipigwa risasi sehemu ya kichwa na akafikia kufariki akiendelea na matibabu.)

Katika tafsiri hii, kuna maelezo zaidi yametolewa ambayo hayakupatikana katika MC lakini yamehusishwa katika ML kama vile *inasemekana kuwa*, *sehemu ya* na *akafikia.* Pia dhana ya *mlinzi* imetafsiriwa kama *afisa.* Hali hii imekengeusha ujumbe wa kimatini uliokusudiwa kuwasilishwa na mwandishi wa MC kwa sababu tafsiri yenyewe imechukua sura ya ufafanuzi wa MC badala ya tafsiri yake. Kwa namna nyingine tafsiri hii inaweza kuangaliwa kama MC iliyotolewa muhtasari kwa sababu japo ujumbe wa MC unaweza kujitokeza ndani ya maelezo au ufafanuzi unaosababishwa na uhuru mwingi

ajipatiao mtafsiri, ni bayana kwamba kuna nyongeza nyingi zinazofikia hadhira ya ML ambazo hazipokelewi na hadhira ya MC. Mfano ufuataao, ulionukuliwa kutoka kielelezo 4, unadhihirisha namna uhuru wa mtafsiri unaweza kusababisha nyongeza katika ML:

5. Sonko amesema sasa anahofia maisha yake kufuatia mauaji hayo.

   *Kamwa Sonko kole mitey akinei sobenyi ole ng'oi amu imuchi kocheng'e biik choto.*

   (Sonko amesema kwamba hata yeye maisha yake yamo hatarini kwa sababu watu hawa wanaweza kuwa wanamsaka.)

Maneno kama vile *hata yeye*, *yamo hatarini* na *kwa sababu watu hawa wanaweza kuwa wanamsaka* hayakuwemo katika MC lakini mtafsiri amejipa uhuru na kuyachopeka katika ML. Upenyezaji wa vipengele hivi vipya hutoa ufafanuzi wa habari kuliko inavyohitajika. Ingawa mtafsiri anaweza kushawishika kuongeza dhana zisizopatikana katika MC kwa lengo la kutaka kutajirisha maana, wakati mwingine nyongeza hii inaweza kusababisha kinyume cha lengo lake kwa sababu badala ya kufanya maana iwe wazi, inaweza kuipotosha.

Kwa sababu ya kupuuza mambo mengi na kujipa uhuru mwingi, aina hii ya tafsiri haifanikishi mawasiliano. Tafsiri huru inaweza kuzidisha au kupunguza uzito na thamani ya mawazo katika LC na hivyo kuzorotesha mawasiliano. Kule kuongeza mambo mapya kunazidisha sifa za matini. Mambo yenyewe yana uwezo wa kuleta mabadiliko kwenye umbo la matini na kusababisha kuondolewa kwa sifa halisi za MC.

### 2.2.3 Tafsiri Maana

Newmark (1982) alifafanua tafsiri maana kama aina ya tafsiri inayojaribu kwa namna inavyowezekana kuwasilisha maana kamili ya ujumbe katika muktadha wa MC ili kuhakikisha kwamba maana inayopitishwa ndiyo inayotarajiwa kupitishwa na mwandishi wa MC. Alieleza kuwa muwala na muumano wa kisarufi kati ya maneno, virai, vishazi na sentensi ni jambo la muhimu linalopaswa kuzingatiwa katika tafsiri maana. Vilevile, mpangilio wa maneno na ukubalifu wa maneno yenyewe katika sentensi za ML unastahili kutiliwa maanani katika tafsiri ili maana ya MC iweze kufikia HL.

Tafsiri ya aina hii inajikita katika nadharia ya isimu iliyopendekezwa na Cartford na Nida. Hujaribu kuwasilisha maana kwa kadri iwezekanavyo katika miundo na sarufi ya LL na mipaka ya maana ya lugha yenyewe. Aina hii huhakikisha kwamba maana kamili na ya ujumla katika MC inatafsiriwa. Inajikita katika miundo na misingi ya MC lakini haipunguzi kanuni za LL. Mfano ufuatao unaonyesha namna maana ya kimatini inaweza kudumishwa pasipo kung’ang’ania kudumisha umbo la MC katika ML:

Kielelezo 5

| | |
|---|---|
| Usalama umeimarishwa mjini Narok na viungani mwake; ili kukabiliana na visa vyovyote vya uhalifu wakati wa maadhimisho ya sherehe za Pasaka. Akiongea na shirika la habari la KNA, kamishna wa Kaunti ya Narok, Moffat Kangi ambaye pia ni mkuu wa maswala ya usalama katika Kaunti hiyo alisema doria zimeimarishwa na kwamba maafisa wa usalama wamewekwa katika hali ya juu ya tahadhari kuhakikisha kwamba wenyeji na pia wageni wanafurahia Pasaka bila kisa chochote kibaya. Alisema doria za maafisa wa traffiki kwenye barabara kuu ya Nairobi kuelekea Narok zimeimarishwa kuhakikisha kwamba waendeshaji magari wanazingatia sheria za traffiki. Hayo yanajiri baada ya Inspekta Generali wa Polisi, Joseph Boinnet, kutoa tahadhari kote nchini kuhusu uwezekano wa kutokea mashambulizi ya kigaidi wakati wa sherehe za Pasaka na kushauri wakenya kuwa waangalifu zaidi. *Wakati huo huo,* watalii wa humu nchini na pia wa kimataifa wanazidi kumiminika kwenye mbuga ya wanyama ya Maasai Mara; wakati huu wa sherehe za Pasaka. **Mwenyekiti wa baraza la kitaifa la watu wanaoishi na ulemavu Dr. David Sankok, ambaye pia ni mmiliki wa hoteli kwenye mbuga ya wanyama ya Maasai Mara, ameripoti juu ya ongezeko la wageni la asilimia 85 msimu huu wa pasaka.** | *Kakikimit ripsetab kalyet eng taonitab Narok koboto komoswek alak chenekitchin asikekirinda tetutik chebo kiplelutinik eng igorta nebo Pasaka. Kongalalchin ketesyani, komwa County Commissioner nebo Narok, Moffat Kangi ne inendet kora ko neo nebo ripsetab kalyet eng kaunti notok kole kakikimit ribseet ak mitei eng chibilindo ribiikab kalyet asikoker kole kabaibachi mengingab komasatak koboto kiprutainik cherutachin komasatak igorta nematindoi kaimut ake tugul. Kamwa kole kakikimit chigilisiet nebo traffic eng oret ne o nebo Nairobi- Narok asikomuch kosub ngatutik tugul chebo oret ketikab karishek. Katestai nitok eng kasarta nekokon kateunet Inspector General nebo police Joseph Boinnet, eng emet komugul kateunet ne komwa kole imuch kobit kabokchinet kobun kiboriotinik eng kasari ba igorta nebo Easter ak kosom biikab emoni kotebi eng chibilindo nebo barak. Eng kasaratak, kotesetai kiprutainik chebo emoni koboto chebunu emontinwek chebo sang korutachin kaptiongin nebo Maasai Mara Game Reserve eng igorta nebo Easter. **Kamwa Dr. David Sankok, ne inendet ko nebo ngecheret eng council nebo poror nebo biik chetindoi kewelutik eng borwek kwak ak kora ko nebo makaweshek chemitei eng kaptiongin nebo Maasai Mara kole kiprutainik che koimuch koitita ko kebebertab 85 eng bokol en kasarta nitok bo Pasaka.*** |

6. Mwenyekiti wa baraza la kitaifa la watu wanaoishi na ulemavu, Dr. David Sankok, ambaye pia ni mmiliki wa hoteli kwenye mbuga ya wanyama ya Maasai Mara, ameripoti juu ya ongezeko la wageni la asilimia 85 msimu huu wa Pasaka.

   *Kamwa Dr. David Sankok, ne inendet ko nebo ng'echeret eng katuyetabge nebo poror nebo biik che tindoi kewelutik en borwek kwak ak kora ko nebo makaweshek che mitei en kaptiong'in nebo Maasai Mara kole kiprutoinik che koimuch koitita ko kebebertab 85 en bogol en kasarta nitok bo Pasaka.*

> (Dr. David Sankok, ambaye ni mwenyekiti wa baraza la kitaifa la watu walio na matatizo katika miili yao na pia ni mmiliki wa hoteli kwenye mbuga ya wanyama ya Maasai Mara amesema kuwa wageni waliofika ni sehemu ya 85 kwa mia katika msimu huu wa Pasaka)

Tafsiri inayotokea kutokana na mfano wa hapo juu inaonekana kuwa ndefu ikilinganishwa na MC. Hii ni kwa sababu mtafsiri ametilia maanani tofauti za kimuundo kati ya LC na LL, na akapania kudumisha maana ipatikanayo katika MC licha ya tofauti hizo. Mtafsiri ametumia ujuzi wa tofauti hizo kutafsiri vifungu fulani kwa kutumia maelezo tofauti na yale yanayopatikana katika MC lakini maana iliyokusudiwa kuwasilishwa imehifadhiwa. Jambo hili ni muhimu kwa sababu huhakikisha kwamba ujumbe unawasilishwa kwa kuzingatia miundo ya lugha zote mbili kwa sababu maana ya maneno haipatikani tu katika maneno bali pia mitindo na miundo ya makala. Maana ya neno huzingatiwa katika muktadha wake katika sentensi na muktadha wa matini au muktadha wa kitamaduni wa MC.

Kwa kuwa muktadha na utamaduni ni vipengele vya muhimu vinavyoathiri zoezi la tafsiri, mtafsiri anafaa kuvizingatia ili kuepuka kutokea kwa hali ya kupotoshwa kwa maana katika mawasiliano pamoja na kudumisha uhalisi na thamani ya MC. Newmark (1982) anasema kwamba tafsiri maana hujifunga kwenye utamaduni wa lugha ya matini inayotafsiriwa. Madhumuni ya tafsiri maana kubakia katika miundo, taratibu na utamaduni wa lugha ya matini ni kumpa msomaji mwongozo wa kupata maana. Kwa sababu hiyo, ni sharti maana inayowasilishwa ifungamanishwe na muktadha. Katika mfano ufuatao, mtafsiri ametumia baadhi ya dhana ambazo si visawe vya zile

zipatikanazo katika MC lakini zimewasilisha maana iliyolengwa kutokana na kule kuhusisha matumizi yake na muktadha.

Kielelezo 6

| | |
|---|---|
| **Cameroon imewahukumu kunyongwa wanamgambo 89 wa kundi la kigaidi la Nigeria la Boko Haram.** Wanamgambo hao walipatikana na hatia ya kutekeleza ukatili na mahakama ya kijeshi ya Cameroon kutokana na kuhusika kwao katika mashmbulizi kadhaa ya kigaidi **katika kisiwa kilichoko kaskazini mwa nchi hiyo kwenye mpaka na Nigeria.** Cameroon ilipitisha sheria za kukabiliana na ugaidi mnamo mwaka wa 2014 ambao adhabu yake ni kifo. Waathiriwa hao 89 ni kati ya wanamgambo 850 waliotiwa nguvuni nchini humo na kuhusishwa na kundi la Boko Haram. Kufuatia kubuniwa kwa sheria hizo, shirika moja la kutetea haki za binadamu limetaka sheria za Cameroon kufanyiwa marekebisho. Mamia ya watu wameuliwa kwenye visa tofauti vya mashambulizi ya kigaidi nchini Cameroon tangu ilipochangia kikosi cha jeshi la kanda hiyo la kukabiliana na ugaidi mwaka jana. Katika siku za hivi majuzi wanamgambo wengi wameripotiwa kujiingiza **kwenye kisa cha ulipuaji wa kujitoa mhanga.** | ***Kaigochi emetab Cameroon kerkongiet nebo meet membaek 89 chebo kunditab kiboriotinik nebo Boko Haram kobun emetab Nigeria.*** *Kokirwokchi kiboriotinichoto eng kapkirwok nebo asikarikab luget eng lelutik chebo kasuldaetab boisionik chebo chelesosnatet ak kabokchinosiek che terter* ***en ikwembeiyot nemi komosta nebo murot katam nebo emetab Cameroon ole tetegei ak kiwato nebo emetab Nigeria.*** *Kiisirto emetab Cameroon ngatutik cheesio yautikab chelesosnatet eng kenyitab 2014 ne kiti kole kigochini kerkongietab meet agetugul nekakinyor kosuldae yautichoto. Bichoto 89 chekokinam koboto alak 850 chekikakinam eng Cameroon ak kirwokchi eng lelutik kele tinyegei tiliandit ak Boko Haram. Kosubgei ak kerkongiet noto bo meet ko koimongei kibagengeisiek cheborchingei imandap kipkosobei kobun emonoto ak kokon kurset nebo keyachi walutik kapkirwok nebo emetab Cameroon. Kikobet sobonwekwak bogolusiekab bik eng kabokchinosiek chekikebaorianchi eng emetab Cameroon kongete ngap kochut asikarichi chebo luget poriet nekitokchini kiboriotinik chebo Boko Haram eng kenyit nekosirtoi. Mwaat kele en kasarta ne kosirtoi ko kokebaorionchi kiboriotinik che begu* ***en yautietab katyolsietab kistoege sobeet.*** |

7. Cameroon imewahukumu kunyongwa wanamgambo 89 wa kundi la kigaidi la Nigeria la Boko Haram.

   *Kaigochi emetab Cameroon kerkongiet nebo meet membaek chebo kunditab kiboriotinik nebo Boko Haram kobun emetab Nigeria.*

   (Nchi ya Cameroon imetoa adhabu ya kifo kwa washiriki 89 wa kundi la magaidi la Boko Haram kutoka nchi ya Nigeria.)

Ingawa maelezo yaliyotolewa kwenye tafsiri yanatofautiana na yaliyo katika MC, maana inayowasilishwa ni ile ile. Kifungu *imewahukumu kunyongwa* inabeba maana ile ya *imetoa adhabu ya kifo* kwa sababu nia ya kuwanyonga wanamgambo wanaozungumziwa ni kuwaadhibu kwa njia ya kuwasababishia kifo au kuwaua. Uchopekaji wa dhana *nchi ya* kabla ya *Cameroon* na *Nigeria* ni kwa lengo la kutajirisha maana.

Katika tafsiri maana, kipengele cha maana hupewa nafasi muhimu. Ili kupitisha ujumbe, mtafsiri anapaswa kuwa mbunifu hasa anapokumbana na aina fulani ya msamiati. Tafsiri maana inaruhusu neno katika LC kutafsiriwa kwa namna nyingi kwenye LL kwa kutegemea muktadha wa matumizi yake. Uhuru huu unaafiki tafsiri ya dhana zitumikazo katika TH kwa kuwa mara nyingi mtafsiri hulazimika kuchunguza maana ya maelezo kwenye habari kisha akawazia jinsi atakavyowasilisha kwa HL. Katika muktadha huu, si lazima neno liwe na uwiano au usambamba wa moja kwa moja kati ya LC na LL bali jambo la muhimu zaidi ni maana ya kimatini.

### 2.2.4 Tafsiri Mawasiliano

Tafsiri hii ilizuka kutokana na udhaifu uliodhihirika katika aina zile nyingine za tafsiri. Wananadharia waliopendekeza nadharia ya mawasiliano walikuwa wanajaribu kutafuta mbinu ambayo inakaribiana na uhalisi wa tafsiri. Suala hili lilitokana na ukweli kwamba tafsiri ina lengo la kuwasiliana na msomaji kwa kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa MC. Ikiwa tafsiri hailengi mawasiliano huchukuliwa kwamba haijafanikiwa na haina manufaa yoyote.

Tafsiri mawasiliano hujaribu kuamsha hisia za msomaji kama ilivyo katika MC. Jambo muhimu katika tafsiri ya aina hii ni mpokeaji wa matini. Mtafsiri anapotafsiri ni sharti afahamu kwamba mpokeaji wa ujumbe hatazamii ugumu au utata wowote katika tafsiri anayosoma. Msomaji wa tafsiri husoma akijua kwamba hakuna maelezo mengine yanayopatikana nje ya tafsiri anayoisoma. Mtafsiri hutoa maelezo kwa nia ya kuufanya ujumbe kuwa dhahiri katika ML. Kwa kila hali, tafsiri hii hulenga kueleweka na hivyo basi huweka ujumbe wazi.

Kielelezo 7

| | |
|---|---|
| **Eneo bunge la Funyula limenakili asilimia 39 pekee ya watu waliojiandikisha kuwa wapiga katika shughuli ya kitaifa ya kusajili wapiga kura.** Hayo yamesemwa na mbunge wa eneo hilo, Dr Paul Otuoma ambaye amesikitika kuwa ni wapiga kura wapya-3,500 pekee waliosajiliwa katika eneo bunge hilo badala ya idadi iliyokuwa imelengwa ya wapiga kura wapya elf-9. Otuoma amewahimiza wale ambao hawajajisali kutumia fursa ya siku moja iliyosalia kujisajili. Otuoma ambaye ni waziri wa zamani wa michezo alisema wakenya sharti wafahamu kuwa kujiandikisha kupiga kura ni haki yao. Mbunge huyo alisema hayo mwishoni mwa wiki katika kijiji cha Kadibworo wakati wa mazishi ya Bi Loice Nyabaya. Waombolezaji pia walihutubiwa na gavana wa kaunti ya Busia Sospeter Ojaamong na aliyekuwa waziri msaidizi Prof Julia Ojiambo ambaye alitoa wito kwa wanawake kutochukulia elimu kuwa mzaha. | ***Koimongei kebebertab 39 eng bogol eng komostab kot ne king'aten ng'atutik nebo Funyula eng tetutiet netesetai nebo siretab biriikab kura.*** *Kamwa Dr. Otuoma kole kotomo betusiek 2 asikiwong tetutiet notok ko biik 3,500 chekokosirgei koek biriikab kura chelelach eng kot nekingate ngatutik nebo Funyala ganda kikitakchin kesir biik 9,000. Karirtae ine kaitet notok mitei ngony eng biik chekoimongei eng tetutiet notok ak kasom ichek komongei eng kasarta nitok kitikin nekokonget ek kosirgei.Otuoma neki minister nebo sports ko kamwachi biikab emoni kole tetutiet notok nebo kesirgei ko imandangwai. Kongalalchin biikab komasatak eng igorta nebo konoretab bortab Loice Nyabaya Governor nebo Busia Sospeter Ojaamong, ak ne ki assistant minister Prof. Julia Ojiambo.Kokon kurset Dr. Ojiambo koitchi kwonyik koib somanet koek kiit nebo kamanut.* |

8. Eneo bunge la Funyula limenakili asilimia 39 pekee ya watu waliojiandikisha kuwa wapiga kura katika shughuli ya kitaifa ya kusajili wapiga kura.

   *Koimongei kebebertab 39 eng bogol eng komostab kot ne king'aten ng'atutik nebo Funyula en tetutiet ne tesetai nebo siretab birikab kura.*

   (Sehemu ya 39 kwa mia katika eneo bunge la Funyula imejitokeza katika mpango unaoendelea wa kuwaandikisha wapiga kura.)

Kuwepo kwa dhana kama *limenakili, asilimia* na *kusajili* kunafanya tafsiri kukabiliwa na matatizo iwapo mtafsiri atang'ang'ania kutafutia visawe maneno hayo katika LL. Inabidi mtafsiri aelewe ujumbe unaowasilishwa katika muktadha wake ili apitishe ujumbe wenyewe kwa njia ambayo HL itaelewa kwa urahisi. Kutokana na ujuzi wake wa hali hiyo, mtafsiri amewasilisha maana ya: *sehemu ya 39 kwa mia imejitokeza katika eneo bunge la Funyula katika shughuli inayoendelea ya kuwaandikisha wapiga kura,* ambayo haitaleta utata wowote kwa HL. Mtafsiri amefutilia mbali dhana zinazotatiza na kutumia maneno ya kufidia maana za maneno yaliyofutwa. Maneno haya ya fidia yaliyotumiwa badala ya yale yaliyoibua changamoto za kutafsiri nayo yamewasilisha maana inayokaribiana zaidi na ile iliyobebwa na maneno asilia katika MC.

Hervy na Higgins (1992) wanaunga mkono kutolewa kwa idhini ya mtafsiri kudondosha na kuchopeka ujumbe katika ML ili kuboresha uelewekaji wa ujumbe. Mtafsiri aghalabu hulazimika kutoa maelezo zaidi ya neno moja au pengine sentensi fupi ili kutoa maelezo ya neno moja linalopatikana katika MC. Kwa kuzingatia aina hii, mtafsiri ana uhuru wa kuboresha matini kwa kuyafanyia marekebisho yanayoweza kufanikisha mawasiliano. Mtafsiri pia husahihisha makosa pale ambapo matini haijaandikwa vizuri. Japo mtafsiri

ana uhuru wa kufanya marekebisho, ni sharti awe makini asije akafanya mabadiliko mengi ambayo yanaweza kukengeusha matini inayotafsiriwa. Hii ni kwa sababu kadri ambavyo mabadiliko kwa lengo la kurekebisha yanaweza kufanywa, ujumbe wa kimatini unastahili kudumishwa. Ana jukumu la kuboresha mantiki na kuhakikisha kwamba matini inatiririka vilivyo. Mtafsiri huondoa mambo yote yanayoweza kuwa vikwazo katika uelewaji wa MC kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

Kielelezo 8

| | |
|---|---|
| **Watu 24 wamelazwa kwenye taasisi tatu za afya katika Kaunti ndogo ya Ugunja kufuatia mlipuko mpya wa ugonjwa wa kipindu-pindu huko Siaya katika muda wa wiki tatu. Kulingana na afisa mkuu wa matubabu katika hospitali ya wilaya ndogo Ambira, jumla ya wagonjwa 10 wamelazwa kwenye kituo cha afya cha Ligega.** Gavana wa Siaya alipotembelea sehemu iliyokumbwa na tatizo hilo **alipiga marufuku shughuli za uvuvi hadi wakati suluhu ya mgogoro unaokumba umiliki wa eneo hilo utakapotatuliwa.** | ***Tesetai konyoru kanyoiset bik 24 eng sipitalisiek 3 chemitei kaunti ne ming'in nebo Unguja kosubgei ak mongunetab miondo nebo kipindupindu eng kaunti nebo Siaya amabek kasarta nebo wikisiek 3. Kosubgei ak ofisaiyat nebo tililindo eng Ambira, kotesetai konyoru kanyoiset bik 10 eng sipitalit ab Ligega.*** *Ye kan korutechi meng'ikab kebeberta ne koityi kaimutyonitok gavana nebo kaunti nebo Siaya ko* **kaitonosi nameetab** ***njirenik agoi kasarta ne kinyoru wolutyetab tiiyet ne kiityi komosatak.*** |

9. Watu 24 wamelazwa kwenye taasisi tatu za afya katika kaunti ndogo ya Ugunja kufuatia **mlipuko** mpya wa ugonjwa wa kipindupindu huko Siaya katika muda wa wiki tatu.

   *Tesetai konyoru kanyoiset biik 24 eng sipitalishek 3 che mitey kaunti ne ming'in nebo Ugunja kosubgei ak* ***mong'unetab*** *miondo nebo kipindupindu eng kaunti nebo Siaya amabek kasarta nebo wikisiek 3.*

   (Watu 24 wanaendelea kupata matibabu katika hospitali tatu katika kaunti ndogo ya Ugunja kutokana na **kujitokeza** kwa ugonjwa wa kipindupindu katika kaunti ya Siaya kabla ya kukamilika kwa muda wa wiki tatu.)

Mtafsiri ametambua dosari inayopatikana katika MC ambapo dhana isiyofaa ya *mlipuko* imetumiwa na mwandishi wa matini yenyewe. Mtafsiri amerekebisha na kutafsiri kuleta maana ya *mkurupuko,* ambayo MC ililenga kuiwasilisha. Vilevile katika mfano huo, mtafsiri amefanya maana kuwa wazi kwa kutafsiri dhana *wamelazwa* kama *wanaendelea kupata matibabu* kwa sababu dhana hiyo ikitafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja inaweza kubeba maana kwamba watu waliotajwa wamefanywa kulala. Pia kifungu *taasisi tatu za afya* kimewasilisha maana kwa udhahiri kwa kutafsiriwa tu kama *hospitali tatu.* Hii inaonyesha kwamba mtafsiri ni sharti awe na stadi za uhariri ili atambue upungufu wa aina yoyote katika matini anayoshughulikia ili asihamishe dosari hizo katika ML.

Ingawa tafsiri mawasiliano ni kwa manufaa ya mpokezi, haipuuzi mtindo, muundo, sarufi, muktadha na vipengele vingine vinavyohusu matakwa ya lugha. Hutilia maanani nafasi inayochukuliwa na maswala ya muundo na sarufi ya LL. Uwiano katika mpangilio wa maneno, mtindo wa matini, mazingira, muktadha, utamaduni, mahitaji ya hadhira na wakati ni mambo ya kimsingi yasiyopuuzwa katika tafsiri mawasiliano. Tafsiri hii hujumuisha mambo yote yanayofanikisha mawasiliano. Pia hutegemea nadharia zote za tafsiri kwa kuwa lengo lake kuu ni mawasiliano. Tafsiri hii ina uwezo mkubwa wa kukabiliana na matatizo ya tafsiri kuliko aina zile nyinginezo za tafsiri na humwezesha msomaji kupata ujumbe, mawazo, itikadi na falsafa ya MC.

## 2.3 HITIMISHO

Katika sura hii tumebainisha kwamba kuna aina mbalimbali za tafsiri namna zilivyo aina za matini. Aina za matini hudhihirika kupitia sifa bainifu za matini husika. Kwa kutegemea sifa za matini, mtafsiri anatarajiwa kuteua mbinu mwafaka ya/za kutafsiria

matini yenyewe ili sifa zake halisi zidumishwe. Hii ina maana kwamba kunapaswa kuwe na mwingiliano wa chanda na pete kati ya aina za matini na aina za tafsiri zinazohusishwa ili zoezi la tafsiri lifikie malengo yanayokusudiwa na mtafsiri.

Kadri ya uwezo wetu tumeonyesha aina za tafsiri zinazotumika katika tafsiri za TH katika kituo cha Kitwek na namna zinavyoathiri viwango vya UM. Vilevile tumeangazia nguvu na upungufu wa kila mojawapo ya aina za tafsiri tulizoshughulikia. Kutokana na udadisi huo ni bayana kwamba japo aina hizo za tafsiri zinatofautiana kwa hali mbalimbali, kila moja huwa na umuhimu pamoja na dosari zake. Hata hivyo ni wazi kwamba aina moja ya matini huweza kushirikisha aina zaidi ya moja ya tafsiri au hata zote japo baadhi yazo zina uwezo wa kupotosha maana zaidi kuliko nyinginezo huku nyingine zikiwa na nguvu za kumwezesha mtafsiri kufikia tafsiri bora zaidi.

Utambuzi wetu katika uchanganuzi wa aina za tafsiri ni kwamba tafsiri mawasiliano na tafsiri maana zinachangiana kwa namna moja au nyingine kufikia tafsiri inayodumisha maana ipatikanayo katika MC za TH. Tafsiri ya moja kwa moja haichukui nafasi kubwa hasa ikieleweka kwamba lugha zinazohusika katika utafiti huu zinatofautiana kisarufi na kimuundo namna tutakavyodhihirisha katika sura inayofuata. Tafsiri ya moja kwa moja inapotumika, kiwango kikubwa cha kupotoshwa kwa maana hushuhudiwa. Kwa upande mwingine, tafsiri huru inaathiri thamani ya matini kutokana na uhuru mwingi unaomfanya mtafsiri kupenyeza mambo yasiyokuwepo katika MC kwenye ML na wakati mwingine kudondosha mambo muhimu yaliyopatikana katika MC.

# SURA YA TATU

# MATATIZO YANAYOKUMBA TAFSIRI ZA TAARIFA ZA HABARI KATIKA KITUO CHA KITWEK

## 3.0 UTANGULIZI

Mtafsiri wa matini ya aina yoyote anapojaribu kuhawilisha maana ya kimatini kutoka LC hadi LL, yeye hukumbana na matatizo chungu tele ambayo yanasababisha hali ya ukosefu wa UM. Matatizo yenyewe ni ya aina mbalimbali na kila tatizo huwa na chanzo chake mahsusi. Mtafsiri anapaswa kuwa na ujuzi wa kuyaainisha matatizo haya ili aweze kuyatafutia njia mwafaka za kuyatatua. Kuna matatizo yanayojikita katika uwezo wa mtafsiri mwenyewe kutomudu lugha moja au zote mbili katika tafsiri. Pia mtafsiri anaweza kuongozwa na mwelekeo wake kuhusu lugha fulani inayohusika, jambo linalosabababisha hatari ya kuathiri maana inayowasilishwa.

Katika sura hii, tuliyachunguza matatizo mbalimbali yanayodhihirika katika tafsiri za TH. Tuliyaainisha matatizo haya katika kategoria mbalimbali kulingana na vyanzo vya matatizo yenyewe pamoja na kuchanganua athari zinazoletwa na matatizo hayo katika uwasilishaji wa maana iliyomo katika MC. Tulifanya hivyo kupitia uchanganuzi linganishi wa TH katika LC na LL, huku tukidondoa mifano kwa kila mojawapo ya aina za matatizo.

### 3.1 Tofauti za Kiisimu kati ya Lugha Chanzi na Lugha Lengwa

Mutie (1997) anaeleza kwamba haiwezekani kupata lugha mbili ambazo zina muundo wa aina moja kiisimu kwa kuwa kila lugha ina upekee wake katika vipengele vya kiisimu. Kule kutoelewa miundo ya ndani ya lugha kwa upande wa mtafsiri kunaweza kupotosha tafsiri kwa kiwango kikubwa. Watafsiri wengi wanapokumbana na matatizo ya kiisimu, wao hujaribu kuyaepuka kwa kuzingatia aina ya tafsiri ya moja kwa moja kutafsiria matini zao. Matatizo yanayokumba tafsiri yanadhihirika katika viwango mbalimbali vya kiisimu. Katika sehemu hii tutangazia matatizo mbalimbali yanayofungamana na tofauti za kiisimu kati ya LC na LL. Tutaangazia matatizo yanayojitokeza katika viwango vya mofolojia, sintaksia na semantiki.

#### 3.1.1 Tofauti za Kimofolojia

Jambo la kimsingi analopaswa kuzingatia mtafsiri ni kuchunguza iwapo kuna ulinganifu wowote kati ya LC na LL kuhusiana na jinsi viambishi vinavyojitokeza. Katika tafsiri, mofu huangaliwa katika mkabala wa majukumu yake ya kiisimu au kisarufi. Mofu huwa na majukumu ya kuonyesha wakati, hali, idadi, ukanushaji n.k. Nyongeza ya viambishi awali au vifuatilizi ni uhalisi ambao mtafsiri anapaswa kutambua kwa sababu mofu huongeza, kupanua au kubadilisha maana ya neno.

Kwa kuwa maneno huundwa kutokana na visehemu vidogo vidogo ambavyo vina maana uelewa wa hali hii humsaidia mtafsiri kutafuta taratibu na mbinu mwafaka za kubainisha, kuainisha, kukadiria na kutathmini maana ya neno kuanzia vipashio vya chini kama mofu hadi vipashio vikuu kama sentensi.

Mofolojia ni mojawapo ya vipengele vya kiisimu ambavyo huleta tofauti kati ya Kiswahili na Kikipsigis. Kutokana na tofauti za kimofolojia baina ya lugha hizi mbili, mtafsiri hupata matatizo kwa kuwa ni vigumu kuleta upatano baina ya vipashio vya kimuundo vya maneno katika lugha zenyewe. Tofauti na lugha ya Kiswahili iliyo na mpangilio wa majina katika ngeli, lugha ya Kikipsigis haina sifa hiyo. Viambishi awali ambavyo huambatana na majina, vivumishi na vitenzi ni vipengele muhimu vinavyotofautisha lugha za kibantu na zile zisizo za kibantu. Upangaji wa majina katika ngeli husababisha kuwepo kwa upatanisho wa kisarufi. Kanuni za upatanisho wa kisarufi ndizo zinazoongoza ufasaha wa lugha yoyote. Kanuni zinazoongoza upatanisho wa kisarufi katika lugha ya Kikipsigs ni tofauti na zile zinazoongoza upatanisho wa kisarufi katika lugha ya Kiswahili. Mtafsiri anapaswa kuwa na ujuzi wa kanuni hizo katika lugha zote mbili zinazohusika.

Pia lugha ya Kiswahili ina njia ya kuonyesha hali ya udogo na ukubwa wa majina kwa kutumia viambishi, hali isiyokuwepo katika lugha ya Kikipsigis. Tafsiri zinazofanyiwa nomino zilizo katika hali ya ukubwa au udogo kutoka Kiswahili hadi Kikipsigis aghalabu hulazimishwa kuwa katika hali wastani. Njia nyingine ambayo mara nyingine hutumiwa na watafsiri kujaribu kudumisha ile hali ya ukubwa au udogo wa nomino ni kufungamanisha nomino zenyewe na vivumishi vya sifa vinavyobainisha hali hizo za ukubwa au udogo, japo wakati mwingine maana halisi iliyokusudiwa haiwasilishwi kikamilifu. Kuwepo kwa changamoto hiyo kunadhihirishwa na mfano ufuatao:

Kielelezo 9

| | |
|---|---|
| Hali ya hofu imetanda katika mji wa Nakuru kufuatia kuzuka kwa uhasama baina ya makundi mawili yanayoishi katika mji huo. Inadaiwa kuwa uhasama huo umesababishwa na matamshi ya kichochezi kutoka kwa viongozi wa kisiasa yaliyofanywa katika siku za hivi majuzi. Imeripotiwa kuwa **vijikaratasi vya uchochezi vilipatikana katika sehemu mbalimbali za mji huo** leo asubuhi ambavyo vinaonya watu wa jamii fulani kuhama. | *Mi barak orogenet en taonitab Nakuru kosubgei ak suriondit ne kobit en kwenutab bororiosiek aeng' che meng'chindos en taonit noton. Mwaat kele suriondiniton kobit ko kotienge ng'ololutikab kabeiset koyob kandoikab bolotet en betusikab konegit. Mwaat kele* ***kaginyor kartasisiek ab kabeyset en kebeberwek che terter chebo sironoton*** *en yegonetab ra che komoche biik ab bororiet agenge koistoge en taoninotok.* |

10. Vijikaratasi vya uchochezi vilipatikana katika sehemu mbalimbali za mji huo…

    *Kaginyor kartasisiek ab kabeyset en kebeberwek che terter chebo sironoton…*

    (Karatasi za uchochezi zilipatikana katika sehemu mbalimbali za mji huo)

Tafsiri hii haikutilia maanani hali ya udogo wa dhana *vijikaratasi* na badala yake kuchukua hali ya wastani ya dhana yenyewe: *karatasi.* Ili kuwasilisha maana inayokaribiana zaidi na ile ya MC, mtafsiri angetumia neno hilo katika hali ya wastani kama alivyofanya kisha akaambatisha nomino hiyo kivumishi kinachofafanua hali ya udogo kama ambavyo MC ilidhamiria kuwasilisha.

### 3.1.2 Tofauti za Kisintaksia

Kupatikana kwa maafikiano ya kimuundo baina ya lugha mbili tofauti ni suala gumu sana. Hivi ni kwa sababu kila lugha huwa na miundo yake ya sarufi inayotofautiana na ya lugha nyingine. Utata wa kimawasiliano hutokea pale ambapo miundo ya kisarufi ya LC italazimishwa kwa LL. Lugha ya Kikipsigis, kama ilivyo lugha ya Kiswahili, ina mpangilio wake wa kipekee wa maneno katika sentensi.

Hata hivyo, mpangilio wake wa kawaida wa maneno katika sentensi ni ule wa kitenzi, kiima na kisha kufuatwa na yambwa. Hali hii ni tofauti na ya Kiswahili ambapo kiima hutangulia kitenzi na kufuatwa na yambwa. Mfano ufuatao utaweka wazi sifa hizo:

Kielelezo 10

| | |
|---|---|
| Kiongozi wa walio wengi katika bunge la kitaifa Aden Duale, amewaambia wakazi wa kaskazini mashariki ya nchi kwamba hawana la kuhofia tena kuhusu kutengwa kwani eneo hilo sasa linadhibiti mabilioni ya pesa kupitia kwa serikali mbalimbali za kaunti. Duale alisema kuwa kwa mara ya kwanza tangu taifa hili kujinyakulia uhuru, kaunti za Garissa, Wajir na Mandera sasa zinaweza kutumia zaidi ya shilingi bilioni 20 katika kila kipindi cha matumizi ya pesa za serikali. Anasema kiasi hicho hakijumuishi hazina za wanawake na vijana. Akiongea huko Garissa wakati wa mkutano wa ushauri ulioandaliwa na wanafunzi wa chuo kikuu cha Kenyatta kutoka eneo hilo, **Duale aliwaambia vijana** kuwa wakati umewadia kwa wakazi wa eneo hilo kushindania nafasi za ajira zinazochipuza sawa na wakazi wa maeneo mengine ya nchi. Aliwahimiza wadau katika sekta ya elimu kujibiidisha ili kuhakikisha wanafunzi zaidi wanajiunga na shule bora za upili na vyuo vikuu huku akiongezea kuwa hazina ya ustawi wa eneo bunge hilo itaendelea kufadhili masomo ya wanafunzi kutoka familia maskini. Viongozi wengine waliokuwepo **wamesisitiza kujitolea kwa serikali kuboresha muundo-msingi katika maeneo hayo.** | *Kakomwochi meng'ikaab Kong'asis nebo Murot Katam kandoindetab membaek chechang eng koot ne king'ate ng'atutik Aden Duale kole matokoib ko biik che kikotaban eng serikali amu eng nguni ko koketobonchi billionishekab rabishek eng counties chotok. Kamwa Duale kole eng kenyisiek chechang tab konyor kandoynatet emoni kotomo lkonyoru rabishek che itey billion 20 counties chebo Garissa, Wajir ak Mandera eng kenyit agenge nebo nfinancial year asi kekanaptae boishonik chechang tabala chebo CDF, neranik ak chebo kwonyik. Kon'gololi eng sukulitab barak nebo garissa eng ng'ololutik che kochobe kibagengeitab kipsomaninik chebo north Eastern province kenyatta university koiyi kipsomaninik chebo sekondari eng taonitab Garissa,* ***kamwochi Duale neranik*** *kole nitok ko kasarta kotoy barnotik ak meng'ikaab komasatak konyorchigey boishonik che terter eng serikalitab boror,chebo counties ak kibagengeishek che mabo serikali. Kates komwa kole nyalu eng biik che chutyin somanet kokimiit boisionikwaak ak koro kole kachuut kipsomaninik chechang sekondari ak sugulisiek ab barak asi konyor somanet ne ititaat amu mitey rabishek chebo CDF che mokchingey taretet. Komiten inendet ak kandoik alak che* ***koikimit kole konunotkei serikali kosuldaen teksetab ortinwek, karetoetab beek ak sitimeet eng kebeberwechoton.*** |

11. Duale aliwaambia vijana…

(Kiima) (kitenzi) (yambwa)

*Kamwochi Duale neranik*

(Kitenzi) (kiima) (yambwa)

Tofauti hizi za miundo ya sentensi huzua changamoto katika uwasilishaji wa maana kwa kuwa mtafsiri asipotambua tofauti hizo na kujaribu kulazimisha kuwepo kwa maafikiano ya kimuundo kati ya MC na ML, miundo isiyokubalika katika LL huzuka. Katika hali hii, mtafsiri ni sharti aelewe kwanza maana unaowasilishwa katika MC, kisha akahawilisha kwa kuzingatia kanuni za kisintaksia za LL. Beecher (1988) anasema kwamba mtafsri anapaswa kudumisha au kutilia maanani miundo ya kisintaksia katika LL kwa kutolazimisha miundo ya LC kwa LL.

### 3.1.3 Tofauti za Kisemantiki

Uwasilishaji wa maana katika MC usipofanywa kwa ukamilifu, basi tafsiri haitakuwa na manufaa kwa HL. Kwa sababu hiyo kipengele cha maana, ambacho hushughulikiwa katika semantiki, hakiwezi kutenganishwa na tafsiri kwa kuwa hatua ya kwanza na ya muhimu katika tafsiri ni kwa mtafsiri kuelewa maana ya dhana au ujumbe unaopitishwa kabla ya kuhamisha katika ML. Larson (1984) anasema kwamba tafsiri ni mchakato wa kimawasiliano unaoanzia katika uchanganuzi wa muundo wa kisemantiki wa matini na kukamilika katika kupatikana kwa ML inayowasilisha ujumbe uliokusudiwa kupitishwa na MC. Uchanganuzi wa kisemantiki utadhihirisha kuwepo kwa utata katika mfano ufuatao:

Kielelezo 11

| | |
|---|---|
| **Rais Uhuru Kenyatta leo atakutana na rais Yoweri Museveni wa Uganda katika Ikulu ya Nairobi. Viongozi hao watashauriana kuhusu ujenzi wa bomba la mafuta baina ya Uganda na Kenya ambao ni mradi muhimu katika mpango wa ujenzi wa muundo msingi kwenye kanda hii.** Kampuni za uzalishaji mafuta nchini Uganda, ile ya Ireland ya Tullow Oil, ile ya ufaransa ya Total na ile ya CNOCn ya China pia zimealikwa kwenye mkutano huo. Mradi huo wa bomba la mafuta unanuiwa kusafirisha mafuta ambayo hayajasafishwa kutoka maeneo ya uchimbaji mafuta ya Hoima hadi bandari ya Lamu, kupitia maeneo ya uchimbaji mafuta humu nchini ya Lokichar. Kwenye taarifa iliyotolewa baada ya ziara ya kiserikali ya rais Kenyatta nchini Uganda mwezi Agosti mwaka uliopita, viongozi hao wawili walisema ujenzi wa bomba hilo unafaa kutekelezwa haraka ili kuzuia kucheleweshwa zaidi kwa biashara ya rasilmali za mafuta nchini Uganda zilizogunduliwa miaka tisa iliyopita. | ***Wendi kotuytos kandoindetab emoni Uhuru Kenyatta ak kandoinetab emetab Uganda Yoweri Museveni eng gotab pororiot Nairobi. Bendi kong'olole kandoichoton chobetab oret nebo mwanik nebune Kenya agoi Uganda ne noton ko tetutiet nebo kamanut nebo tekseet en kebeberiton.*** *Kakitaach kora kampunishekab mwanik kou chebo Irish company, Tullow oil, French company total ak nebo China koitita tuyonotok. Kikitoy project nitok bo pipeline koib mwanik kongete ole kinyorchin eng komastaab loima akoy port nebo Lamu ak chebo Lokichar. Kingobata ng'alalutik che kiay Kenyatta ak Museveni kenyit konye arawetab 10 eng emetab Uganda, koyonchin kandoik chotok tuway kochob ortinwek chotok eng chokchinet asi kenyorchi kelchin che kikinyoru kenyishek 9 che kikobata.* |

12. …viongozi hawa watashauriana kuhusu ujenzi wa **bomba** la mafuta baina ya Kenya na Uganda ambao ni mradi muhimu katika mpango wa ujenzi wa muundo msingi kwenye kanda hii.

    *…bendi kong'ololen kandoichoton chobetab* ***oret*** *nebo mwanik ne bune Kenya agoi Uganda ne noton ko tetutiet nebo kamanut nebo tekseet en kebeberiton.*

    (… viongozi hawa wanaenda kuzungumzia utengenezaji wa **njia** ya mafuta inayopitia Kenya hadi Uganda ambao ni mradi muhimu wa ujenzi katika sehemu hii.)

Kutokana na ugumu wa kupatikana kwa kisawe cha dhana *bomba,* imembidi mtafsiri awasilishe ujumbe wa MC kwa kuzingatia maana ya kimuktadha. Hata hivyo, matumizi ya neno *njia* kama tafsiri ya neno *bomba* huwasilisha maana inayosheheni utata kwa sababu HL itafasiri kwa namna tofauti. Hii inaokana na sababu kwamba dhana iliyotumika katika MC ina maana ya kileksika huku ile ya ML ikibeba maana husishi. Japo tafsiri hii imefanywa kama mkakati wa kukabiliana na ukosefu wa ulinganifu wa maana, mkakati wenyewe umechangia kupotoka kwa maana kutokana na tofauti kati ya lugha hizi mbili katika namna zinavyogawa mawanda ya maana.

Kila mara katika miktadha ya tafsiri, maneno yanayotumiwa hayatumiki katika upekee wao bali yanatumika yakiwa katika hali za ujirani na mahusiano ya aina mbalimbali na maneno mengine. Hali hizi za ujirani na mahusiano hufanya maneno kuibua maana mbalimbali, tofauti na maana za maneno yenyewe kama zinavyoelezwa katika kamusi. Kutokana na hali hii, neno katika matini linaweza kuwa na maana ya moja kwa moja, ya kimantiki, halisi, ya kipragmatiki, ya kidhamira, ya kiistiari, ya kijamii, kihisia, ya kiuamili na ya kimuktadha miongoni mwa nyinginezo. Mfano ufuatao unadhihirisha namna maana tofauti huibushwa kutokana na utangamano wa maneno, wakati maneno fulani hutangulia maneno fulani au wakati maneno fulani hufuatwa na maneno fulani.

Kielelezo 12

| | |
|---|---|
| Wanamgambo wa tawi la Afrika Kaskazini la mtandao wa al Qaeda wamewaua watu-16 wakiwemo wazungu wanne katika eneo la ufuoni la Grand Bassam nchini Ivory Coast. Wanamgambo sita waliwamiminia risasi watu waliokuwa katika ufuo huo ambao ni maarufu kwa watalii kutoka nchi za Ulaya, umbali wa kilomita-40 Mashariki mwa Abidjan. Haya yanajiri wakati ambapo wenyeji wengine **walikiri kuwa walilazimishwa kula kiapo kama njia ya kuwa wanachama wa kundi hilo haramu** miezi mine iliyopita. | *Kobar kiboriotinik chebo al Qaeda chemitei eng murot katam nebo Afrika biik 16 koboto biik 4 kobun emet nebo kiplalechek eng betutab jumapili eng makawet agenge eng emetab Ivory Coast. Kotakchin biik loo chekotindoi bundukisiek komwokto risasinik eng makawet nebo Grand Bassam, eng weekend nekosirtoi ole cham kobendi kiplelachek akomitie makawanatak eng loindab kilomitaisiek 40 cherongo eng nganasetab Abidjan. Katestai yautioni en kasarta ne kaimong'ke meng'ik alak che* ***kang'ong' kole kikimololchi ichek koyosio ne notok ko oret ne kichuten katuiyonotok ma iyanat*** *en arawek ang'wan che kikosirto.* |

13. … walikiri kwamba walilalizimishwa **kula kiapo** kama njia ya kuwa wanachama wa kundi hilo haramu

    *… kang'ong' kole kikimololchi ichek* ***koyosio*** *ne notok ko oret ne kichuten katuiyonotok ma iyanat.*

    (… walifichua kuwa walishurutishwa kuapa kama njia ya kujiunga na kundi hilo lisilokubalika)

Katika tafsiri ya hapo juu maana huwa wazi kutokana na namna ya utangamano wa maneno *kula* na *kiapo.* Kama neno *kula* lingefuatwa na neno jingine tofauti, maana pia ingebadilika. Hii inaonyesha kwamba utangamano wa maneno kutangulia au kufuata jingine aghalabu hujenga maana fulani dhahiri au maana mahsusi kiasi kwamba kule kubadilishwa kwa maneno katika utangamano kunabadilisha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC. Kuwa na ufahamu huu kunamwezesha mtafsiri kutilia maanani miungano na mahusiano mbalimbali ya maneno na kufahamu kwamba miungano na mahusiano hayo yanajenga maana mahsusi.

Katika kutafsiri TH, mara nyingi mtafsiri hukumbana na maneno ambayo si rahisi kutoa maana yake kikamilifu kutoka MC hadi ML. Kutolewa kwa maana kamili huwa jambo zito ndiposa mtafsiri anapaswa kuwa mwangalifu ili aweze kuchunguza maana na vijimaana vinavyopatikana katika vifungu mbalimbali bila kupuuza athari inayoweza kutokea pale ambapo dhana fulani inapofasiriwa visivyo na mtafsiri. Tafsiri potovu za dhana husababisha kupotoka kwa maana na hivyo jambo hilo linaweza kuepukika mtafsiri anapokuwa makini na mwangalifu anapochunguza maana zinazoweza kuibuka katika ML wakati vifungu mbalimbali vya TH vinapotafsiriwa.

### 3.2 Tofauti za Kitamaduni kati ya Lugha Chanzi na Lugha Lengwa

Nida (1964) anaeleza kwamba mtafsiri anapoendesha shughuli yake huwa anatangamanisha tamaduni za lugha mbili tofauti. Kwa sababu hiyo, tafsiri bora itafikiwa pale ambapo mtafsiri anaelewa tofauti na mapatano ya kitamaduni ambayo lugha mbili zinazohusika kwenye tafsiri zinasheheni. Utamaduni ni jinsi watu wanavyoishi na namna maisha yao yanavyojibainisha kipekee katika jamii mahsusi inayotumia lugha fulani katika mawasiliano. Utamaduni hufungamana na mazingira ambayo watu wa jamii fulani wanaishi. Mazingira hutazamwa kama malighafi ya lugha kwa kuwa jamii inachota msamiati kutokana na vitu ambavyo vinaizunguka jamii yenyewe.

Osano (1997) anafafanua dhana ya mazingira kama hali ya anga na ya kimaumbile inayoizunguka eneo fulani la kijiografia. Mazingira yenyewe huathiri maisha ya wanadamu kwa namna mbalimbali. Anatoa mifano ya mimea, wanyama na vitu vinginevyo ambavyo hupatikana katika maeneo mbalimbali kwa kutegemea mazingira ya mahali. Vitu vyenyewe vinapatikana katika mazingira maalum na ya kipekee. Kwa

sababu ya kuwepo kwa hali tofauti za kimazingira, watu hujitokeza na dhana mbambali za kutajia vitu vinavyopatikana katika mazingira yao, kama inavyodhihirika katika mfano huu:

Kielelezo 13

| | |
|---|---|
| **Cameroon imewahukumu kunyongwa wanamgambo 89 wa kundi la kigaidi la Nigeria la Boko Haram.** Wanamgambo hao walipatikana na hatia ya kutekeleza ukatili na mahakama ya kijeshi ya Cameroon kutokana na kuhusika kwao katika mashmbulizi kadhaa ya kigaidi **katika kisiwa kilichoko kaskazini mwa nchi hiyo kwenye mpaka na Nigeria.** Cameroon ilipitisha sheria za kukabiliana na ugaidi mnamo mwaka wa 2014 ambao adhabu yake ni kifo. Waathiriwa hao 89 ni kati ya wanamgambo 850 waliotiwa nguvuni nchini humo na kuhusishwa na kundi la Boko Haram. Kufuatia kubuniwa kwa sheria hizo, shirika moja la kutetea haki za binadamu limetaka sheria za Cameroon kufanyiwa marekebisho. Mamia ya watu wameuliwa kwenye visa tofauti vya mashambulizi ya kigaidi nchini Cameroon tangu ilipochangia kikosi cha jeshi la kanda hiyo la kukabiliana na ugaidi mwaka jana. Katika siku za hivi majuzi wanamgambo wengi wameripotiwa kujiingiza **kwenye kisa cha ulipuaji wa kujitoa mhanga.** | ***Kaigochi emetab Cameroon kerkongiet nebo meet membaek 89 chebo kunditab kiboriotinik nebo Boko Haram kobun emetab Nigeria.*** *Kokirwokchi kiboriotinichoto eng kapkirwok nebo asikarikab luget eng lelutik chebo kasuldaetab boisionik chebo chelesosnatet ak kabokchinosiek che terter* ***en ikwembeiyot nemi komosta nebo murot katam nebo emetab Cameroon ole tetegei ak kiwato nebo emetab Nigeria.*** *Kiisirto emetab Cameroon ngatutik cheesio yautikab chelesosnatet eng kenyitab 2014 ne kiti kole kigochini kerkongietab meet agetugul nekakinyor kosuldae yautichoto. Bichoto 89 chekokinam koboto alak 850 chekikakinam eng Cameroon ak kirwokchi eng lelutik kele tinyegei tiliandit ak Boko Haram. Kosubgei ak kerkongiet noto bo meet ko koimongei kibagengeisiek cheborchingei imandap kipkosobei kobun emonoto ak kokon kurset nebo keyachi walutik kapkirwok nebo emetab Cameroon. Kikobet sobonwekwak bogolusiekab bik eng kabokchinosiek chekikebaorianchi eng emetab Cameroon kongete ngap kochut asikarichi chebo luget poriet nekitokchini kiboriotinik chebo Boko Haram eng kenyit nekosirtoi. Mwaat kele en kasarta ne kosirtoi ko kokebaorionchi kiboriotinik che begu* ***en yautietab katyolsietab kistoege sobeet.*** |

14. … katika **kisiwa** kilichoko kaskazini mwa nchi hiyo kwenye mpaka na Nigeria.

    *… en* ***ikwembeiyot*** *nemi komosta nemi murot katam nebo emetab Cameroon ole tetegei ak kiwato nebo emetab Nigeria.*

    (kwenye **mahali katikati ya maji** kaskazini mwa nchi ya Cameroon karibu na mpaka wa nchi ya Nigeria)

Hadhira ya ML itapata ugumu kuelewa maana ya dhana *kisiwa* hata baada ya mtafsiri kung'ang'ania kuitafutia kisawe. Hii ni kwa sababu dhana hiyo inarejelea mazingira ambapo HL ya Wakipsigis hawana mazoea nayo. Katika muktadha huu, HL itapata tu kuelewa tukio lililotokea lakini mazingira ya kutokea kwake si bayana kutokana na kutotangamana nayo. Dhana iliyotumika imeundwa ili kukabiliana na ukosefu wa dhana linganifu lakini dhana hiyo haijazoeleka kimatumizi kutokana na ugeni wa maumbile ya mazingira yanayorejelewa.

Katika zoezi la tafsiri, mtafsiri aghalabu hukumbana na majina ya vyombo vya kitamaduni au vitu vipatikanavyo katika jamii ambayo ambayo MC iliandikwa na ikawa kwamba vyombo vyenyewe havipatikani katika jamii ya ML. Mara nyingi mtafsiri anapokumbana na msamiati kama huo, yeye hulazimika kutafsiri kwa kutumia msamiati wa vitu vinavyokaribiana japo havihusiani kama inavyodhihirishwa na mfano huu:

Kielelezo 14

| | |
|---|---|
| Serikali ya Malaysia imesema watu 15 walioshukiwa kupanga njama ya kufanya mashambulizi nchini humo wamekamatwa. Washukiwa hao wanahusishwa na wanamgambo wa kundi la Islamic State. Washukiwa hao akiwemo afisa mmoja wa polisi walikamatwa kwenye mji mkuu Kuala Lumpur, na katika majimbo mengine sita. **Maafisa wa polisi wamesema watu hao walishukiwa baada ya kujaribu kununua kemikali za kutengeneza mabomu.** | *Kamwa afisaekab police eng emetab Malaysia kole kakonam biik 15 chekibwotchin kotete kabokchinosiek eng emonotok. Kates kole bichotok koimuchi koboisie eng kibagenge ak kiboriotinikab Islamic State. Agenge eng bichotok ko afisayatab police ako kokinam icheket eng nganasetab Kuala Lumpur.* ***Kang'ong' polis kole kochenge bichotok tuguk che kichoben bomisiek.*** |

15. Maafisa wa polisi wamesema watu hawa walishukiwa baada ya kujaribu kununua **kemikali** za kutengeneza mabomu.

    *Kagong'ong' polis kole kacheng'e bichotok* ***tuguk*** *che kichoben bomisiek.*

    (Polisi walifichua kuwa watu hawa walikuwa wakisaka **vitu** vya kutengeneza mabomu)

Tafsiri ya dhana *kemikali* imejitokeza kama *vitu.* Dhana hizo hazina uhusiano wa moja kwa moja lakini kule kuongezwa kwa maneno ya ufafanuzi: *vya kutengenezea mabomu,* ambayo yamejitokeza baada ya dhana hiyo kumesababisha kuwepo kwa maana inayokaribiana na ile ya MC.

Suala la utamaduni husababisha tatizo kuu la ukosefu wa dhana linganifu. Mtafsiri anaweza kukumbana na dhana katika LC isiyo na dhana linganifu katika LL kwa njia mbalimbali kama vile:

MC kuwa inaeleza au kurejelea dhana ambayo inaeleweka katika LL lakini ikatokea kwamba dhana yenyewe katika LL haina neno faafu au lililo na maana linganifu. Mfano ufuatao unadhihirisha ugumu wa kupatikana kwa visawe vya baadhi ya dhana zipatikanazo katika MC:

Kielelezo 15

| | |
|---|---|
| **Rais Uhuru Kenyatta amehimiza kuimarishwa kwa biashara na uwekezaji** kati ya Kenya na Ghana. Rais alisema ingawa biashara kati ya nchi hizo mbili imeimarika, bado kuna mengi ya kufanya kufanikisha hata zaidi ushirikiano huo. Rais Kenyatta aliyasema hayo katika uwanja wa Black Star mjini Accra alipoungana na rais John Dramani Mahama na watu wa Ghana kuadhimisha mwaka wa 59 wa uhuru wa nchi hiyo ya Afrika Magharibi, sherehe ambayo pia ilihudhuriwa na rais wa Guinea Bissau Jose Mario Vaz. Rais huyo wa Ghana alikuwa miongoni mwa wageni waliohudhuria maadhimisho ya 51 ya jamhuri mwaka 2014 katika uwanja wa taifa wa Nyayo, kwa mwaliko wa rais Kenyatta. Rais Kenyatta alikariri kujitolea kwake kushirikiana sio tu na rais Mahama, bali pia viongozi wengine wa Afrika katika maswala ya biashara na uwekezaji. Rais Mahama kwa upande wake alimshukuru rais Kenyatta kwa kuitikia mwaliko wa kuungana na watu wa Ghana kuadhimisha siku hiyo muhimu katika historia ya taifa hilo. | ***Kakosom kandoindetab emoni Uhuru Kenyatta ketes kekanapta mung'aret*** *eng kwenetab emoni ak emetab Ghana ne agenge eng tetutik che kikonoptoy tilyandit eng kwenetab emotinwek che mitey Africa. Kang'ong kole eng nguni komitey mung'aret ne tesetay eng oret ne kararn eng kwenetab emotinwek chuto tuway ngandaan tokomitey boroindo kekimiit mising. Kang'oli Uhuru eng betutab raini ole kotaach president John Dramani nebo emetab Ghana eng igorta ne kiboybochin kenyitaab 59 kong'ete konyor katyaknatet emonotok, ne kamitey kora president nebo Guinea Bissau Jose Mario Vaz ne kakiyae kiwanjetab Black star square ne mitey Accra. Kabiit nitok ye kingorutechi emoni president Mahama eng kenyitaab 2014 ye kisuldoe emoni igortaab Jamhuri nebo kenyitaab 51 ne kikiyae kiwanjetab Nyayo. Kaikimiit Uhuru kole nyalu kokimiit emoni ak emetab Ghana tokchinet nebo keyai mung'aret ne makiyochegey ne naat ko Continental Free Trade ne tie kibagengeitab ECOWAS ak nebo EAC. Kakon kayamiset Uhuru kole wendi koboishe ak president Mahama ak kandoik alak chebo Africa.Kaiwekchi kongoi Preident Mahama president Kenyatta ne koiyan koitita igoratok.* |

16. Rais Uhuru Kenyatta amehimiza kuimarishwa kwa biashara na **uwekezaji**…

*Kakosom kandoindetab emoni Uhuru Kenyatta ketes kekanapta mung'aret*…

(Kiongozi wa nchi hii Uhuru Kenyatta ameomba kuzidi kuimarishwa kwa biashara…)

Dhana ya *uwekezaji* inaeleweka katika LL kwamba inahusu mchakato fulani wa kibiashara wa kutumia raslimali chache ili kuzalisha faida lakini hakuna neno faafu linaloweza kutumika kama kisawe cha dhana yenyewe ndiposa mtafsiri amefungia nje dhana hiyo kwa kusema *amehimiza kuimarishwa kwa biashara* na kupuuza tafsiri ya dhana *uwekezaji.*

Tofauti kati ya LC na LL katika namna zinavyogawa maana ya uhalisi wa jinsi moja mahususi. Katika hali hii neno linaloibusha changamoto za ulinganifu wa maana linaweza kuwa linarejelea kitu ambacho kinatambulika katika lugha zote mbili zinazohusika lakini ikatokea hali ambapo uhalisi wa kitu chenyewe unaeleweka kwa njia ambazo zinatofautiana. Mfano huu utaweka wazi suala hilo:

Kielelezo 16

| | |
|---|---|
| **Jaji wa mahakama kuu Nicholas Ombija atasailiwa tena baada ya mahakama ya juu kukubalia ombi la bodi ya kuwasaili mahakimu na majaji la kufanya hivyo.** Bodi hiyo iliwasilisha rufaa ya kupinga uamuzi wa mahakama ya rufani mwezi Disemba mwaka jana wa kusimamisha kusailiwa upya kwa jaji Ombija. Majaji wa mahakama ya juu Dr. Willy Mutunga, Kalpana Rawal, Mohammed Ibrahim, Jackton Ojwang, Smokin Wanjala na Njoki Ndung'u waliruhusu bodi hiyo kuwasilisha rufaa hiyo na kuagiza kwamba shughuli ya kumsaili kwa mara nyingine jaji huyo ianze mara moja. Aidha, majaji hao waliagiza shughuli hiyo ifanywe kila siku hadi itakapokamilika tarehe 31 mwezi huu. | ***Tetat keyochi kokeny chigilisiet kirwokindetab kapkirwok nebo barak Nicholas Ombija ye kankotil kesit kapkirwok neo ole katii bodi nebo kirwogik che ech en kapkirwok.*** *Eng kenyitab 2015 kokikaesio kapkirwok nebo somet maget nekimachei board notok koyachi kokeny chigiliset kirwokindonotok. Tilanotok kakikon eng betutab raini kokakonunu kirwokikab kapkirwok nebo supreme dr Willy Mutunga, Kalpana Rawal, Mohammed Ibrahim, Jacktone Ojwang ak Njoki Ndungu. Kates kole tetat konaam chigilisionotok akoi tun kikes eng tarik 31 nebo arawani.* |

17. **Jaji** wa mahakama kuu Nicholas Ombija atasailiwa tena baada ya mahakama ya juu kukubali ombi la bodi ya kuwasaili mahakimu na majaji la kufanya hivyo.

*Tetat keyochi kogeny chigilisiet* ***kirwogindet*** *ab kapkirwok nebo barak Nicholas Ombija ye kan kotil kesit kapkirwok neo ole katii bodi nebo kirwogik che ech en kapkirwok.*

(**Hakimu/jaji/chifu** wa mahakama ya juu Nicholas Ombija amepangiwa kufanyiwa tena uchunguzi baada ya mahakama ya juu kufanya uamuzi uliounga mkono bodi ya mahakimu wakuu)

Dhana ya *jaji* inatafsiriwa katika LL kwa neno linalobeba maana mbalimbali. Neno lenyewe lina maana ya chifu, jaji au yeyote anaweza kutoa hukumu. Kueleweka kwa maana ya dhana hiyo kunakuwa kwa kiwango cha juu pale ambapo dhana hiyo inatoholewa kuliko inapotafutiwa kisawe chake katika LL.

Hali ya LL kuwa na neno lililo na maana halisi lakini ikawa kwamba halina neno la kijumla. Hali hii huzuka hasa kutokana na kuwepo kwa vikoa vya maana katika lugha. Dan (2010) anaeleza vikoa vya maana kama kikundi cha maneno yanayohusiana kimaana. Ni jozi za maneno zilizo na uhusiano wa kisemantiki. Katika kikoa fulani mahsusi kuna maana ndogo ndogo ambazo huwakilisha maana halisi huku kikoa chenyewe kikiwasilisha maana ya kijumla. Changamoto zinaoibushwa na sifa hii ya lugha ni kwamba kuna baadhi ya vikoa vyenye uhusiano wa karibu kiasi cha kuweza kumchanganya mtafsiri katika kutofautisha dhana zinazohusika. Pia kuna baadhi ya vikoa ambavyo ni changamano na zinaweza kuwasilisha dhana zaidi ya moja. Vilevile kuna

vikoa vya maana vinavyotofautiana kulingana na eneo na utamaduni na hii ina maana kwamba utamaduni fulani unaweza kuwa na vikoa vinavyotumika ambavyo vinatofautiana na vya utamaduni mwingine kutegemea idadi ya vitu vinavyorejelewa katika jamii fulani. Tutaangazia suala hilo kupitia mfano huu ambao umenukuliwa kutoka kielelezo 10:

18. …wamesisitiza kujitolea kwa serikali kuboresha **muundo-msingi** katika maeneo hayo…

    …*koikimit kole konunotkei serikali kosuldaen* ***teksetab ortinwek, karetoetab beek ak sitimeet*** *eng kebeberwechoton…*

    (… amesisitiza kuwa serikali imejitolea kufanikisha **ujenzi wa barabara, usambazaji wa maji na stima** katika maeneo hayo)

Dhana *muundo-msingi* ina maana ya kijumla ya huduma mbalimbali zinazoboresha maisha ya wananchi na huduma zenyewe zinapotajwa moja moja maana halisi hujitokeza. Changamoto iliyomkumba mtafsiri ni ile ya kupata neno lenye maana ya kijumla ndiposa akaishia kuorodhesha huduma zenyewe moja baada ya nyingine.

Hali ya LL kuwa na neno lililo na maana ya kijumla lakini ikawa kwamba halina neno halisi. Ukosefu wa maana halisi katika lugha yoyote ile hauchukuliwi kama udhaifu wa lugha bali ni hali inayotokana na uhalisi wa kimazingira na uhalisi wa kihistoria wa lugha inayohusika. Tutarejelea mfano ufuatao ili kubainisha hali hii ya kukosekana kwa dhana linganifu katika ML yenye maana halisi:

Kielelezo 17

| | |
|---|---|
| Wanachama wa bunge la kaunti ya Embu wamehimiza kuchunguzwa mitindo ya maisha ya maafisa wa utumishi wa umma katika kaunti hiyo ambao wameanza kufanya kampeni za kuwania viti mbalimbali vya kisiasa kabla ya uchaguzi mkuu mwaka ujao. Wakiongozwa na mwakilishi wa wodi ya Runyenjes ya kati, Steve Simba, waakilishi hao wa wodi walidai mishahara ambayo watumishi wa umma hupata haiwezi kufadhili kampeni zao za kisiasa na huenda wanajihusisha na ufisadi. **Walisema maafisa hao wamekuwa wakihudhuria mazishi, harusi na kupanga mikutano ya kisiasa** huku wakipuuza utekelezaji majukumu yao ya utumishi kwa umma. Simba alisema atawasilisha hoja katika bunge la kaunti ya Embu ili kuwafuta kazi maafisa kama hao kwa kushiriki kwenye siasa wakiwa bado wanahudumu kama watumishi wa umma. | *Kakokon kurset membaekab kobun kaunti nebo Embu kole kechigil atebosiek ak malik chebo ofisaek chebo poror cheboisie eng county chekokotoi koyai campaign chebo ngecherok che terter chebo bolatet amait keyai lewenisiet neo eng kenyit nenyonei. Kondochini MCA nebo Runyenjes kwen, Steve Simba, komwa MCAs kole mlekwek chetachei kiboitinichoto bo serikali komagoi koyamiche koyaei campaigns chebo ngalekab bolatet ak komuch kotesetai chorsetab rabinikab poror.* ***Komwa kole ofisaechoto kobendi igorwek chebo konoretab borwek, igorwek chebo katunisiet ak kotetei tuiyosiekab bolatet*** *ne katayachini boisiet bikab emet. Komwa Simba kole wendi eng konekit koibe motion kowo county assembly asi keisto eng boisiet ofisaechoto amu yoei ngalekab bolatet eng kasarta nemi eng ofisisiekwak.* |

19. Walisema maafisa hawa wamekuwa wakihudhuria **mazishi, harusi** na kupanga mikutano ya kisiasa…

    *Komwa kole ofisaechoton kobendi* ***igorwek chebo konoretab borwek, igorwek chebo katunisiet*** *ak kotetei tuiyosiekab bolatet…*

    (Walisema kuwa maafisa hawa huhudhuria **sherehe za kuzika miili, sherehe za ndoa** na kupanga mikutano ya kisiasa.)

Katika kielelezo kilichotolewa, mtafsiri ametumia ufafanuzi kutolea maelezo tafsiri za dhana *mazishi* na *harusi* kwa sababu ni maneno yenye maana halisi katika LC lakini LL haina maneno yenye maana halisi ya kueleza dhana hizo. Ili zoezi la tafsiri lifanikiwe, mtafsiri ametumia neno lenye maana ya kijumla, *sherehe,* kisha akafafanua aina ya sherehe inayorejelewa.

Hali ya LC na LL kuwa na maneno ambayo yanawiana kimaana lakini yanatofautiana kimatumizi kwa sababu ya hisia ambazo zinaibushwa na maneno hayo. Maneno hayo yanaweza kuwa yametumika kwa njia ya tasfida kuzungumzia masuala yanayofungamana na dini, jinsia, siasa n.k. Kwa upande mwingine, maana ambazo zinatokana na tofauti za maumbo ya maneno aghalabu hukosa ulinganifu wa maana kati ya LC na LL pale ambapo maana inayohusika imetokana na maumbo ya maneno katika LC. Hali hii ni tokeo la taratibu zinazotumika kuongeza au kupanua maana. Mara nyingi taratibu zinazotumika katika LC ni tofauti na zile zitumikazo katika LL, kama inavyowekwa wazi na mfano huu:

Kielelezo 18

| | |
|---|---|
| Mjukuu wa aliyekuwa waziri Njenga Karume, ametiwa nguvuni kwa madai ya kumsababishia kifo rafikiye wa kike, baada ya kumsukuma kutoka orofa ya nne ya jumba wanamoishi katika eneo la Ndumberi, Kaunti ya Kiambu. Habari zinasema kwamba msichana huyo wa umri wa takribani miaka 20 akifariki papo hapo. Akidhibitisha kisa hicho, Naibu afisa mkuu wa polisi katika Kaunti ya Kiambu Johnstone Lyambila alisema tayari wameanzisha uchunguzi juu ya swala hilo. Lyambila alisema mshukiwa atasalia kwenye korokoro ya polisi hadi uchunguzi kukamilika. Kwingineko katika kaunti hiyo mwanamume mmoja **amepatikana na hatia ya kumbaka na kumjeruhi msichana wa umri mdogo katika sehemu zake za siri.** | ***Kakinam mochokoretab neki minista Njenga Karume eng mwaet kele koyokta chamanet nenyi kongeten koropetab 4 eng apartment nengwai nemite Ndumberi eng county nebo kiambu. Chebotok kibwotchin kobo kenyisiekab 20 ak kiy, kokoibet sobet nenyi eng yotok. Koyoni imanitab logoywek chotok, komwa rubeywotab OCPD nebo Kiambu Johnstone Lyambila kole kakotoi afisaekab police chigilisiet kosubkei ak nyasutionotok. Kates kole ngetu werotok eng korkoret akoi kokesgei chigilisiet. Eng kebeberta age nebo kaunti notok ko kakinam muren ne kakinyorchi leluut ne mwaat kele kiyochi tuguk che manyalunot chepto ne ming'in ak kogochi kagotenosiek che echen.*** |

20. …amepatikana na hatia ya **kumbaka** na kumjeruhi msichana huyo katika **sehemu zake za siri.**

    *…kakinyorchi leluut ne mwaat kele* ***kiyochi tuguk che manyalunot*** *chebotok ak kogochi kagotenosiek che echen.*

(… amepatikana na kosa la **kumtendea mambo yasiyokubalika** msichana huyo na kumpa majeraha makubwa.)

Ili kuepuka kukorofisha mbeko za jamii ya LL, mtafsiri amepuuza kisawe cha dhana *kumbaka*, japo kisawe chenyewe kipo, na kuamua kutumia maelezo yanayopunguza ukali wa hisia ambazo zingeibushwa na tafsiri yenyewe. Hivyo basi, tafsiri ya dhana *kumbaka* imetolewa kama *kumtendea mambo yasiyokubalika*. Kwa upande mwingine, mtafsiri ameepuka kutolea tafsiri *sehemu zake za siri* na badala yake akaifuta dhana hiyo na kujumlisha hali ya kujeruhiwa pasipo kutaja sehemu ya mwili iliyopokea majeraha.

Kuwepo kwa matumizi ya maneno ya mkopo au ya kigeni katika MC kunaweza kusababisha kupotea kwa maneno hayo katika ML. Hata hivyo, japo maneno hayo ya mkopo hupotea katika ML, maana ya maneno yenyewe haipotei. Matumizi ya maneno ya kigeni katika MC huenda yanatokana na mapendeleo ya mwandishi binafsi au kuna uwezekano kwamba maneno hayo yalitumika kutoa msisitizo na pia huenda yametokana na matarajio ya sajili husika bila kupuuza sababu za kutaka kupamba MC. Dondoo lifuatalo katika MC linabeba neno la mkopo ambalo itambidi mtafsiri alifutilie mbali katika ML.

Kielelezo 19

| | |
|---|---|
| Wakristu kote ulimwenguni jana waliadhimisha Jumapili ya Mitende ambayo ndiyo jumapili ya mwisho kabla ya sikukuu ya Pasaka. Siku hii huadhimishwa kama kumbukumbu ya kuingia kwa Yesu Kristu mjini Yerusalem akiwa amebebwa na mwana punda huku makundi ya watu wakimshangilia na kuweka matawi ya mitende kwenye njia aliyopitia. **Ni desturi ya makanisa mbalimbali kuandamana wakibeba matawi ya mitende sikukuu hii inayoadhimishwa kila mwaka.** Aliwahimiza viongozi kuiga maisha ya Yesu Kristo ya kiongozi mtumishi. **Akiongea na maelfu ya mahujaji katika eneo la St. Peter's Square** wakati wa misa ya Jumapili ya mitende, baba mtakatifu Francis, alisema njia ya kuelekea kwa wokovu inazingatia unyenyekevu na utumishi kwa wengine. Aliwahimiza mahujaji kutafakari yaliyomsibu Yesu Kristo hadi kifo chake wakati wa wiki hii takatifu. **Aliyasema hayo baada ya kuwapokeza waumini sakramenti ya Pentenensia katika kanisa hilo.** | *Koibwaat eng betutab amut kristianik tugul betutab ne letchin nebo Jumapili ne naat kou jumapili nebo sosik kotomo koit betut ne kibwote akobo pasaka. Betut nitok kebwoti Jumapili nekiwo Jeiso Kristo Jerusalem ole kibunoti sigiriet ak kindee sageekab palm oret tugul ne kibunoti.* ***Eng betuniton kiboiboenchin eng kenyit age tugul ko piitet eng kristianik kobendat eng oret ak sosik.*** *Betutab raini ne naat ko jumapilitab sosik ko taunet nebo wikiit ne tilil ole ibe kasartanywa kristianik ak kobwaat betushek che kiletchin komitey ng'oyduni Jeiso kotomo kikartat eng kimurtoiyot. Kora ko betut ne letchin eng karugutetabgey ole nyalu kosaa, korugutgey kristianik yotok kosuldoe boishonikab toretoshek. Boybochin kanisoshek tugul chebo kristianik betut nitok.* ***Kangong'ololchin elfuisiek ab biik eng kanisetab St. Peter's Square*** *komwochi kobwaat nyalildab Jesu Kristu eng wikinitok tilil.* ***Kamwoe ngalechuton kan kobata sakramenti nebo ng'ong'unetab leluutik en kanisanatak.*** |

21. Aliyasema hayo baada ya kuwapokeza waumini sakramenti ya **Pentenensia** katika kanisa hilo…

    *Komwoe ng'alechuton kan kobata sakramenti nebo* ***ng'ong'unetab leluutik*** *en kanisanatak…*

    (Aliyasema maneno haya baada ya kukamilika kwa sakramenti ya **kuungama dhambi** katika kanisa hilo.)

Mtafsiri anapokumbana na dhana halisi ya kitamaduni. Mara nyingi inabainika kwamba neno fulani katika MC linaweza kuwa linarejelea dhana ambayo haifahamiki katika LL au dhana yenyewe ikawa haielezeki katika LL kwa njia ya kutumia neno moja bali maelezo yanahitajika ili maana idhihirike. Neno linalorejelewa hapa huenda likawa

linahusiana na dhana inayohusu imani fulani au kitu fulani kilicho dhahiri katika dini fulani. Vilevile dhana inaweza kuwa inarejelea taratibu za kijamii, mchakato wa maandalizi ya chakula cha aina fulani, desturi fulani ya kijamii, miiko, maadili na michakato mingineyo ya kitamaduni. Mfano huu unadhihirisha ugumu wa kutafsiri dhana inayohusu desturi fulani katika jamii mahsusi:

Kielelezo 20

| | |
|---|---|
| **Watu 24 wamelazwa kwenye taasisi tatu za afya katika Kaunti ndogo ya Ugunja kufuatia mlipuko mpya wa ugonjwa wa kipindu-pindu huko Siaya katika muda wa wiki tatu. Kulingana na afisa mkuu wa matubabu katika hospitali ya wilaya ndogo Ambira, jumla ya wagonjwa 10 wamelazwa kwenye kituo cha afya cha Ligega.** Gavana wa Siaya alipotembelea sehemu iliyokumbwa na tatizo hilo **alipiga marufuku shughuli za uvuvi hadi wakati suluhu ya mgogoro unaokumba umiliki wa eneo hilo utakapotatuliwa.** | ***Tesetai konyoru kanyoiset bik 24 eng sipitalisiek 3 chemitei kaunti ne ming'in nebo Unguja kosubgei ak mongunetab miondo nebo kipindupindu eng kaunti nebo Siaya amabek kasarta nebo wikisiek 3. Kosubgei ak ofisaiyat nebo tililindo eng Ambira, kotesetai konyoru kanyoiset bik 10 eng sipitalit ab Ligega.*** *Ye kan korutechi meng'ikab kebeberta ne koityi kaimutyonitok gavana nebo kaunti nebo Siaya ko* ***kaitonosi nameetab njirenik agoi kasarta ne kinyoru wolutyetab tiiyet ne kiityi komosatak.*** |

22. …alipiga marufuku shughuli za **uvuvi** hadi wakati mgogoro unaokumba umiliki wa eneo hilo utakapotatuliwa.

    *…kaitonosi* ***nameetab njirenik*** *agoi kasarta ne kinyoru wolutietab tiyeet ne kiityi komosatak.*

    (… alisitisha **kushikwa kwa samaki** hadi wakati suluhu ya mgogoro uliokumba sehemu hiyo itakapopatikana.)

Uvuvi ni mojawapo ya shughuli za kijamii ambazo hazijazoeleka katika mazingira na utamaduni wa jamii ya LL na hivyo ni vigumu kupata neno moja linaloweza kusimama kama kisawe cha dhana hiyo. Imemjuzu mtafsiri kutumia maelezo ili kuwasilisha maana kwa udhahiri.

Neno katika MC kuwa na muundo tata kisemantiki. Japo si suala la lazima, maneno ya aina hii pia yanaweza kudhihirisha utata wa kimofolojia. Maneno mengine huwa na mofimu changamano na vilevile kuwa na maana changamano. Kifungu kilichokolezwa katika mfano ufuatao, kilichonukuliwa kutoka kielelezo 13, kina muundo tata kisemantiki:

23. … kwenye kisa cha **ulipuaji wa kujitoa mhanga…**

*…en yautietab **katyolsietab kistoege sobeet…***

(… kwenye kitendo cha **ulipuaji wa kujiondolea uhai**)

Inakuwa vigumu kubaini iwapo mlipuaji ndiye anayelenga kuondoa uhai wake au anashirki kitendo cha kulipua ili kudhuru au kuondoa uhai wa wengine. Tafsiri inayotolewa ina utata mwingi kwa sababu mlipuaji na anayelengwa na ulipuaji si dhahiri. Zaidi ya utata unaoletwa na muundo wa maneno, pia kuna uchangamano unaoibushwa na matumizi ya nahau *kujitoa mhanga.*

### 3.3.0 Udondoshaji wa Vipengele vya Matini Chanzi katika Matini Lengwa

Mtafsiri mara nyingi huchukua hatua ya kufutilia mbali baadhi ya vipengele vipatikanavyo katika MC kwa kusudi la kustawisha maana ya ujumbe unaowasilishwa katika ML. Jambo hili huenda akafanya kimakusudi au kimakosa pasipo kujua athari inayoweza kuibushwa na hatua hiyo katika uwasilishaji wa ujumbe wa kimatini. Mfano ufuatao unabainisha kiwango cha athari iletwayo na udondoshaji wa maneno fulani au vifungu fulani vya maneno:

Kielelezo 21

| | |
|---|---|
| Vituo vya kupigia kura kwenye uchaguzi wa ubunge huko Malindi na ule wa useneta huko Kericho vitafunguliwa kesho mwendo wa saa kumi na mbili asubuhi na kufungwa saa kumi na moja jioni. **Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka, IEBC** hata hivyo imesema wapiga kura watakaokuwa kwenye foleni kufikia saa kumi na moja jioni wataruhusiwa kupiga kura. Tume hiyo ya uchaguzi imemteua Moses Ledama Sunkuli kuwa afisa msimamizi wa uchaguzi wa useneta huko Kericho, ilhali Stephen Kitsao Karani amejukumiwa kusimamia uchaguzi wa ubunge wa Malindi. Kulingana na IEBC matokeo ya uchaguzi yanatarajiwa kutangazwa wakati wowote baada ya saa tatu usiku hapo kesho. Wakiongea na wanahabari huko Kericho, makamishna wa tume hiyo wakiongozwa na afisa mkuu wa tume hiyo Ezra Chiloba, walisema maandalizi ya chaguzi hizo mbili ndogo yamekamilika. **Alitaja madai ya kuwahonga wapiga kura, ununuzi wa vitambulisho na kadi za kupiga kura kuwa baadhi ya changamoto zinazoikumba tume hiyo, lakini akaongeza tume hiyo inashirikiana na vitengo vingine husika kuchunguza madai hayo kwa lengo la kuwachukulia hatua wahusika.** Naibu mwenyekiti wa tume hiyo Mahiri-Zaja aliwaongoza makamishna wengine kuwahakikishia wanaowania viti hivyo viwili kwamba uchaguzi huo utaandaliwa kwa njia huru na ya haki. Kiti cha seneta wa Kericho kimevutia wagombea sita akiwemo Aaron Cheruiyot wa chama cha Jubilee na Paul Sang wa Kanu. Huko Malindi kivumbi kitakuwa kati ya Phillip Charo wa jubilee na Willy Mtengo wa ODM. Kampeni zilikamilika rasmi jana jioni. | *Kibendi keyote ketesiosiekab biretab kura eng county nebo Kericho ak koot ne king'ote ng'atutik nebo Malindi sait taman ak aeng nebo karon ak keker sait taman ak agenge nebo koskoleng' eng betutab mutay. Kakomwa **Kibegengeit ne Telelchinge nebo Lewenishet ak Kiwatosiek, IEBC** kole biriikab kura che tokomitey lainda kokakobeek sait keyonchin kobir kura. Wendi koeku returning officer Moses Ledama Sunkuli eng county nebo Kericho ak Stephen Kitsao Karani koek ne telelchin lewenishet eng Malindi. Kimong'u komong' walutik eng sait somok nebo kemboy eng betutaab mutay. Kan kong'olole Chiloba ak siriikab logoywek ko **kamwa kole kaimutik che konyor ko kou ng'olset ak aletab kurainik ak kibandok ak kaimutik alak.** Kamwochi rubeywotab nepo ng'echeret eng IEBC Mahiri Zaja che bendi kobeligey eng lewenishetab mutay kole wendi kosuldoe tetutio notok eng oret ne taku ak nebo imanit. Koimongey biik 6 cheibelchingey ng'echeretab senate eng county nebo kericho che boto Aaron cheruiyot nebo JAP ak Paul Sang nebo KANU. Eng komastaab Malindi kobendi kobeligey Philiph Charo nebo JAP ak Willy Mtengo nebo ODM che kokomongey eng kabeletabgey ne mitey barak. Kobeek tetutitab sometab kurainik eng betutaab amut.* |

24. Alitaja madai ya kuwahonga wapiga kura, ununuzi wa vitambulisho na kadi za kupiga kura kuwa baadhi ya changamoto zinazoikumba tume hiyo, **lakini akaongeza tume hiyo inashirikiana na vitengo vingine husika kuchunguza madai hayo kwa lengo la kuwachukulia hatua wahusika.**

*Kamwa kole kaimutik che konyor ko kou ng'olset ak aletab kurainik ak kibandok ak kaimutik alak.*

(Alisema kwamba matatizo waliyopata ni udanganyifu na ununuzi wa kura na vitambulisho miongoni mwa matatizo mengine.)

Sehemu yote iliyokelezwa katika MC hapo juu imefutwa licha ya kuwa sehemu yenyewe inabeba habari za muhimu zinazostahili kufikia HL. Kando na hayo, ufutaji huu umechangia kuvurugika kwa ujumbe wa ML. Mtafsiri amejipa uhuru mwingi wa kudondosha maelezo hayo na ni wazi kwamba ile athari itakayoibushwa kwa hadhira ya ML haitalingana na ile iliyokusudiwa na mwandishi ifikie kwenye hadhira ya MC.

Ni vyema kwa mtafsiri kuelewa kwamba kudondoshwa kwa baadhi ya vipengele vya MC huweza kusababisha dosari za kimaana na kimawasiliano katika ujumbe unaotarajiwa kufikishwa kwa HL. Udondoshaji huweza kufanya HL kufasiri ujumbe kwa njia isiyofaa kwa sababu vipengele vinavyofutiliwa mbali aghalabu vina dhima ya kutajirisha maana au kudumisha thamani ya ujumbe uliopo katika MC. Ni wazi kwamba hata neno fulani moja litolewapo katika matini, uwezekano wa kuathirika kwa maana huwa mkubwa kama inavyobainishwa na mfano ufuatao ulionukuliwa kutoka kielelezo 20:

25. Kulingana na afisa **mkuu** wa matibabu katika hospitali ya wilaya ndogo ya Ambira, jumla ya watu 10 wamelazwa kwenye kituo cha afya cha Ligega.

*Kosubgei ak afisayat nebo tililindo eng Ambira, ko tese tai konyoru kanyoiset biik 10 en ketesietab kanyoiset nebo Ligega.*

(Kulingana na afisa wa afya huko Ambira, watu 10 wanaendelea kupata matibabu katika kituo cha matibabu cha Ligega.)

Katika tafsiri ya hapo juu, dhana *mkuu* imedondoshwa. Ufutaji wa sifa hiyo ya afisa wa afya umeathiri uwasilishaji wa maana kwa sababu tafsiri inayopatikana inapotosha hadhi ya afisa anayezungumziwa kwa sababu amerejelewa kama afisa yeyote mwingine ingawa

kulikuwa na uwezekano wa mtafsiri kupata tafsiri mwafaka ya sifa hiyo kwa kutumia mojawapo ya mikakati inayokubalika ya tafsiri.

### 3.4 Upenyezaji wa Vipengele Vipya katika Matini Lengwa

Tafsiri za aina fulani hutoa ufafanuzi wa habari zaidi ya inavyohitajika ili ujumbe uwasilishwe kikamilifu. Mtafsiri hupata mshawasha wa kuingiza vipengele vipya visivyopatikana katika MC kwenye ML kwa dhamira ya kutaka kuimarisha mawasiliano. Jambo lingine linalomchochea kufanya hivyo ni hali ya kutaka kuyaweka wazi mambo fulani ambayo kwake yeye anayaona kwamba yanazua utata na hivyo akadhamiria kuyafumbua kwa kuchopeka vipengele vipya vinavyorahisisha uelewaji wa ujumbe unaowasilishwa.

Hata hivyo, wakati mwingine hatua hii huwa tatizo pale ambapo maana ingebakia katika ile asilia pasipo nyongeza ya vipengele vipya. Kitendo hicho mara nyingi huleta matatizo yanayoathiri maana na mawasiliano katika ujumbe unaopitishwa na ML kwa HL. Katika hali nyinginezo, dhana inayoongezwa na mtafsiri katika ML huenda haitekelezi dhima ya kiufafanuzi na kwa hivyo haipaswi kuingizwa katika tafsiri. Levinson (1984) anaeleza kwamba katika mawasiliano, mtu hastahili kutoa maelezo ya mambo zaidi ya yale yanayohitajika. Tutatathmini athari ya uchopekaji wa maneno mapya kwenye maana iliyopaniwa kupitishwa na mwandishi wa MC kupitia mfano ufuatao ulionukuliwa kutoka kielelezo 1:

26. Shughuli ya upigaji kura inaendelea katika kaunti ya Kericho…

*Tese tai* ***en inguni en oret ne kararan*** *lewenisiet en county nebo Kericho…*

(Uchaguzi unaendelea sasa **kwa njia iliyo nzuri** katika kaunnti ya Kericho)

Sehemu iliyokolezwa katika matini imepenyezwa licha ya kuwa haipatikani katika MC. Sehemu hiyo ikiondolewa, maana ile ipatikanayo katika MC itadumishwa na kutakuwepo na kiwango cha juu cha ulinganifu wa maana. Kando na maneno hayo yaliyoongezwa kuwasilisha maana isiyokusudiwa, pia kuna ukengeushaji wa umbo la matini. Habari inayowasilishwa katika sehemu hiyo ni kwamba shughuli ya upigaji kura inaendelea *kwa njia iliyo nzuri*. Hii inadhihirisha kwamba nyongeza iliyofanywa na mtafsiri imeathiri vibaya uwasilishaji wa habari.

Uzidishaji unaweza kuleta mabadiliko kwenye umbo la matini na kuchangia kuondolewa kwa sifa halisi za MC. Hali hii inaweza kufikia kiwango cha ML kutochukuliwa tena kama tafsiri na badala yake kuonekana kama ufafanuzi wa MC. Sifa hii ya kuongeza vipengele fulani pamoja na ile ya kudondosha ni baadhi ya sifa bainifu za tafsri huru.

### 3.5 Uchangamano katika Tafsiri za Misemo na Nahau

Katika matumizi ya lugha yoyote ile, kuna mpangilio fulani wa maneno ambao hauonyeshi kufungika katika maana za kikamusi za maneno yanayohusika. Mara nyingi utangamano wa maneno katika mpangilio huo hauonyeshi hali ya kutawaliwa na sheria za kiisimu. Mpangilio wenyewe unatokana na mazoea ya maneno yanayounganika na kujenga mahusiano fulani ambayo ni ya kinasibu. Miungano hii ya maneno inatofautiana

kutoka lugha moja hadi nyingine. Hivyo basi, miungano inayotokea katika lugha moja huwa nadra kujitokeza kwa hali hizo katika lugha ya pili.

Katika hali mbalimbali, mwandishi wa MC hubaini kwamba misemo au nahau fulani inaweza kupitisha ujumbe wake kwa namna ambao utaeleweka bayana kuliko pale ambapo kauli za kawaida zinatumika. Mtafsiri anapokumbana na matini inayosheheni misemo na nahau, huwa anakabiliwa na changamoto za kutafsiri vipengele hivyo. Mtafsiri anaweza kukumbana na msemo ambao haupatikani katika LL na hivyo kufanya zoezi la tafsiri kukosa kisawe cha msemo huo katika LL, kama inavyodhihirika hapa:

Kielelezo 22

| | |
|---|---|
| **Mwanasheria mkuu Githu Muigai anaitaka mahakama kuu kutupilia mbali rufaa ya mwanaharakati Okiya Omtatah** ya kupinga ustahilifu wa Sharad Rao kuwa mwenyekiti wa jopo la kuchunguza madai ya ufisadi dhidi ya jaji wa mahakama ya juu Philip Tunoi. Muigai alisema Rais Uhuru Kenytta alikuwa akitekeleza majukumu yake kuambatana na sheria wakati alipomteua Rao kuwa mwenyekiti wa jopo hilo. Muigai alimwambia jaji Joseph Oguto kwamba utakuwa ukiukaji katiba kuingilia kati uamuzi huo wa Rais. Inadaiwa kuwa Tunoi alipokea hongo ya shilingi milioni 200 kutoka kwa gavana wa Nairobi Evans Kidero ili kushawishi uamuzi wa kesi iliyowasilishwa na mbunge wa sasa wa Kabete Ferdinand Waititu kupinga kuchaguliwa kwake. | ***Mochei ogilyot ne nomu ng'atutik Prof Githu Muigai kapkirwok nebo barak koesio kesit ne kiib Okiya Omtatah*** *komache kapkirwok notok koesio tribunal nekichob president Uhuru Kenyatta asi komuch kochigil kirwokindetab kapkirwok nebo supreme Philip Tunoi. Kamwa Muigai kole tinye kimnatet president Kenyatta kolewen Sharad Rao kondochi tribunal notok. Kamwachi Muigai kirwokindetab kapkirwok nebo Barak Joseph Oguto kolenchi wendi koegu birutiet neo ngot kochutchi kapkirwok kakwautietab president Kenyatta. Kikimwaitae Tunoi kele kinyorchigei rabinik silingisiek million 200 kobun governor Evans Kidero asi kotil kesitab lewenisietab governor eng kaunti nebo Nairobi ne kikiyai eng kenyitab 2013.* |

27. Mwanasheria mkuu Prof Githu Muigai anaitaka mahakama kuu **kutupilia mbali**...

*Mochei ogilyot ne nomu ng'atutik Githu Muigai kapkirwok nebo barak* ***koesio****...*

(Wakili mkuu Githu Muigai anaitaka mahakama kuu **kukataa…**)

Badala ya kutafsiri nahau iliyotumika katika MC, mtafsiri ameishia kutumia neno linalowasilisha maana inayokaribiana na ile inayowasilishwa na nahau hiyo kwa kuzingatia muktadha ambamo nahau yenyewe imetumika. Changamoto hii inaonyesha umuhimu wa mtafsiri kuwa na ujuzi katika nyanja mbalimbali zinazohusiana na tafsiri hasa fasihi. Ikiwa mtafsiri hatokuwa na utaalamu wa kutosha katika uwanja wa fasihi, yeye atashindwa kufasiri kwa ufasaha misemo inayotumika katika matini inayotafsiriwa.

## 3.6 HITIMISHO

Sura hii imeshughulikia matatizo mbalimbali ambayo mtafsiri hukumbana nayo katika tafsiri. Tumebaini kwamba kuna matatizo yanayotokana na tofauti za kiisimu baina LC na LL, tofauti za kitamaduni baina ya jamii zinazotumia lugha zinazohusika katika tafsiri, matatizo yanayojikita katika ujuzi wa mtafsiri na mengine ambayo mtafsiri hana uwezo wa kuepukana nayo. Matatizo ya aina yoyote yana athari ya kupotosha maana na kusababisha ukosefu wa ulinganifu wa TH za MC na za ML. Vilevile imedhihirika kwamba matatizo ya aina mbalimbali yanasababishwa na vyanzo tofauti tofauti. Hivyo basi, ni sharti mtafsiri awe na ufahamu wa chanzo cha kila tatizo ili ateue mikakati ya kukabilana na kila aina ya tatizo analokumbana nalo anapoendeleza zoezi la tafsiri.

# SURA YA NNE

# MIKAKATI YA KUKABILIANA NA UKOSEFU WA ULINGANIFU WA MAANA KATIKA TAFSIRI ZA TAARIFA ZA HABARI

## 4.0 UTANGULIZI

Matatizo yanayokumba tafsiri za TH yana athari ya kupotosha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC. Hali hii huibusha ukosefu wa ulinganifu wa TH za LC na LL. Hata katika hali ambapo mtafsiri ni mtaalamu katika shughuli za tafsiri, ukosefu wa UM ni jambo lisiloepukika. Hata hivyo, ni sharti maneno yanayoonekana kuwa yanaweza kuzua utata yabainishwe kisha yachunguzwe yanavyoweza kushughulikiwa. Mtafsiri anaweza kukabiliana na hali hii kwa kutumia mikakati mbalimbali.

## 4.1 NJIA ZA KUKABILIANA NA UKOSEFU WA ULINGANIFU WA MAANA

Mikakati inayotumiwa na mtafsiri kukabiliana na ukosefu wa UM hudhibitiwa na uelewa kwamba uteuzi wa dhana mwafaka au dhana iliyo na maana linganifu hutokana na utambuzi wa muktadha wa matumizi ya dhana hiyo na kufanya tathmini ya namna ilivyotumika. Pia yafaa ieleweke kwa mtafsiri kuwa kuteuliwa kwa dhana mwafaka kunapaswa kuongozwa na utambuzi kwamba muktadha ambamo MC ilizalika unaweza kuwa tofauti na muktadha ML itakapopokelewa. Katika hali hiyo pia, ni vyema ieleweke kwa mtafsiri kwamba hadhira ya MC ni tofauti na ile ya ML.

### 4.1.1 Urejeleaji wa Makamusi

Makamusi yana manufaa mengi kwa mtafsiri pale anapokabiliwa na changamoto ya kutafsiri dhana mbalimbali. Kamusi hutoa kisawe cha dhana na maelezo kuhusu dhana yenyewe. Makamusi ya aina mbalimbali yanaweza kutumika kwa pamoja na mtafsiri kwa sababu yeye hukumbana na dhana kutoka nyanja mbalimbali ambazo zinafaa kutafutiwa kisawe mwafaka. Ili matumizi ya zana hii yamfae mtafsiri, yeye anafaa kutambua dhana anayoshughulia ni ya uwanja au taaluma ipi kisha arejelee kamusi ya taaluma ambayo dhana hiyo inapatikana. Mfano ufuatao, ulionukuliwa kutoka kielelezo 19, unaangazia dosari ambazo zingeepukika iwapo marejeleo ya kamusi yangefanywa:

28. …ni **desturi** ya makanisa mbalimbali kuandamana wakibeba matawi ya **mitende** sikukuu hii inayoadhimishwa kila mwaka.

    *…eng betuniton kiboiboenchin eng kenyit age tugul ko **piitet** eng kristianik kobendat eng oret ak **sosik.***

Tafsiri ya dhana *desturi,* ilivyoendelezwa kama *piitet* inaweza kufasiriwa visivyo kuleta maana ya kitendo cha kunyunyiza maji au kitu chochote kiowevu kwa kitu kingine. Aidha, tafsiri ya neno *mitende* kama *sosik* inawasilisha maana ya watu wenye kudharau. Kulingana na kamusi ya Seronei (2011), tafsiri za maneno haya, *desturi* na *mitende,* zinapaswa kuendelezwa kama *piiteet* na *soosik* mtawalia. Mifano iliyotolewa inadhihirisha umuhimu wa makamusi katika orodha ya zana za kukabiliana na changamoto za tafsiri.

Kuna makamusi ya aina mbalimbali katika lugha ya Kikalenjin ambayo yatamsaidia mtafsiri kutekeleza mambo mbalimbali yaliyokwisha kutajwa hapo juu. Kuna kamusi ya uwililugha ya Kibnyaanko Seroney (2009), iliyo na vidahizo katika Kikalenjin na maelezo kutolewa katika lugha hiyo, na kisawe chake katika Kiingereza kutolewa. Umuhimu mkubwa wa aina hii ya kamusi ni kule kutoa visawe katika Kikalenjin ambavyo vinampa mtafsiri uwezo wa kufanya uteuzi wa kisawe kilicho mwafaka zaidi kulingana na muktadha wa MC. Kamusi ya Ng'elechei C (1972) na ile ya Toweett Taitta (1979) ni miongoni mwa zana zinazomwezeha mtafsiri kukabiliana na changamoto za tafsiri.

### 4.1.2 Matumizi ya Dhana yenye Maana Elezi

Mkakati huu unatilia maanani uwasilishaji wa maana katika MC kwa njia ya kutumia neno ambalo linaweza kuleta maana kwa namna ya kutoa maelezo badala ya mtafsiri kung'ang'ania kupata maana halisi. Maana inayoibushwa hapa ni ile inayofungamanisha dhana inayotumika kwenye tafsiri na muktadha ambamo neno hilo limetumika katika MC. Katika mfano ufuataо, kutoka kielelezo 11, mtafsiri amekabili changamoto ya kutafsiri dhana zilizokolezwa kupitia matumizi ya dhana zenye maana halisi:

29. ... **Rais** Uhuru Kenyatta atakutana leo na **Rais** Yoweri Museveni wa Uganda katika **Ikulu** ya Nairobi.

    *...wendi kotuytos **kandoindetab emoni** Uhuru Kenyatta ak **kandoindetab emetab** Uganda Yoweri Museveni eng **gotab pororiot** Nairobi.*

    (**…Kiongozi wa nchi hii** Uhuru Kenyatta anaenda kukutana na **kiongozi wa nchi ya** Uganda Yoweri Museveni katika **jumba la kitaifa,** Nairobi.)

Dhana ya *rais* imetafsiriwa ili kuleta maana ya *kiongozi wa nchi* huku dhana *ikulu* ikitafsiriwa kama *jumba la kitaifa.* Dhana hizi zenye maana elezi zimetumika kwa kuzingatia miktadha ambamo zimetumika. Dhana hizi ni mwafaka kwa kuwa urais ni wadhifa wa juu zaidi wa uongozi katika nchi au taifa. Aidha, tafsiri ya *ikulu* kama *jumba la kitaifa* ni faafu kwa sababu huhusisha wadhifa ule wa urais kama kiongozi wa taifa na jumba anamokaa rais kwamba ni ya hadhi ya kitaifa kama wadhifa wenyewe. Kutokana na kutumika kwingi kwa maelezo kuliko dhana moja mahususi katika mkakati huu, ni wazi kwamba njia hii inatilia maanani zaidi muktadha wa kile kinachozungumziwa katika MC ili kiwasilishwe katika ML kwa njia itakayodumisha muktadha huo bila kujikita katika visawe vya dhana.

### 4.1.3 Matumizi ya Dhana yenye Maana ya Kijumla

Mara nyingi mtafsiri anapokumbana na neno lenye maana halisi au lenye urejeshi halisi huenda ikawa vigumu kuhamisha maana ya aina hiyo hadi ML kutokana na sifa ya LL kukosa maana halisi ya neno lenyewe. Hali kama hii itokeapo, mtafsiri anapaswa kutafutia dhana inayotatiza kisawe chenye maana ya kijumla kama ilivyofanywa katika mfano ufuatao uliotolewa kutoka kielelezo 22:

30. …anaitaka mahakama kuu kutupilia mbali **rufaa** ya mwanaharakati Okiya Omtatah...

*…moche kapkirwok nebo barak koesio* ***kesit*** *ne kiib Okiya Omtatah…*

(… anaitaka mahakama kuu kukataa **kesi** iliyowasilishwa na Okiya Omtatah…)

Katika mfano wa hapo juu, mtafsiri ameshindwa kupata kisawe cha dhana *rufaa* katika LL na akaishia kutumia neno lenye maana ya kijumla. Tafsiri iliyofanywa imechukua dhana yenye maana ya *kesi* ambayo ni neno linalojumlisha aina zote za kesi ikiwemo ile ya rufaa. Maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC bado itawasilishwa katika LC kwa njia inayoeleweka, japo si kikamilifu, lakini hali ya kuhusishwa kwa kesi yenyewe na kiwango cha mahakama iliyotajwa-mahakama kuu-itawasilisha habari inayokaribiana zaidi na ile iliyokusudiwa katika MC.

### 4.1.4 Matumizi ya Neno Fidia katika Lugha Lengwa

Neno linalozua ukosefu wa ulinganifu wa maana katika LC aghalabu hurejelea dhana halisi, kitu halisi au taratibu halisi za utamaduni wa LC. Ikiwa matumizi ya neno hilo katika LL yatazua utata katika kueleweka kwake au yatapingana na adabu ya LL, basi neno hilo linaweza kuachwa nje ili kutoa nafasi ya kutumika kwa maneno katika LL ambayo yatatambulika, kueleweka au kuleta ujumi kwa kuvutia kimatumizi. Tutaonyesha namna mkakati huu ulivyotumika katika mfano ufuatao:

Kielelezo 23

| | |
|---|---|
| **Spika wa bunge la taifa, Justin Muturi, amehimiza kuundwa upya Tume ya Maadili na Kupambana na Ufisadi** ili kusaidia kukabiliana na visa vya uhalifu ambavyo vimeathiri uchumi wa nchi hii. Spika Muturi alisema kuipa tume ya EACC muundo mpya ni muhimu ili kuiwezesha kushughulikia visa vikubwa vya uhalifu wa kiuchumi ambavyo vimeathiri uchumi wa nchi hii. Muturi ambaye alisema hayo leo kwenye mkutano wa kuchanga pesa katika kanisa la PCEA huko Karatina, Nyeri, alisema tume ya kupambana na ufisadi yapasa kuzingatia kuwafichua washukiwa wa shughuli haramu ambazo zinawanyima wananchi huduma muhimu. Alizihimiza taasisi zilizokabidhiwa majukumu ya kuchunguza na kushtakiwa kwa kesi za ufisadi ikiwemo ofisi ya mkurugenzi wa mashtaka ya umma na idara ya mahakama kujizatiti zaidi katika kushughulikia kesi kama hizo. | ***Kakon kurseet spika nebo kot neking'aten ng'atutik Justin Muturi kibakengeit ne leel ne borien asoya*** *en emoni notok nepo Ethics and Anti-Corruption Commission asi komuch koborien kaimutik cheimuch kongemei bandap tai en emoni. Kates komwa muturi kole nitok kowendi kokochin kimnotet kibakengeinotok asi koborien nametap asoya en oret nenyolunot ole kikebaorionchi kabetetat chepkondok en emoni che takikeyaen boisionik cheechen ak kokanapta bandap tai en emet komugul. Kongololei muturi en kayumanik che kakiyai en Karatina PCEA nemiten Nyeri ole kasom kibakengeinotok komong kainutikap kandoik che isuldoen nametap asoya en emoni ole kaip boroinotok kosom ofisit nepo Director of Public Prosecution kotoi chikilisiet kotiny kei ak kesisiek chepo nametap asoya.* |

31. Spika wa bunge Justin Muturi amehimiza kuundwa upya kwa Tume ya Maadili na Kupambana na **Ufisadi**...

*Kakon kurseet spika nebo kot ne king'aten ng'atutik Justin Muturi ketoo kibagengeit ne leel ne borien **asoya**…*

(Spika wa bunge Justin Muturi ametoa wito kubuniwa kwa tume mpya ya kupambana na **hongo…)**

Ugumu wa kutafsiri dhana *ufisadi* umemlazimu mtafsiri kutumia neno fidia lenye maana ya *hongo.* Hata hivyo, ufisadi ni dhana inayohusu mambo mengi kama matumizi mabaya ya mamlaka, mapendeleo katika utoaji wa nafasi au raslimali, wizi wa mali ya umma, utoaji na uchukuaji wa hongo miongoni mwa mengineyo. Kutumiwa kwa dhana ya hongo na mtafsiri, japo ni finyu, kunafidia dhana ya ufisadi kuliko pale ambapo dhana yenyewe inafutwa katika tafsiri kwa sababu hii ni njia iliyozoeleka au kufikirika kwamba ufisadi hutendeka zaidi kuliko njia nyinginezo zinazojulikana au kudhaniwa.

### 4.1.5 Matumizi ya Neno la Mkopo

Mkakati huu huhakikisha kwamba neno linalozua ukosefu wa ulinganifu wa maana linatafsiriwa kwa kutumia neno la mkopo ambalo linatoholewa kisha kutolewa maana. Njia hii ni mwafaka hasa katika tafsiri ya maneno yanayoibua dhana zenye maana halisi katika utamaduni wa LC. Dhana zinazoshughulikiwa kwa kutumia mkakati huu huenda zikawa za kidini, kiuchumi, kisiasa, kidhahania au za taratibu za kijamii kwa jumla. Katika matumizi ya mkakati huu, inatarajiwa kwamba neno ambalo linatoholewa linapojitokeza kwa mara ya kwanza katika MC, linapaswa kutoholewa na kutolewa maelezo mafupi. Neno hilo linapojitokeza kwa mara ya pili katika matini yenyewe basi

litatumika kama lilivyotoholewa katika hali ya kwanza. Tutarejelea mfano huu ili kudhihirisha ufaafu wa mkakati huo:

Kielelezo 24

| | |
|---|---|
| **Waziri wa utalii, Najib Balala, amesema serikali itawaondolea ushuru wawekezaji wanaonuia kuwekeza katika sekta ya kuwahudumia wageni** katika kaunti. Akiongea alipofungua rasmi hifadhi ya taifa ya wanyama pori ya Rimoi katika kaunti ya Elgeyo-Marakwet, Balala alisema huku kaunti zikiwa na maeneo mengi ya utalii, majumba ya malazi kwa wageni yangali changamoto. Alizihimiza kaunti kutenga ardhi kwa wawekezaji ili kuwawezesha kutekeleza ustawi wa muundo msingi. Balala ambaye aliandamana na waziri wa hazina ya taifa Henry Rotich na gavana wa Lamu, Issa Timamy, alisema wizara yake kupitia hazina ya kustawisha sekta ya utalii itatoa shilingi milioni 8 kwa kaunti hiyo kufanya utafiti wa kuzindua uchukuzi wa vigari vinavyotumia kebo kwa watalii kutoka nyanda za juu hadi hifadhi za wanyama pori. | ***Kakomwa minista nebo kiprutoinik Najib Balala kole wendi serikali koistoi rabinik chebo aisurut chelibani chemung'arainik chemochei koyai mungaret eng sekta nebo kiprutoinik*** *eng komoswek chebo counties. Kongalali eng kasarta nekoyatei kaptiongin nebo Rimoi eng county nebo EMC, komwa Balala kole kole agot eng kasarta netinyei counties chechang tuguk cheboiboichini kiprutoinik kobun emotinwekab sang, ko kikoek kanagutiet neo mising rarunetab korik chekiruitos. Kokon kurset koityi counties kogochi chemungarainik mbarenik asi komuktechi iche kotoi tetutikab bandaptai chemogotin eng sekta nebo kiprutoinik. Komitei Balala koboto minista nebo lekutab poror, Henry Rotich, gov nebo Lamu, Issa Timamy ak komwa kole wendi minstry nenyi kobun rabinik chekikitabanchi sekta nebo kiprutoinik kotioktoi siling milion 8 koityi county nebo EMC asi komuch koboisie eng chigilisiet ak chobetab karisiek chenootin kou Cable Cars cheimuti kiprutoinik kongete komoswek chemi barak agoi kaptiongin nebo Rimoi* |

32. Waziri wa Utalii Najib Balala amesema serikali itawaondolea **ushuru** wawekezaji wanaonuia kuwekeza katika **sekta** ya kuwahudumia wageni …

*Kakomwa minister nebo kiprutoinik Najib Balala kole wendi serikali koistoi* ***rabinik chebo aisurut*** *che libani chemung'arainik che mochei koyai mung'aret en* ***sekta*** *nebo kiprutoinik…*

(Waziri wa Utalii Najib Balala amesema serikali inaenda kuondoa **pesa za ushuru** zinazolipwa na wawekezaji wanaonuia kufanya biashara katika **sekta** ya utalii…)

Mtafsiri amechukua dhana *ushuru* kisha akatohoa kama *aisurut* halafu akatolea maelezo mafupi kubainisha kwamba kinachotajwa katika LC ni aina za malipo au fedha ambazo hutozwa watu wanaoendesha shughuli za kibiashara au wanaojipatia mapato kwa njia

mbalimbali zinazokubalika. Aidha, utohozi wa neno *sekta* umeambatishwa maelezo yanayodhihirisha kwamba dhana hiyo inarejelea kitengo, uwanja, sehemu au idara inayoshughulikia suala fulani mahususi katika upana wake. Hii ni hatua ambayo mtafsiri amechukua ili kukabiliana na changamoto iliyoibushwa na ugumu wa kupata visawe vya dhana hizo katika LL.

### 4.1.6 Matumizi ya Ufafanuzi na Maelezo

Katika mkakati huu, mtafsiri huwa na uhuru wa kujenga maana upya. Njia hii ya kutafsiri hutumika pale ambapo mtafsiri anakumbana na neno linaloweza kuwasilisha dhana inayorejelewa kwa uhalisia zaidi au kwa njia inayovutia zaidi katika LL, kama inavyodhihirika hapa:

Kielelezo 25

| | |
|---|---|
| Serikali imepuuzilia mbali madai ya muungano wa CORD kwamba kulikuwa na mapendeleo katika uteuzi uliofanywa hivi majuzi wa wenyeviti wa mashirika mbali mbali ya serikali. Mkurugenzi wa mawasiliano katika Ikulu ya rais Munyori Buku amesema rais alizingatia ujuzi na uwakilishi wa maeneo katika uteuzi huo, kinyume na madai ya upinzani. Kwenye taarifa kwa vyombo vya habari, Munyori alisema uteuzi unaofanywa na rais ni wa kitaifa na unawakilisha maslahi ya Wakenya wote. Aliongeza kuwa rais amewateua Wakenya wanaostahili kuisaidia serikali kutimiza ahadizake kwa Wakenya. Munyori amesema katika uteuzi huo, rais aliwapa vijana fursa ya kuongoza, akitoa mfano wa Ronald Osumba aliyeteuliwa mwenyekiti wa bodi ya ushauri kuhusu maswala ya vijana na mwanariadha Paul Tergat, aliyeteuliwa kuwa mwenyekiti wa bodi ya kituo cha kukuza michezo hapa nchini. Munyori alisema kuwa wakuu wa benki za Equity na KCB **James Mwangi na Joshua Oigara waliteuliwa kuwa wenyeviti wa Bodi ya Ruwaza ya 2030 na bodi ya kuthibiti sekta ya Kawi mtawalia** ili kuharakisha na kufanikisha mageuzi yanayoendelea katika asasi za serikali. **Wabunge wa chama cha ODM wametoa wito kurejelewa upya zoezi la uteuzi.** | *Koesio serikali ngalek chekomwa komosta neesio tetutikab serikali nebo CORD kole kokisub ngalekab tiliandit eng lewenisiosiek chekoyai eng konekit. Komwa director nebo letaetab logoiywek eng kotab pororiot, Munyori Buku kole kokilewen ngamotik kobun komoswek tugul chebo emoni koek chebo ngecherok eng board cheterter chebo kibagengeisiekab serikali. Eng logoiywek chekoimong eng betutab jumapili, ko komwa Munyori kole lewensionoto koboru itondo nebo emetab Kenya. Kotes komwa kole koituiyo presidentbarnotik chetinyei kimnatet ak kamugetab koyai boisiet. Koiaror agobo Ronald Osumba nekokilewen koek nebo ngecheret eng Youth Advisory Board ak nekinamu record nebo ngwony komugul eng labatetab marathon Paul Tergat ne eng nguni ko nebo ngecheret eng Kenya Academy of Sports Council. Komwa Munyori kole kongelewen ofisaek cheech chebo benkitab Equity ak Kenya Commercial Bank,* ***James Mwangi and Joshua Oigara koek chebo ngecherok eng Vision 2030 ak Kibagengeit nebo tetutik ab kimnotosiek kosubigei kou noto*** *kowendi koyaei kisuldae eng chokchinet walutik chetesetai serikali eng mornokchik.* ***Kakon kurseet membek ab kot ne king'oteen ng'atutik chebo chamait ab ODM keketyi kogeny tetutiet ab lewenisionotok.*** |

33. …James Mwangi na Joshua Oigara waliteuliwa kuwa wenyeviti wa Bodi ya Ruwaza ya 2030 na Bodi ya kuthibiti sekta ya Kawi **mtawalia**…

*…kokilewen James Mwangi ak Joshua Oigara koek chebo ng'echerok eng Vision 2030 ak kibagengeit nebo tetutik ab kimnotosiek **kosubgei kou notok…***

(James Mwangi na Joshua Oigara walichaguliwa kama wenyeviti wa Ruwaza ya 2030 na Bodi ya Mipango ya Kawi **kufuatana namna ilivyo…)**

Neno *mtawalia* linaibusha changamoto ya kulitafsiri kutokana na hali ya LL kukosa neno moja mwafaka linaloweza kujisimamia kama kisawe chake. Mtafsiri ameikabili changamoto hii kwa kutumia njia ya ufafanuzi au kulitolea maelezo. Tafsiri ya neno *mtawalia* kuleta maana ya *kufutana namna ilivyo* kunakaribia maana iliyokusudiwa kwa kuwa HL itahusisha mhusika wa kwanza na wadhifa wa kwanza naye mhusika wa pili akahusishwa na wadhifa wa pili.

**4.1.7 Ufutaji wa Neno Linalotatiza**

Mtafsiri anaposhindwa kabisa kuelewa maana iliyokusudiwa ya dhana fulani, anaweza kufungia nje neno hilo hasa pale ambapo ufutaji huo hauathiri pakubwa maana ya matini kwa jumla. Hata hivyo, hali ya mtafsiri kufutilia mbali neno anaposhindwa kuelewa maana ya neno lenyewe haichukuliwi kama mkakati wa kukabiliana na matatizo ya tafsiri. Pale ambapo mtafsiri anafanya uamuzi wa kimakusudi kufungia nje neno kwa sababu zinazoeleweka basi huangaliwa kama mkakati. Maneno yanayoibua haja ya kufutwa ni kama maneno ya mwambatano, istilahi za taaluma mahususi ambazo ni ngumu kuzitafsiri na maneno yanayokwenda kinyume na adabu ya LL au yanayokorofisha mbeko za jamii ya LL. Mkakati huu umetumiwa na mtafsiri kukabiliana

na ugumu wa kutafsiri dhana iliyokolezwa katika dondoo lifuatalo la MC kutoka kielelezo 19:

34. Akiongea na maelfu ya **mahujaji** katika eneo la St. Peter's Square…

*Kangong'ololchin elfuisiekab biik eng kanisetab St. Peter's Square…*

(Akiongea na maelfu ya **watu** katika kanisa la St. Peter's Square…)

Mtafsiri ametumia mkakati wa kufungia nje neno *mahujaji* kwa kuwa ni neno linalofungamana na dini na ni desturi ambayo haipatikani katika jamii ya LL. Kule kurejelewa na mtafsiri kwa wahusika hawa kama *maelfu ya watu* katika tafsiri hakuathiri pakubwa maana katika MC kwa kuwa inaweza kueleweka kwa HL hasa inapowekwa katika muktadha wa dini inayorejelewa katika matini. Hii ni kwa sababu inakuwa bayana kwamba *mahujaji* lazima ni 'watu' waliofika eneo lililotajwa kwa shughuli maalum ya kidini japo shughuli yenyewe huwa ni ya kidhahania kwa HL kwa sababu hadhira yenyewe haina mazoea ya shughuli hiyo kutokea katika mazingira yake halisi.

### 4.1.8 Uundaji wa Istilahi Mpya

Mtafsiri anapokumbana na dhana isiyo na kisawe chake, wakati mwingine anapaswa kuwa mbunifu na kuunda istilahi zinazowakilisha dhana zinazotataiza. Lugha zote zina sifa ya kuwa na uhai kwa mantiki kwamba kila lugha haiachi kukua. Kukua kwa lugha kunasababishwa na kuibuka kwa dhana mpya katika jamii za ulimwenguni kutokana na ukuaji na maendeleo ya kiteknolojia, kiuchumi, kisiasa, kijamii n.k (Iribemwangi na Mukhwana 2011:156) Katika uundaji wa istilahi, ni sharti mtafsiri awe na misingi imara inayotumika katika uundaji wake. Istilahi ziundwapo ni lazima zioane na dhana ambazo

zinawakilisha. Lugha zote huwa na mbinu mbalimbali za kuunda istilahi zake. Katika sehemu hii, tutachunguza njia zinazotumika kuunda istilahi katika lugha ya Kikipsigis ambayo ni LL katika utafiti huu.

#### 4.1.8.1 Ukopaji

Mbinu hii hutumika kwingi katika uundaji wa maneno katika lugha nyingi za ulimwengu. Ni jambo la kawaida kwa lugha kukopana maneno na sifa hii haistahili kuangaliwa kama udhaifu wa lugha inayokopa. Ukopaji tunaorejelea hapa ni ule wa kuchukua neno jinsi lilivyo katika LC na kulitumia vivyo hivyo katika LL bila kupitia mabadiliko yoyote. Katika matini za TH mbinu hii inadhihirika ifuatavyo namna ilivyotumika katika kielelezo 20:

35. Watu 24 wamelazwa kufuatia ugonjwa wa **kipindupindu** huko Siaya…

    *Tesetai ak kanyoiset biik 24 kosubkei ak miondo nebo* ***kipindupindu*** *eng' Siaya…*

    (Watu 24 wanaendelea na matibabu kufuatia ugonjwa wa **kipindupindu** huko Siaya…)

Neno lililokolezwa limetumika vivyo hivyo katika lugha zote zinazohusika, LC na LL pasipo kuathiri maana kwa licha ya neno hilo kuwa geni katika LL, maana yake hueleweka kwa HL kwa namna kama ile inayofikia hadhira ya MC.

Pia kuna aina ya ukopaji unaojulikana kama tafsiri mkopo. Njia hii inahusu tafsiri ya neno kwa neno au mofimu kwa mofimu kutoka LC hadi LL. Katika mbinu hii, neno au umbo lake halikopwi bali maana ya neno au fungu la maneno hukopwa kutoka LC. Njia

hii hutumika sana hasa katika tafsiri ya dhana zipatikanazo katika majina ya makampuni, mashirika, tume, vyama na taasisi mbalimbali. Imeshuhudiwa kwamba mara nyingi mbinu hii inapotumika, huandamana na vifupisho vya majina ya taasisi hizo katika lugha ya Kiingereza iwe katika MC au ML. Hali hii huchochewa na hadhi au jukumu la Kiingereza kama lugha rasmi na kule kutumika kwake kwa mapana kuliko lugha zinazohusika katika utafiti huu. Tutarejelea kielelezo 21 ili kuthibitisha matumizi ya mbinu hii.

36. … Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka, IEBC

*… Kibagengeit ne Telelchinge nebo Lewenishet ak Kiwatosiek, IEBC*

(… Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka, IEBC)

Kutokana na mifano iliyotolewa, ni wazi kwamba LL imejitajirisha kimsamiati kwa kupata maneno kutoka LC na kuyatafsiri. Hali hii inadhihirisha umuhimu wa mtafsiri kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu kanuni zinazoongoza shughuli ya tafsiri kama njia ya kupanua msamiati wa lugha mbalimbali.

#### 4.1.8.2 Utohozi

Mbinu hii huhakikisha kwamba neno linalokopwa linafanyiwa urekebishaji ili lifuate kanuni za kifonolojia za LL. Mbinu hii ya kukuza msamiati husisitiza kwamba neno geni linatolewa ugeni ili liingiliane kimuundo na maneno ya LL. Mabadiliko yanayofanyiwa neno huepusha LL hatari ya kulemazwa na miundo mipya kutoka LC inayochangia msamiati. Katika mbinu hii, si lazima LL ipate maneno kutoka LC ya tafsiri tu bali

huvuka mipaka ya lugha za tafsiri na kupata maneno kutoka lugha nje ya zile zinazohusika katika tafsiri.

37. … **wabunge** wa **chama** cha ODM wametoa wito kurejelewa upya zoezi la…

*… kakon kurseet* ***membaek*** *ab kot ne king'oteen ng'atutik chebo* ***chamait*** *ab ODM keketyi kogeny tetutiet ab…*

(… **Wabunge** wa **chama** cha ODM wametoa wito kurudiwa kwa mpango wa…)

(Rej kie 25)

Neno la kwanza, *membaek* limetoholewa kutoka lile la Kiingereza, *members,* huku neno la pili, *chamait* likitoholewa kutoka neno la Kiswahili, *chama.*

**4.1.8.3 Uhulutishaji**

Hii ni njia ya kuchukua visehemu vya maneno katika maelezo na kuunda neno moja. Vipashio viwili au zaidi ambavyo katika hali ya kawaida havipaswi kuwa pamoja kulingana na muundo wa lugha huletwa pamoja.

38. … katika **kisiwa** kilichoko kaskazini…

*… en* ***ikwembeiyot*** *nemi murot tai…*

(Rej kie 13)

Neno lililozalika linatokana na kuunganishwa kwa visehemu vya maneno tofauti kama ifuatavyo:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| *I* | + | *kwen* | + | *bei* | + | *yot* |
| ↑ | | ↑ | | ↑ | | ↑ |
| Kiambishi awali cha nomino | | katikati | | maji | | kiambishi tamati cha nomino |

Kutokana na kuunganishwa kwa visehemu vya maneno haya, inabainika kwamba kuna mabadiliko yanayotokea katika neno linalozalika. Neno linakuwa *ikwe**m**beiyot* badala ya *ikwe**n**beiyot* kama inavyotarajiwa. Hii inatokana na mojawapo ya mifanyiko ya kifonolojia inayotajwa kama usilimisho pamwe wa nazali ambapo nazali huchukua sifa ya kutamkiwa katika sehemu moja na konsonanti inayoitangulia. Katika muktadha huu nazali /n/ inayotamkiwa ufizini huchukua sifa ya /m/ inayotamkiwa midomoni, sawa na /b/ ambayo inaitangulia.

#### 4.1.8.4 Ukatizaji

Njia hii ya kuunda istilahi inahusu ufupishaji wa majina, maneno au vifungu vya maneno. Ufupishaji huu huyafanya maneno yanayopitia mabadiliko ya aina hii kuwa na silabi chache kuliko maneno asilia. Ufupishaji katika lugha ya Kikipsigis aghalabu hufanywa ili kutofautisha dhana halisi na dhana ya kijumla. Hata hivyo kuna wakati ambapo neno asilia na lile lililofupishwa hubeba maana sawa.

Kielelezo 26

| | |
|---|---|
| Wafanyikazi katika kampuni moja ya pareto katika kaunti ya Nakuru wameanza mgomo wao leo kushinikiza kampuni hiyo kuwalipa mishahara yao. Walisema **wamekasirishwa na kitendo cha kampuni hiyo kutowapa malipo yoyote kwa kazi waliyofanya katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita.** Haya yanajiri wakati makarani wawili wamekamatwa kwa kushukiwa kuhusika katika uteketezaji wa nyumba ya karani mwenzao katika kampuni hiyo. **Inadaiwa kuwa washukiwa hawa waliteketeza nyumba hiyo ili kuharibu ushahidi uliokuwa katika stakabadhi zilizohifadhiwa mle.** | *Kagongelelchi boisiet kiboitinik che kampunit agenge nebo mauek en kaunti nebo Nakuru kosubgei ak melekwek che tomo kigochi ichek.* ***Kaibor neregek kosubgei ak yautiet ne komwa kole tomo kolibonchi kampunit notok melek alak tugul en kasartab arawek somok che kogosirto.*** *Kabit nitok en kasarta ne kakinam siriik aeng' en mwaet kele kobel ichek kootab sirindet ne boisiei tugul en kampuninotok.* ***Mwaat kele kobel bichoton kimusyin agobo lelutionotok kootok asi kowechawech baornatetab baronok che komi yotok.*** |

39. … wamekasirishwa na kitendo cha kampuni hiyo kutowapa **malipo** yoyote kwa kazi waliyofanya katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

*… kaibor neregek che ech kosubkei ak yautiet ne komwa kole tomo kolibonchi kampunit notok **melek** alak tugul en kasartab arawek somok che kogosirto.*

Tafsiri ya dhana *malipo* imefupishwa kuwa *melek* kutokana na dhana asilia ya *melekweek* au *melekta.* Jambo hili ni la kawaida katika lugha nyingi na mara nyingi lengo lake ni kuleta mvuto katika lugha. Aidha, ufupishaji wakati mwingine hutumiwa kutekeleza majukumu ya kisemantiki pale ambapo neno lililofupishwa linawasilisha maana tofauti na ile iwasilishwayo na neno asilia katika ukamilifu wake kabla ya kufupishwa.

#### 4.1.8.5 Urudufishaji

Hii ni njia ya kuunda neno jipya kutokana na kurudiwa kwa shina la neno fulani. Katika mbinu hii, maana inayoibushwa huenda ikahusiana na maana iliyoko kwenye shina linalorudiwa au liwe na maana tofauti.

40. … inadaiwa kuwa washukiwa hawa waliteketeza nyumba hiyo ili **kuharibu** ushahidi uliokuwa katika stakabadhi zilizohifadhiwa mle.

*... mwaat kele kobel bichotok kimusyin agobo lelutionotok kootok asi ko**wech**a**wech** baornatetab baronok che komi yotok.*

(Rej kie 26)

Dhana *ko-**wech**-a-**wech*** ni kitenzi kilichotafsiriwa kutokana na kitenzi *kuharibu.* Kitenzi hiki kinatokana na kurudufishwa kwa shina -*wech*- ambalo lina maana ya kuharibu. Njia hii imemfaa mtafsiri kukabili changamoto ya ukosefu wa dhana linganifu. Mara nyingi urudufishaji hutumika kwa lengo la kuweka msisitizo kwenye ujumbe.

### 4.1.9 Ujuzi na Stadi za Tafsiri

Kutokana na hali kwamba lugha za ulimwengu hazina maingiliano wala maafikiano katika taratibu za kidhana na kiistilahi, uhawilishaji wa maana ya kimatini kutoka LC hadi LL si jambo la moja kwa moja bali ni zoezi linalopitia mchakato tata. Ni shughuli ya kiutekelezi ambayo humhitaji mtekelezaji, ambaye katika muktadha huu ni mtafsiri, ajihami na ufahamu, maarifa, ujuzi na stadi za aina mbalimbali:

Maarifa na stadi za kimawasiliano katika LC na LL. Hii ni kwa sababu lugha zinatofautiana kwa namna mbalimbali. Aidha, kila lugha imepangwa kwa njia ya kuueleza uhalisia wa ulimwengu kwa kutumia mionoulimwengu inayotofautiana. Anapaswa kuelewa niundo, maumbo na mipangilio ya sheria za kisarufi za lugha zote mbili zinazohusika katika tafsiri. Ili kutekeleza shughuli ya tafsiri katika ubora wake, anapaswa kuwa na umilisi wa kutosha katika lugha hizo ili kumudu zoezi lake katika kiwango chochote cha uchangamano.

Maarifa kuhusu jinsi mafungu ya kimaana yanavyoundwa na kuhusishwa katika matini. Kwa kuwa tafsiri ni taaluma iliyo na uhusiano wa chanda na pete na isimu, mtafsiri anapaswa kuwa ujuzi wa kutosha katika kiwango cha semantiki. Anapaswa kuwa na utaalamu wa kusoma na kuandika katika lugha zote mbili. Udhibiti wa maumbo na

matumizi ya lugha zenyewe, sheria na masharti ya kisarufi katika lugha hizo, sheria na masharti ya kimsamiati pamoja na sheria zinazohusiana na maana na mifumo ya maana ni mambo ya muhimu yanayomwongoza mtafsiri kufikia ubora wa juu ya kazi yake. Maendelezo ya maneno, uakifishaji na uundaji wa sentensi ni mambo yanayoweza kuzua maana tofauti tofauti kutegemea namna vipengele hivyo vimejitokeza katika matini.

Maarifa na stadi za ulinganishaji. Ujuzi huu utamsaidia kulinganisha mambo mbalimbali yapatikanayo katika matini kwa kuzingatia mifumo miwili ya lugha zinazohusika katika tafsiri. Ulinganishaji na uhusishaji wa matini katika LC na LL ni stadi inayohitajika kwa mtafsiri anayelenga matokeo bora ya zoezi la tafsiri. Matini ya aina yoyote husheheni mambo mbalimbali ambayo yanahitaji ulinganishaji ili kumwezesha mtafsiri kukadiria iwapo ulinganifu wa maana umefikiwa. Uwezo wa kutafsiri pia unahitaji mtafsiri awe na utambuzi wa mambo yanayohusiana kwa namna mbalimbali.

Maarifa ya namna ya kushughulikia matini inayotafsiriwa. Awe na uelewa kuhusu sifa za matini za aina mbalimbali na kuwa na uwezo wa kubainisha sifa za aina hizo za matini. Ujuzi wa aina hii utamwezesha kuitathmini matini anayoitafsiri kwa uhakika na baadaye kuidurusu ML ambayo huibuka kutokana na tafsiri anayoshughulikia. Ujuzi wa masuala muhimu kuhusu taaluma mbalimbali zinazoingiliana na taaluma ya tafsiri pia humwezesha mtafsiri kukabili kwa wepesi utekelezi wa tafsiri. Hivyo basi mtafsiri anapaswa kuwa na udhibiti wa msamiati na istilahi katika taaluma mbalimbali.

## 4.2 HITIMISHO

Katika sura hii tumechanganua mikakati mbalimbali ya kukabiliana na ukosefu wa ulinganifu wa maana katika tafsiri za taarifa za habari, unaosababishwa na matatizo ya aina mbalimbali. Imebainika kwamba jambo la muhimu ambalo mtafsiri anapaswa kutilia maanani kabla ya kuteua mkakati wowote ule ni kutambua miktadha ya matumizi ya maneno au dhana zinazozua changamoto za kutafsiri. Ni kutokana na utambuzi huo ndiposa anaweza kukadiria mkakati utakaomwezesha kuhakikisha kwamba anawasilisha ujumbe wa kimatini katika MC kwenye ML kwa namna itakayoeleweka kwa hadhira za MC na ML kwa njia iliyo sawa au kwa namna zinazokaribiana zaidi. Pia ni dhahiri kwamba mikakati miwili au zaidi inaweza kutumiwa kwa pamoja kukabiliana na tatizo fulani moja. Aidha, ni bayana kwamba ujuzi, maarifa, utaalamu na ubunifu wa mtafsiri mwenyewe ni uti wa mgongo wa tafsiri bora zaidi.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 UTANGULIZI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza ulinganifu wa TH kwa kufanyia tathmini tafsiri zinazofanywa kutoka lugha ya Kiswahili katika idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Kitaifa-KBC hadi Kikipsigis katika kituo cha Kitwek ambacho ni mojawapo ya vituo vya redio vinavyotoa matangazo katika lugha za kienyeji katika Shirika la Utangazaji la Kitaifa. Uchunguzi huu umefanywa kwa kuzingatia nadharia ya ulinganifu huku mwegemeo ukiwa kwenye ulinganifu amilifu. Aidha, nadharia ya mawasiliano imetumika kama nadharia changizi. Nadharia hizo mbili zimetumika kwa usambamba kutoka na uhusiano mkubwa uliopo katika misingi yazo.

Uchunguzi huu umebainisha kwamba kuna matatizo ya aina mbalimbali yanayomkumba mtafsiri anapojaribu kuhawilisha ujumbe wa kimatini katika TH. Matatizo yenyewe yana athari ya kusababisha ukosefu wa ulinganifu wa maana kati ya MC na ML za TH. Matatizo yanayorejelewa hapa yanasababishwa na vyanzo mbalimbali, na ujuzi wa vyanzo vyenyewe kwa mtafsiri humwongoza katika uteuzi wa mikakati mwafaka ya kukabiliana na matatizo hayo. Aidha, imebainika kwamba ubora wa tafsiri huathiriwa na aina ya tafsiri inayotumiwa kushughulikia zoezi lenyewe. Kwa ujumla, tatizo la ukosefu wa ulinganifu wa maana ni suala ambalo linaathiri tafsiri zinazofanywa katika vyombo vya habari.

Kupitia mahojiano yetu na wanahabari wanaohusika na tafsiri za TH, ilibainika kwamba kuna muda mfupi sana wa kushughulikia tafsiri za habari zilizokwisha kukusanywa. Kwanza ukusanyaji wa habari zenyewe huchukua sehemu kubwa ya muda uliotengewa mchakato mzima wa upataji na uwasilishaji wa habari. Baada ya ukusanyaji wa habari kuna uhariri wa habari hizo zikiwa bado katika LC. Uhariri hujumlisha shughuli mbalimbali zikiwemo urekebishaji wa makosa ya aina tofauti tofauti na kuainisha habari zenyewe kulingana na upeo kama ni za kimaeneo, kitaifa na kimataifa; au kulingana maudhui kama ni za siasa, afya, michezo, utabiri wa hali ya anga n.k.

Uhariri pia huhusu kutathmini athari inayoweza kuibushwa na uwasilishaji wa habari fulani kwa wasikilizaji, k.m huenda habari fulani zikamharibia mtu sifa na akachukulia shirika hatua za kisheria au habari fulani zikaathiri vibaya hisia za wasikilizaji na kusababisha uhasama miongoni mwa makundi fulani ya watu. Muda unaobaki unatumika katika kutafsiri TH na mara nyingi shughuli hii hufanywa haraka kutokana upungufu wa muda. Jambo hili linasababisha kutokea kwa makosa ya aina mbalimbali. Pia wakati mwingine kunakosekana muda wa kutosha kuipitia tena kazi iliyotafsiriwa.

## 5.1 HITIMISHO

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza aina mbalimbali za tafsiri zinazotumika katika tafsiri za TH kutegemea aina za matini zinazoshughulikiwa. Tumetathmini jinsi aina za tafsiri zinazoteuliwa zinavyoathiri ulinganifu wa maana. Aidha, tumeangazia nguvu na upungufu wa kila mojawapo ya aina nne za tafsiri zilizoteuliwa: tafsiri ya moja kwa moja, tafsiri huru, tafsiri maana na tafsiri mawasiliano. Uchanganuzi wetu umebainisha kwamba japo aina hizo za tafsiri zinatofautiana kwa

namna mbalimbali, kila mojawapo huwa na umuhimu pamoja na dosari zake. Pia ni wazi kwamba aina fulani moja ya matini huweza kushirikisha aina zote za tafsiri almuradi kila mojawapo huwa na sehemu ambayo ina ufaafu zaidi ya nyingine.

Uchanganuzi wa aina za tafsiri umedhihirisha kwamba tafsiri mawasiliano na tafsiri maana zinachangiana kwa namna moja au nyingine kuibusha tafsiri bora inayodumisha maana ya kimatini. Katika muktadha wa uchunguzi wetu, lugha tunazoshughulikia hazitoi nafasi kubwa kwa tafsiri ya moja kwa moja kutumika kutokana na lugha zenyewe kutofautiana kisarufi na kimuundo. Viwango vikubwa vya upotoshaji wa maana hushuhudiwa pale ambapo tafsiri ya moja kwa moja hutumika. Uhuru mwingi wa mtafsiri unaohusishwa na tafsiri huru humfanya mtafsri kuchopeka mambo yasiyopatikana katika MC kwenye ML na wakati mwingine afutilie mbali mambo muhimu yapatikanayo kwenye MC ya TH.

Madhumuni yetu ya pili yalikuwa ni kuchunguza matatizo yanayokumba tafsiri za TH. Imedhihirika kwamba matatizo haya yanasababishwa na vyanzo anuwai. Yapo matatizo yanayoletwa na tofauti za kiisimu baina ya lugha zinazohusika katika tafsiri, kutofautiana kwa lugha hizo katika vipengele mbalimbali vya utamaduni, matatizo yanayohusu upungufu kwa upande wa mtafsiri na matatizo mengine ambayo hayahusiani na ujuzi na maarifa ya mtafsiri. Kueleweka kwa matatizo haya na vyanzo vyake kunamsaidia mtafsiri kufanya uteuzi mwafaka wa mikakati itakayomwezesha kukabiliana na changamoto za tafsiri.

Madhumuni yetu ya mwisho yalikuwa yalikuwa ni kupendekeza mikakati mbalimbali ambayo mtafsiri anaweza kutumia kukabiliana na matatizo ya tafsiri. Jambo linalochukua nafasi muhimu katika zoezi la tafsiri ni utambuzi wa mtafsiri wa miktadha ya matumizi ya maneno au dhana zinazozua changamoto za kutafsiri. Hali hiyo itamwezesha kutathmini mikakati itakayomfaa ili kuhakikisha kwamba ujumbe wa kimatini anaohawilisha kutoka MC hadi ML unaweza kufasiriwa na kueleweka kwa HL kwa njia isiyoleta utata wowote. Mtafsiri, kwa hivyo, anapaswa kuwa na ujuzi, maarifa na utaalamu katika mambo mbalimbali kupatikana kwa tafsiri bora.

## 5.2 MAPENDEKEZO

Kuna haja ya kufanywa kwa utafiti zaidi ili kubaini ulinganifu wa maana katika tafsiri zinazofanywa kutoka Kiswahili kama LC hadi lugha nyinginezo za kiasili. Utafiti huu ulijikita katika tafsiri za TH kutoka Kiswahili hadi Kikipsigis na tunapendekeza utafiti wa aina hii kufanywa kwa kuzingatia lugha nyininezo za kienyeji kama LL. Kwa kuwa utafiti huu ulizingatia lugha moja ya kibantu na nyingine isiyo ya kibantu kama LC na LL mtawalia, tunapendekeza utafiti kufanywa kwa kuzingatia Kiswahili na lugha yoyote nyingine ya kienyeji yenye asili ya kibantu ili kutathmini iwapo tofauti za jamii za lugha zina athari katika viwango vya ulinganifu wa maana.

Vilevile tunapendekeza utafiti kufanywa kuhusu tafsiri zinazofanywa kutoka Kiingereza hadi lugha za kiasili kwa sababu lugha za Kiswahili na Kiingereza zina hadhi sawa katika katiba ya sasa ya Kenya kama lugha rasmi na zina matini za aina nyingi ambazo zimetafsiriwa hadi lugha nyingi za humu nchini. Utafiti wa aina hii unaweza kufanywa katika vyombo vingine vya habari kama runinga, magazeti na majarida. Kuna jarida la

‘Kass Weekly’ ambalo lina safu mbili katika kurasa zake, safu moja ikiwa na makala katika lugha ya Kiingereza huku tafsiri zake hadi Kikalenjin zikiwa katika safu nyingine. Tafsiri za sampuli hiyo zinaweza kutathminiwa ili kustawisha taaluma ya tafsiri inayoendelea kunawiri.

Tunapendekeza utafiti wa aina hii pia kufanywa nje ya mipaka ya vyombo vya habari. Kuna tafsiri nyingi za kimatibabu zinazofanywa katika hospitali, zahanati na taasisi nyinginezo za kiafya zinazotoa maelekezo kuhusu sehemu mbalimbali za taasisi hizo, maelezo kuhusu maradhi ya aina fulani, namna ya kutumia dawa fulani n.k. Pia kuna tafsiri zinazofanywa katika biashara, maandiko ya kidini na tafsiri katika nyanja nyinginezo. Kutokana na tofauti za kisajili katika nyanja hizi huenda kuna mambo fulani mapya yanayofungamana na taaluma ya tafsiri ambayo tafiti hizo ambazo zinaweza kufanywa kwa kuegemea nadharia mbalimbali zitaweka wazi na kuziba mianya katika taaluma ya tafsiri.

## MAREJELEO


Ali, C. W. (1981). The Problem of Translating from English into Kiswahili as Exemplified by VOK News Items. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Austin, J. L. (1962). *How to Do Things with Words*. London: OUP.

Baker, M. (1992). *In Other Words: A Coursebook on Translation*. London: Routledge Publishers.

Beekman, J. A. & J. Callow (1974). *Translating the Word of God.* Michigan: Zondervan Public House.

Buliba, A na wengine (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili.*Nairobi: JKF.

Cartford, J. (1965). *Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.

Chesaina, C. (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. Nairobi: Heinmann Kenya Limited.

Correia, R. (2001). Translation of EU Legal Texts. Katika A. Tosi (Mha), *Crossing Barriers and Bridging Cultures: The Challenges of Multilingual Translation for the European Union* (uk. 38 - 44). Frankfurt: Multilingual Matters Ltd.

Crystal, D. (2008). *Dictionary of Linguistics and Phonetics* (6th Ed). London: Routledge.

Djik, T. A. (1977). *Text and Context: Explorations in the Semantics and Pragmatics of Discourse.* London: Longman.

Gutt, E. A. (1989). *Translation and Relevance*. University of London: Tasnifu ya Uzamifu.

Hatim, B., na Mason, I. (1990). *Discourse and the Translator*. London: Routledge.

__________________ . (1997). *The Translator as a Communicator*. London: Routledge.

Hatim, B., na Munday, J. (2004). *Translations: An Advanced Resource Book.* Oxon: Routledge.

Hermans, T. (2002). Paradoxies and Aporias in Translation and Translation Studies. Katika A. Riccadi (Mha), *Translation Studies: Perspectives on an Emerging Discipline* (uk. 10 -23). Cambridge: Cambridge University Press.

Hickey, L. (1998). Introduction. Katika L. Hickey (Mha), *The Pragmatics of Translation* (uk.1-9). Johannesburg: Multilingual Matters.

House, J (1977). *Translation Quality Assessment: A Model Revisited.* Tubigen: Narr.

Hudson, R.A (1980). *Sociolinguistics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Iribemwangi, P&A. Mukhwana (2011). *Isimujamii.* Nairobi: Focus.

Jakobson, R. (2000). On Linguistic Aspects of Translation. Katika L. Venuti (Mha), *The Translation Studies Reader* (uk. 113 - 118). London: Routledge.

Jerono, P (2011). Tugen Word Order. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Kamau, G. (2008). Meaning Translation in the Kiswahili Translation of George Orwell's Animal Farm. MA Thesis. Kenyatta University: Unpublished.

Kilonzo, O. (2011). Challenges of Attaining Equivalence in Television News Translation in Kenya. MA Thesis. University of Nairobi: Unpublished.

Kimugung, S. (2014). Mitindo Mamboleo ya Ubaadausasa Katika Nyimbo Teule za Jamii ya Kikalenjin. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Moi. Haijachapishwa.

Kipkorir, B. (1985). *People of Rift Valley: Kalenjin*. London: Evans Brothers Limited.

Larson, M. L. (1984). *Meaning Based Translation: A Guide to Cross-Language Equivalence*. New York: University Press of America.

Leech, G. (1983). *Principles of Pragmatics*. Nairobi: Longman.

Lefevere, A. (1975). *Translating Poetry*. Goreum of Assen.

Manfredi, M. (2008). Translating Text and Context: Translation Studies and Systemic Functional Linguistics. Bologna.

Moraa, A. (2013). Matatizo Yanayodhihirika Katika Matini Tafsiri za Kimatibabu: Utafiti Kielelezo Katika Hospitali ya Kisii Level 5. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Muchemi, L. (1998). Kuathirika kwa Usahihi na Udhahiri Katika Tafsiri: Magazeti ya Daily Nation na Taifa Leo. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Muchiri, G. (2012). Issues of Kswahili Language Interference in Students' English Translations and vice versa: A Case Study of Masters/Undergraduate Translations in English and Kiswahili. MA Thesis.University of Nairobi: Unpublished.

Munday, J. (2008). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications*. Oxon: Routledge.

Mutie, E. (1997). Sanaa Katika Tafsiri: Matatizo na Athari Zake. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Mutugi, H. K. (2012). Pronominal Arguments in Translation: A Case of Translating Between English and Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili iliyotolewa Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Mwangi, I. (1996). Matatizo ya Leksikografia-Tafsiri: Tathmini ya F. Johnson (1939) Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Mwansoko, H. J., Mekacha, R. D., Masoko, D. L., na Mtesigwa, P. C. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu* (Toleo la Pili). Dar es Salaam: TUKI.

Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation.* Hertfordshire: Prentice Hall International English Language Teaching Ltd.

Nida, E. (1964). *Towards a Science of Translating.* Leiden: E. J. Brill.

_______ (2000). *Principles of Correspondence*. Katika L. Venuti (Mha), *The Translation Studies Reader* (uk. 126 - 140). London: Routledge.

Nyaga, P. (2009). Dhana ya Ulinganifu Katika Tafsiri ya Fasihi: Tathmini ya Usaliti Mjini. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Nyangeri, A (2014). Vitendo Usemi na Ulinganifu wa Maana Katika Tafsiri: Mifano Kutoka Tafsiri za Kazi Mbili za Barbara Kimenye. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Omboga, Z. J. (1986). Fasihi Tafsiri katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili. Matatizo na Athari Zake. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

____________ . (2006). Siting Text Culture and Pedagogy in Literal Translation: A Theorization of Translation in Culture Transfer with Examples from Selected

Texts in Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu iliyotolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Osano, O (1997). Dhana na Matatizo ya Tafsiri: Tathmini ya Risasi Zianzapo Kuchanua. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Otwere, S. (2012). Usonde Katika Tafsiri: Tathmini ya Mafundisho ya Biblia Katika Shule za Sabato kwa Watu Wazima. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Pym, A. (1998). *Method in Translation History*. Manchester: St Jerome.

______ (2010). *Translation and Text Transfer: An Essay on the Principles of Intercultural Communication.* Frankfurt: Tarragona: Intercultural Studies Group.

______ (2010). *Exploring Translation Theories.* London: Routledge.

Quine, W. V. (2000). *Meaning and Translation*. Katika L. Venuti (Mha), *The Translation Studies Reader* (uk. 94 -112). London: Routledge.

Rabin, C. (1958). *The Linguistics of Translation*. Katika H. Smith (Mha), *Aspects of Translation: Studies in Communication*. London.

Robinson, D. (2003). *Becoming a Translator: An Introduction to the Theory and Practice of Translation* (2nd Ed.). New York: Routledge.

Saldanha, G. (2009). Linguistic Approaches. Katika M. Baker, na G. Saldanha (Wah), *Routledge Encyclopedia of Translation Studies*, (2nd ed.). London: Routledge.

Sequeiros, X. R. (2009). Translation, Pragmatics. Katika J. L. Mey (Mha), *The Concise Encyclopedia of Pragmatics* (2nd Ed.) (uk. 1097 - 1100). Oxford: Elsevier Ltd.

Seronei, K. (2011). *Samburtaab Ng'aleekaab Kaleenchiin.* Nairobi: Focus.

Shitemi, N. L. (1990). Mawasiliano katika Tafsiri: Uteuzi wa Mfasiri. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa.

Snell-Hornby, M. (2006). *The Turns of Translation Studies.* Amsterdam: John Benjamins.

Sultan, K. M. (2007). *The Semantics, Pragmatics and Translation of Speech Acts*. Journal of College of Basic Education No. 50, 32 – 52.

Tosi, A. (2001). Conclusions. Katika A. Tosi (Mha), *Crossing Barriers and Bridging Cultures: The Challenges of Translatoin for Multilingual European Union* (uk. 128 - 131). Frankfurt: Multilingual Matters Ltd.

Toury, G. (1995). *Descriptive Translation Studies and Beyond.* Amsterdam: John Benjamins.

Toweett, A. (1979). *A Study of Kalenjin Linguistics.* Nairobi: KLB.

Trudgill, P (1974). *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society*. London: Harmonds-worth: Penguin Books.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Nairobi: OUP.

## KIAMBATISHO 1

## Vielelezo zaidi vya Taarifa za Habari

Jedwali 1

| | |
|---|---|
| Watu sita walifariki na wengine kadhaa wakajeruhiwa wakati wa jaribio la wizi lilipotibuka katika eneo la Isebania, kaunti ndogo ya Kuria Magharibi, kaunti ya Migori. Afisa mkuu wa polisi katika kaunti ya Migori, David Kirui alisema wanne kati ya watu hao walikuwa washukiwa wa wizi, ilhali wengine wawili walikuwa wapita njia. Kisa hicho kilitokea pale washukiwa hao waliojihami kwa bunduki aina ya AK-47 walipojaribu kuiba kutoka duka la Wilson Saiya ambaye ni afisa wa zamani wa polisi. Wananchi waliowaona washukiwa hao wakiingia ndani ya duka hilo waliwapasha habari maafisa wapolisi waliofika mahali hapo na wakisaidiwa na wananchi wakakimbizana na washukiwa hao hadi vichakani ambapo ufyatulianaji risasi ulizuka. Washukiwa hao waliuawa kwa kupigwa risasi huku raia wawili pia wakifariki kutokana na majeraha ya risasi. Watu wengine waliojeruhiwa wamelazwa kwenye hospitali kuu ya kaunti hiyo ambapo wanapokea matibabu. | *Kaibet biik 6 sobonwekwak ak konyor kakotonosiek alake chechang kosubkei ak chorset nemaimugak eng kebebertab Isebania nemite eng kuria cherongo, county nebo Migori. Kamwa county commander nebo Migori David Kirui kole cheboto biik chekaibet sobonwekwak ko chorik 4 ak kora raia 2 chekakinamda eng mwogetabgei ne kabit eng kwenutab askarik ak chorichotok. Kates logoywek kole chorichotok kokatieme kobokchi Hardware nebo Wilson Siya ne inee koki afisayatab police. kamwa kole icheket kokatinye bundukisiekab AK 47. Kamwa baorinik kole kakeer chorichotok kiit ne kayach konaisiechi afisaekap police che kaib kakwautietab chokchinet ak koyon icheket ole kabit mwoketabgei nebo barak. Biik che kanyor kaokotonosiekab risasisiek kotesetai konyoru kanyaiset eng sipitalitab kaunti nebo Migori.* |

Jedwali 2

| | |
|---|---|
| Upinzani nchini Syria unasema utahudhuria mazungumzo ya amani yaliyopangiwa kufanywa Jumatatu ijayo bila kutaja kwa mapana uwezekano wa kuafikia makubaliano na serikali ya Syria.Mazungumzo hayo chini ya udhamini wa umoja wa mataifa, na ambayo yameandaliwa wakati wa kuadhimisha miaka mitano tangu kuzuka kwa mzozo wa Syria, yatafanyika huko Geneva. Kamati ya mashauriano ya kundi la upinzani inasema itahudhuria mazungumzo hayo kama dhihirisho la kujitolea kwake kwa juhudi za kimataifa za kukomesha umwagikaji damu. | *Kamwa kebeberta ne esio serikali eng emetab Syria kole tun komite tuyet nebo chengetab kalyet ne tetat keyai eng betutab jumatatu asikomuch koityi kasyinet ak serikali. Tuiyonotok kotun kowendi kondochin kibagengeitab UN ak keyoen nganasetab Geneva ne notok korinyeke ak ak kenyisiek 5 kongetekei kotoikei chemarket eng emetab Syria. Kamwa committee nebo tuiyonotok kole makoyoni kotaketumda korotik eng emetab Syria.* |

Jedwali 3

| | |
|---|---|
| Vikosi vya usalama nchini Burundi jana vilimwasilisha mbele ya wanahabari mwanamme anayetuhumiwa kwa kufanyia ujasusi serikali ya Rwanda huku taharuki kati ya nchi hizo mbili ikitanda kufuatia malumbano ya kisiasa yaliyodumu katika muda wa miezi kumi. Mwanamme huyo aliyetajwa kama Corporal Rucyahintare Cyprien, alikamatwa Jumatatu katika eneo la Rushenya kwenye mpaka ya nchi hiyo. Hayo yamesemwa na msemaji wa polisi Pierre Nkurikiye. Cyprien alikiri kwa wanahabari kwa lugha ya Kinyarwanda, kuwa alikuwa nchini humo kwa lengo la kufanya ujasusi. | *Kanam afisaekab polis chi agenge ne kibwotyin kele mwoytoy emeetab Burundi eng sirikaab logoiywek akobo emetab Rwanda ye tesetay kowendi barak kayweishet eng suryet ne mitey kwenunwa nebo bolotet ne kokotar arawek taman eng nguni. Kamwa afisayat agenge nebo polis Pierre Nkurikiye kole kokinam corporal Rucyahintare Cyprien eng betutab jumatau eng kiwato nebo emetab Rwanda ak Burundi. Mwaat kele koiyab Cyprien eng kutitab kinyarwnada kole kinyoo emetab Burundi nyo konyor logoiywek tugul ak komwayta.* |

Jedwali 4

| | |
|---|---|
| Walimu katika kaunti ya Baringo wametoa wito kwa serikali kufutilia mbali barua zilizotolewa kwa walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari kwa kuto-waadhibu walimu walioshiriki mgomo wa kitaifa wa walimu mwezi Septemba mwaka uliopita. Wakiongea katika mkutano ulioandaliwa katika shule ya msingi ya Kabel katika tarafa ya Muchongoi, walimu hao walitishia kushtaki serikali iwapo barua hizo zilizoandikwa na tume ya TSC hazitafutiliwa mbali. Wakiongozwa na mweka hazina wa chama cha kitaifa cha walimu cha KNUT, tawi la Baringo, Elizabeth Keitany, walimu hao walikariri kuwa watapinga hatua ya tume ya kuratubu mishahara na marupurpu ya watumishi wa umma-SRC ya kutathmini utendakazi wa walimu iwapo matakwa yao hayatatimizwa. | *Kakokon kurset kanetik eng kaunti nebo Baringo koitchi serikali koisto baronok chekikakigachi kanetik cheechen chebo sukulishekab primary ak Secondary kotinygei ak amune asikitemene kogachi kergongyet kanetik chekisuldae kangelelchinetab boisiet eng arawetab 9 eng kenyit konye. Kongololi eng tuiyet nekokiyai eng sukulitab primary nebo Kabel nemitei eng division nebo Muchonoi eng kaunti nebo Baringo ole kokon kateunet kanetik kole bendi komuti serikali kapkirwok ak kotko meisto baronok chotok kikasir commission nesirei kanetik boisiet nebo TSC. Kondochin Treasurer nebo kipagengeitab kanetik nebo KNUT eng mornet nebo Baringo Elizabeth Keitany, ko kikimit kanetik chotok kole kiit neesio ichek tetutiet nebo job evaluation neisuldae commission nebo melekwek nebo SRC agoi kasarta nekaketeschi melekwek.* |

Jedwali 5

| | |
|---|---|
| Kesi inayowahusisha watu wanne waliokuwa wamekamatwa kuhusiana na ghasia kati ya jamii za Ogiek na Tugen, haikuanza baada ya polisi kuiomba mahakama kuwapa muda zaidi kukamilisha uchunguzi. Miongoni mwa wanne hao ni mwanachama maalumu wa bunge la kaunti la Kericho Joseph Miangari aliyeteuliwa kuwakilisha jamii za walio wachache. Wengine ni Sharon Rotich, Lilian Chebet na Josphine Kuresoi. Mahakama hata hivyo iliamua kuwa washukiwa waachiliwe kwa dhamana na kufika mahakamani wakati stakabadhi kuhusu kesi dhidi yao zitakapokuwa tayari. Ghasia kati ya jamii hizo mbili zilisababishwa na ung’ang’aniaji shamba kubwa la Ngongongeri katika sehemu ya Njoro, ambapo nyumba saba ziliteketezwa. | *Maimukak kotoikei kirwaket ne tinyei biik 4 chekikinam kotinygei ak chemarget nekibit eng kwenutab pororietab Ogiek ak Tugen. Kakosom kapkirwok koyanchi ichek kotokotestai ak chigilishet kwo kowong kotokomitei bichotok eng eunek kwak.Boto bichotok 4 MCA nekikitoror eng kaunti nebo Nakuru Joseph Miangari nekikikwei kotelelndachi pororioshek chekikitaban.Alak koboto Sharon Rotich, Lilian Chebet ak Josphine Kuresoi. Agot kou notok ko ketikon kapkirwok kitiakta bichotok eng bond nebo police ak koitita taitab kapkirwok eng kasarta nekakochobok kartasisiekab kirwaget. Maitos pororietab Ogiek ak nebo Tugen mbaret neo nebo Ngongongeri farm nemiitei komasta nebo Njoro kiit nekoyai kebel korik 7.* |

Jedwali 6

| | |
|---|---|
| Rais Barack Obama wa Marekani amewasili nchini Cuba kwa ziara ya kihistoria ambapo anatarajiwa kufanya mazungumzo na kiongozi wa kikomunusti wa taifa hilo. Rais Obama ndio rais wa kwanza aliye mamlakani kuzuru Cuba tangu mapinduzi ya mwaka wa 1959 ambayo yalisababisha uhasama wa miaka mingi. Akiongea katika ubalozi wa Marekani uliofunguliwa tena huko Havana, Obama alitaja ziara hiyo kuwa ya kihistoria. Rais Obama anatarajiwa kukutana na rais wa taifa hilo Raul Castro. Hata hivyo hatakutana na kiongozi wa zamani wa taifa hilo Fidel Castro. | *Kakoitita president Barrack Obama emet nebo Cuba eng rutoitonyi netai nebo ikwembeiyonoto ak ngalalutik chetetat koyai ak kandoindenyi. Netai President Obama eng kandoik tugul chekimi eng kandoinatet nebo emetab Amerika korutechi Cuba kotakondoi kongete kenyit nebo 1959 yekingobit walutik eng kandoinatet, nekiit kotoigei kenyisiek chechang chebo chemarget. Kangong'ololi eng kapkiyok nebo Amerika nekokiyat kogeny eng Havana, komwa kole rutoitonyi koba kamanut mising. Korutechi kora komosta nebo old city. Tetat kotuiyo Obama ak Raul Castro, ago matuitos ak kandoindet nekiindochini walutikab kandoinatet, ne kikowo kamung'et Fidel Castro.* |

## KIAMBATISHO 2

### Hojaji kwa Mtafsiri

(a) Ulihitimu lini mafunzo ya uanahabari?

Agosti 2009

(b) Je, ulihitimu katika kiwango gani?

Stashahada (Diploma)

(c) Kando na uanahabari, kuna taaluma nyinginezo ulizosomea? Kama ndiyo, ni zipi?

Ualimu (Stashahada – Chuo cha Ualimu cha Kagumo)

(d) Umekuwa mtafsiri wa habari kwa muda gani?

Miaka minne (Tangu 2012)

(e) Je, habari zinazosomwa katika kituo hiki zinatafsiriwa kutoka lugha ipi/zipi?

Kiswahili (habari za Kimaeneo) Nyinginezo kutoka Kiingereza (hasa habari za michezo na habari za Kimataifa)

(f) Ni hatua zipi zinazofuatwa katika ukusanyaji wa habari hadi kusomwa?

(i) Kupokea ripoti kutoka nyanjani hasa katika Kiswahili.

(ii) Kuhaririwa.

(iii) Kutafsiriwa katika lugha za Kienyeji katika vituo mbalimbali.

(iv) Kusomwa katika vituo husika.

(g) Je, ni aina zipi za tafsiri mnazotumia kutafsiria taarifa za habari?

(i) Tafsiri mawasiliano.

(ii) Tafsiri huru.

(iii) Tafsiri maana.

(iv) Tafsiri ya moja kwa moja

(h) Ni matatizo yepi mnayokumbana nayo katika tafsiri za taarifa za habari?

(i) Muda mfupi wa kutafsiri.

(ii) Kukosa visawe vya dhana fulani.

(iii) Kushindwa kutafsiri nahau/misemo/lugha ya kitamathali.

(iv) Kiswahili na Kikipsigis kutofautiana kiisimu

(v) Tofauti za kitamaduni kati ya Kiswahili na Kikipsigis.

(i) Je, matatizo haya yanasababishwa na nini?

(i) Sayansi na teknolojia - kuwa na dhana mpya zilizo ngumu kutafsiriwa.

(ii) Upungufu wa muda.

(iii) Ukosefu wa umakini ifu wakati wa kutafsiri.

(j) Ni mikakati ipi mnayotumia kukabiliana na matatizo mliyotaja?

(i) Kutajirisha stadi za tafsiri - kutokana na uzoefu na utafiti.

(ii) Kutumia maelezo panapokosekana kisawe.

(iii) Kufuta dhana inayotatiza kama haina athari kubwa katika uwasilishaji wa maana.

## KIAMBATISHO 3

## Orodha ya Vituo vya Redio Nchini Kenya

1. Radio Citizen - 106.7
2. Mbaitu FM - 92.5
3. **KBC Kiswahili - 92.9**
4. **Kitwek - 98.0**
5. Milele FM - 99.7
6. Muuga FM - 88.9
7. Q FM - 94.4
8. Lake Victoria FM - 92.1
9. Jambo FM - 97.5
10. Radio Star - 105.9
11. Inooro FM - 98.9
12. Bahari FM - 94.2
13. KISS FM - 100.3
14. Kaya FM - 95.9
15. Kameme FM - 101.1
16. Kisima - 89.7
17. Ghetto Radio - 89.5
18. Risala - 96.7
19. Coro FM - 95.7
20. Capital FM - 98.4
21. Ramogi FM -107.1
22. Classic FM - 105.2
23. West FM - 94.9
24. Musyi FM - 102.2
25. Kass FM - 89.1
26. Easy FM - 96.3
27. Chamgei FM - 90.4
28. KBC English - 95.6
29. BBC - 93.9
30. Radio Maisha - 102.7
31. Sayare Radio - 102.9
32. Egesa FM - 103.4
33. Mulembe FM - 97.9
34. KBC North Eastern - 87.7
35. Bibilia Husema - 90.7
36. Radio One - 97.1
37. Syokimau FM - 88.7

38. Injili FM - 103.7
39. Minto - 101.7
40. Pwani FM - 104.7
41. Baraka FM - 95.5
42. Wimwaro
43. Metro FM - 101.9
44. Imani FM - 88.8
45. Nam Lolwe FM -97-3
46. Sauti ya Mwananchi - 100.9
47. Hope FM - 93.3
48. Sahara FM - 106.4
49. Jesus Is Lord - 105.3
50. Mambo FM - 91.7
51. Anguo
52. Ghetto FM - 89.9
53. Radio Waumini - 88.3
54. Frontier FM
55. Radio Salaam
56. Radio Djibouti
57. Sheki FM
58. Uptown - 91.1
59. Radio Rahma
60. Radio Ethiopia
61. Family
62. Hot 96 - 96.0
63. Homeboyz Radio - 103.5
64. Mururi 107.3
65. Mata FM
66. Hosana
67. MMUST FM
68. Sifa FM
69. KBC Eastern
70. East Africa FM
71. Radio Maria
72. Radio Mwiriama
73. X FM Rock - 105.5
74. Iqra FM - 95.1
75. Radio Simba
76. Voice of America
77. Fish FM
78. Mwanendu FM

79. KBC Western
80. Amani FM
81. Kill FM
82. Kangema FM
83. Radio Free Africa (RFA)
84. Rehema
85. Light & Life
86. RFI - 89.9
87. Radio Mang'elete
88. Radio Umoja
89. Best FM
90. Cloud FM
91. Bahasha
92. Radio Star
93. ECN
94. Maendeleo
95. RTD Tanzania
96. Rock Mambo
97. Sema Radio
98. Deutchse-Welle
99. Step FM
100. Mwangaza
101. Sound Asia FM
102. East FM
103. Radio China International
104. Turkana FM
105. Radio Pamoja
106. KBC Central
107. TBC TZ
108. Mandeq
109. Touch FM
110. Koch FM
111. Triple-A
112. Irib
113. CRI
114. Lokichogio FM
115. Neema FM